

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Thelathini na Mbili - Tarehe 21 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. OMAR S. CHUBI (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO) - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:**

Maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. AISHA P. MAGINA – MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni yake Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 304

### **Tume ya Kushughulikia Madai ya Walimu**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA (K.n.y .MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliunda Tume ya kuchunguza madai ya walimu wa shule za msingi ambao walikuwa wanalamika kuwa hawalipwi mishahara na mafao yao kwa muda mrefu bila sababu za msingi:-

(a) Je, ni walimu wangapi wa Wilaya ya Serengeti wamelipwa mishahara na marupurupu yao hadi sasa na ni kiasi gani cha fedha kimelipwa?

(b) Je, ni walimu wangapi wa Wilaya hiyo hawajalipwa hadi sasa na Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha kuwa walimu hao wanlipwa madai yao mapema iwezekanavyo?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kisheria kwa wale waliofanya makosa ya kuiba mafao na mishahara ya walimu nchini ikitajwa kwa kila Mkoa kuanzia mwaka 2001 – 2005?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mhesimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati ninajibu swali Na.237 la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, tarehe 12/7/2005 nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli Serikali iliunda Tume ya kuchunguza madai mbalimbali ya walimu wa hsule za msingi zoezi ambalo limekamilika. Hivi sasa Serikali imeanza kuwalipawalimu madai yao mbalimbali kwa kadri yaliyohakikiwa na Tume. Madai ya walimu 741 yaliyohakikiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti yanafikia kiasi cha shilingi 145,692,296/=. Hadi sasa walimu 417 wamelipwa madai yao mbalimbali ya jumla ya Sh.124,000,783/= yakiwa na mchanganuo ufuatao:-

- Masomo - Shs. 14,197,130/=;
- Uhamisho - Shs. 90,102,574/=;
- Likizo - Shs. 638,100/=;
- Matibabu - Shs. 10,267,979/=;

- Posho ya ajira - Shs. 8,795,000/=;

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaendesha zoezi la malipo kwa watusika kwa uwazi kwa kutangaza majina ya wanaolipwa katika magazeti.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya walimu 324 wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti hawajalipwa malimbikizo yao ya mishahara yanayofikia Shs.21,691,513/=. Madai haya yanashughulikiwa na Hazina. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge Wanyancha kwamba madai hayo yatalipwa na Serikali kwa kuwa yamehakikiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, madai ya walimu kwa upande mmoja yametokana na Watendaji kutozingatia Sheria za fedha na taratibu zingine zinazotakiwa. Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kuzingatia Bajeti yake kila mwaka ili kuona kama inakidhi matakwa mbalimbali kama vile uhamisho wa watumishi wake na kadhalika. Watendaji ambao kwa makusudi hawakuzingatia Sheria za fedha wamekwishachukuliwa hatua mbalimbali za kisheria kama vile kufunguliwa mashitaka, kupata karipio kali, kusimamishwa kazi au kuvuliwa madaraka.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa malipo ya watumishi mbalimbali wakiwemo walimu ulitokea kwa karibu Halmashauri zote nchini na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kwa Halmashauri zote.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imechukua hatua nzuri kabisa ya kuwalipa walimu wote waliokuwa wanadai. Lakini Serikali inakiri kuwa kuna walimu karibu 300 katika Wilaya ya Serengeti hawajalipwa na katika sehemu nyingine ya nchi walimu wengi bado hawajalipwa. Je, Serikali inasema nini kwa hao walimu ambao bado wanaendelea kudai Serikali yetu, watalipwa lini? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO ( K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi hapa kwamba wale walimu zaidi ya 300 wa Wilaya ya Serengeti ambao bado hawajalipwa, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kuwalipa na nimesema hapa kwamba kwa vile madai yao sasa yamehakikiwa Hazina itawalipa kwa uwazi kama ambavyo wenzao wengine wamelipwa. Hivyo hivyo, hata kwa walimu wengine wa Wilaya zingine ambao bado hawajalipwa, azma ya Serikali ni kuwalipa wote kwa haraka kadri iwezekanavyo mara baada ya madai yao kuhakikiwa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa walimu wote nchini wamefurahishwa sana na kitendo cha Serikali kuunda Tume kufuatilia madai yao na mafao yao; na kwa kuwa sasa hivi Serikali inaanza kuwalipa kwa awamu kama ilivyozungumzwa pamoja na walimu wa kule Morogoro na katika maeneo mengine nchini. Je, sasa Serikali baada ya

kumaliza zoezi hilo la awamu ya kwanza la kuwalipa walimu, lipo zoezi lingine litafuata siyo karipio kali tu, kuwachukulia hatua za *Ki-financial regulation* kwa wale walioleta matatizo kusababisha walimu kukosa fedha hizo; kwa kuwa Serikali ina macho kama chandarua itawajua tu wako wapi, wamefanya nini na Serikali itawafanya nini sasa hivi? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina uwezo wa kushughulikia matatizo yote na ndiyo maana hata hii kero ya kuwalipa walimu imeshughulikiwa sasa. Lakini nataka tu niongeze kwamba kwa wale wote waliozembea na kusababisha kero hizo baadhi yao wameishaanza kuchukuliwa hatua. Kwa mfano, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Lindi, Tabora, Rufiji, Musoma, Meatu, Mkuranga, Kondoa, Mpwapwa, Simanjiro na Maswa tayari yameishasimamishwa kazi kutokana na uzembe walioufanya na wengine wanaendelea kufikishwa Mahakamani. (*Makofi*)

Na. 305

### **Majina ya Mitaa na Namba za Nyumba**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wanaopatwa na matatizo kama ya ajali barabarani, majanga ya moto au kuibiwa wanapowaarifu Polisi hutakiwa waeleze majina ya mitaa na barabara na kutaja namba za nyumba lilipotokea tukio hilo:-

- (a) Je, maeneo yote ya Mijini yana majina ya mitaa na namba za nyumba?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba lawama kwa Polisi za kutofika kwenye matukio haraka siyo zao bali ni za mamlaka Serikali za Mitaa?
- (c) Je, kuna hatua zozote zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba yote ina majina na nyumba zina namba?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Siyo maeneo yote ya Mijini yana majina ya mitaa na namba za nyumba. Kwa mujibu wa Jedwali la kwanza kifungu Na. 83 chini ya kifungu cha 118 cha Sheria Na.7 ya mwaka 1982 Halmashauri za Wilaya zimepewa Mamlaka ya kuipa majina maeneo mbalimbali ya Mijini, barabara na namba za nyumba. Hata hivyo, baadhi ya maeneo Mijini hayana majina ya Mitaa wala namba za nyumba kwa sababu kubwa zifuatazo:-

- (i) Ujenzi holela wa makazi Mijini.
- (ii) Upuuzaaji wa Sheria zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuhakikisha Mitaa inakuwa na majina na nyumba kuwa na namba ni la Mamlaka ya Mji husika hasa Kamati ya Uchumi, Maendeleo ya Jamii na Mipango ambayo ndiyo yenyewe jukumu la moja kwa moja la kusimamia, kuelekeza na kuhakikisha kuwa majina ya Mitaa na namba za nyumba imekamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa kiwango fulani maeneo yasiyokuwa na majina ya mitaa wala namba za nyumba matukio yaliyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge yanapotokea yanaweza kabisa yakasababisha Polisi kuchelewa kufikia katika eneo la tukio. Hata hivyo, Polisi wanaweza pia kuchelewa kufikia katika maeneo hayo kutokana na sababu mbalimbali kama uhaba wa Askari, matatizo ya vyombo vya usafiri na kadhalika.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa maeneo yale ambayo yana mitaa Halmashauri zilikwishaagizwa na naendelea kuziagiza kuhakikisha zinaweka majina ya mitaa na namba za nyumba kwa mujibu wa Sheria. Kwa upande wa maeneo ambayo yamejengwa kiholela Serikali imeendelea kuwasisitiza wananchi kuhakikisha kwamba angalau nyumba zao zinawekwa namba. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya Kimataifa kama vile *HABITAT* inaendelea kuyafanyia marekebiso maeneo ya makazi yaliyojengwa kiholela kwa kuweka barabara katika maeneo husika, jambo ambalo 1 itarahisisha uandikishaji wa majina ya mitaa na hivyo kupunguza kero inayoelezwa na Mheshimiwa Mbunge. Vilevile hatua hii inaziwezeshe Halmashauri zetu kukusanya mapato ya majengo kwa urahisi na pia kuwezesha wananchi kufika kwenye maeneo hayo kwa urahisi.

**MHE. WILLIAM H.SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa namba za nyumba na majina ya barabara yanahuksika vilevile kwenye barabara kuu. Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuangalia upya majina ya barabara na umbali mathalani barabara inayotoka Chalinze kwenda Segera mpaka Tanga vibao vyake vinaonyesha Segera – Tanga, lakini havionyeshi kwamba njia hiyo hiyo ni ya kwenda mpaka Moshi au Arusha. Katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya

Chalinze mpaka Chalinze Wajenzi wa barabara wamebadilisha wameandika umbali wa Chalinze kwenda Segera, lakini ukishamaliza hicho kipande kilichorekebishwa unaingia Segera-Tanga. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atoe ombi hili kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ili arekebishe hilo kwa ajili ya usafiri wa watalii.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimeeleza katika majibu ya msingi hapa kwamba mamlaka ya kuweka namba za nyumba na majina ya mitaa iko chini ya mamlaka ya Halmashauri zinazohusika. Lakini hili la barabara za umbali wa eneo pamoja na barabara zinakokwenda nadhani tumelipokea na tutalifikisha kwenye Mamlaka zinazohusika ili liweze kuzingatiwa ipasavyo.

Na. 306

**Serikali Kusaidia Sekondari za Binafsi**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. MONICA N. MBEGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshatangaza ya kuwa kuanzia Januari, 2005 ada za Sekondari zilizo chini ya Serikali zitakuwa nusu ya ada iliyoko sasa:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu kusaidia Sekondari za Binafsi ili wazazi wasio na uwezo waweze kuwapeleka watoto katika shule hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo kuu ya MMES 2004-2009 ni kuongeza vjana wa Tanzania wanaosoma na kuhitimu Elimu ya Sekondari wakiwa na matokeo mazuri ya kujifunza kutoka vijana 345,000 mwaka 2003 hadi vijana 2,000,000 ifikapo mwaka 2010 na wahitimu wasiopungua 500,000 kila mwaka. Ili kuwezesha kufikia malengo hayo, Serikali inautambua pia mchango wa sekta binafsi katika kutoa elimu nchini. Katika kutekeleza MMES, Serikali imechukua hatua mbalimbali za makusudi za kuisaidia sekta hiyo, ili iweze kuboresha shule zake. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- Kutoa ruzuku ya uendeshaji ya Sh.10,000/= kwa kila mwanafunzi kwa shule za Sekondari ambazo sio za kibashara na sio Seminari kwa ajili ya kununulia vitabu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia.
- Kutoa ruzuku ya maendeleo kwa mwenye shule aliyeidhinishwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa ajili ya ujenzi wa shule za wanafunzi wenyewe ulemavu kwa viwango sawa na ile inayotolewa kwa ajili ya Sekondari za Serikali zinapojengwa na wananchi. Viwango hivyo ni shilingi milioni 7.0 kwa darasa na shilingi milioni 9.0 kwa nyumba ya mwalimu.
- Kuendelea kutoa huduma ya usajili wa shule, Ukaguzi wa shule, kuiandaa walimu na mitihani ya Kitaifa kwa ajili ya shule zote.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zina lengo la kuziimarisha shule za Sekondari zisizo za Serikali kwa kuzifanya zitambulike na ziaminike. Kwa kuwa “kupanga ni kuchagua” kwa sasa Serikali imeamua kuzingatia misaada yake kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo na Uendeshaji kwa wananchi wanaojenga Sekondari ngazi ya Tarafa au Kata kwa kuamini kuwa wananchi wengi zaidi watanufaika na shule hizo ambazo kisheria zitakuwa Sekondari za Serikali zinazojengwa na wananchi.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa watoto wengi wa Tanzania wanaosoma katika shule hizo za binafsi si kwamba walifeli kwa kutokuweza kupata elimu ya sekondari katika shule za sekondari za Serikali, lakini hiyo inatokana na ufinyu wa shule za sekondari za Serikali katika maeneo yetu; na kwa kuwa Serikali imeamua kutoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi ama kwa ajili ya maendeleo ya shule hizo na si ada ya kuwasaidia watoto hao wa Kitanzania waliofaulu na kukosa nafasi katika shule za Sekondari za Serikali. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kufikiria kutoa ruzuku sasa kwa ajili ya ada ili kuwasaidia watoto hao ambao wanakosa nafasi katika shule za Sekondari za Serikali waweze kupata elimu kulingana na wenzao ambao walipata nafasi katika shule za Sekondari za Serikali? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi shule za binafsi zinatoa mchango mkubwa kuchukua wale wanafunzi ambao wamefaulu darasa la saba, lakini kwa sababu ya nafasi chache kwenye shule za sekondari za Serikali hawakwenda kwenye hizo shule za sekondari za Serikali na jana hapa tulijibu swali.

Kwa mfano, mwaka jana kuna watoto 100,008 ambao walifaulu darasa la saba, lakini hawachaguliwa kwenda kwenye shule za sekondari za Serikali kutokana na ufinyu wa nafasi. Kwa hiyo, hao wote karibu walichukuliwa na shule za binafsi na kwa sababu hiyo ndiyo maana sasa Serikali imeanza kutoa ruzuku. Kwa sababu huko nyuma ilikuwa haisaidii chochote katika shule zisizokuwa za Serikali. Kwa mwaka huu wa fedha ndiyo

Serikali imeanza walau sasa kuanza kutoa ruzuku ni hatua muhimu na kubwa na mbele ya safari kama hali ya mapato ya Serikali yataongezeka hilo linaweza likafikiriwa.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza. Serikali ilivyoamua kutoa shilingi 10,000/= kwa kila mwanafunzi kwa kusaidia shule hizo za binafsi iliweza kuangalia bei za vitabu au bei za vifaa ya sayansi na kuona kwamba vina bei kubwa. Je, isingekuwa vyema Serikali ikaongeza fedha kidogo kwa vitabu au ikatoa vitabu vyenyewe kuwasaidia watoto yaani kiasi kadhaa cha vitabu kuliko shilingi 10,000? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba gharama halisi za vitabu na vifaa mbalimbali vinavyotakiwa kufundishia haviwezi kukidhiwa kwa hizi shilingi 10,000/= ambazo Serikali inatoa kwa kila mwanafunzi.

Lakini kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba Serikali inatambua mchango wa shule za binafsi na huu ni mwanzo wa kuanza kuwasaidia na kiasi cha shilingi 10,000/= kimetolewa kama kianzio.

Lakini mbele ya safari kama mapato ya Serikali yataongezeka nia kusema kweli ni kuzisaidia shule za binafsi ziwe na vifaa vya kutosha na vitabu vya kutosha ili elimu inayotolewa katika shule za binafsi iwe sawasawa na ile inayotolewa katika shule za sekondari za Serikali.

Na. 307

#### **Majanga ya Moto kwenye Majengo ya Ofisi za Serikali**

**MHE. ARIDI M. ULEDI (K.n.y. MHE. IBRAHIMU W. MARWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa siku za hivi karibuni kumekuwepo na matukio mengi ya mara kwa mara ya majanga ya moto nchini yakiwemo yale ya kuungua moto majengo ya Ofisi za Serikali na za wananchi kama vile, jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, *NASACO*, *NIC Investment*, na mengine kama yale ya kuungua kwa meli iliyokuwa inashusha shehena ya mafuta Musoma; na kwa kuwa matukio hayo yamesababisha uharibifu mkubwa wa mali za Serikali na za wananchi pamoja na kupoteza maisha ya wananchi wetu; na kwa kuwa kumeendelea kuwepo kwa kauli mbalimbali za vitisho za kutaka kulipua majengo mengine mbalimbali kwa moto au kwa mabomu yakiwemo yale ya Benki ya *CRDB*, Ushirika na kadhalika:-

- (a) Je, Serikali imechukua hatua gani za kukabiliana na hali hizo kama tahadhari kwa matukio ya aina hiyo, hasa kwa kuangalia mfano wa nchi jirani ya Uganda ambayo imojiimarisha kuthibiti majengo na maeneo yenye mikusanyiko?

(b) Je, Serikali inatambua na kuzingatia jukumu lake la msingi la kulinda maisha na mali za wananchi, badala ya kusingizia kubinafsishwa kwa huduma hizo kwa kampuni za watu binafsi kama vile *Knight Support Group* ambao lengo lao kuwa ni biashara kuliko huduma?

(c) Je, Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika wa kuimarisha vikosi vya Zimamoto kwenye Halmashauri zetu ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Musoma ili kujenga uwezo wa kupambana na majanga hayo?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa shughuli za Zimamoto na uokoaji nchini zinafanywa kwa mujibu wa Sheria Na.3 ya mwaka 1985. Zipo pia Kanuni; ikiwemo ile ya mwaka 2000 inayositisiza umuhimu wa tahadhari na kinga ya moto kwenye majengo, kumbi za burudani, viwanda,mashule, mahospitali, vituo vya mafuta na vyombo vya usafiri vya nchi kavu na majini. Baada ya vyombo hivyo kukaguliwa hutolewa cheti kuthibitisha kuwa vimekaguliwa.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa kukabiliana na majanga ya moto ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- Kufanya ukaguzi wa kuwepo vifaa vya kuzima moto na pia kusisitiza juu ya umuhimu wa kuchukua hatua za tahadhari ya moto.
- Kutoa elimu kwa umma kuhusu jinsi ya kutumia vifaa vidogo vidogo vya kuzimia moto na kuhakikisha kuwa kila jengo la Ofisi linakuwa na watu maalum mwenye ujuzi wa kuzima moto (*Fire House Warden*).
- Serikali inatekeleza mkakati wa kuhakikisha kuwa kila eneo la Wizara za Serikali, Viwanda, majengo marefu, mashule, Vyuo pamoja na maeneo yote ya hatari kwa moto, wahusika wanajenga visima vya maji vya akiba ili kutumiwa na wazimamoto endapo janga la moto litatokea.
- Kuwaelimisha na kuwaelekeza wanaojenga majengo mapya kuwa na ving'amuza vya moto (*Fire Alarm and Detectors*) na njia za dharura (*Fire Escape Stair Cases*) kwenye maghorofa marefu au majumba yenye mikusanyiko ya watu.
- Katika kupambana na moto kwenye majengo marefu, Serikali imepatia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam gari lenye uwezo wa kuzimamoto kwenye majengo marefu mpaka kwenye ghorofa ya 18.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuzingatia jukumu lake la msingi la kulinda maisha na mali za wananchi dhidi ya ajali za moto. Kutokana na kutambua hivyo, Serikali imehamasisha ushirikiano wa karibu wa vikosi vya Zimamoto vya Bandari, Viwanja vya Ndege, Halmashauri za Miji na makampuni ya watu binafsi ya Zimamoto.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia thabiti ya kuziwezesha Halmashauri za Miji ukiwemo Mji wa Musoma kuimarisha vikosi vyao vya Zimamoto kwa kuzipatia vitendea kazi. Katika kutekeleza nia hiyo, Serikali imekuwa inatoa magari ya Zimamoto kwa Halmashauri za Majiji na Miji kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 2003/2004 magari ya zimamoto yaliyotolewa kwa Jiji la Dar es Salaam, Manispaa za Temeke, Ilala, Kinondoni na Jiji la Mwanza.

(ii) Mwaka 2004/2005 Halmashauri za Miji tisa yaani Tanga, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Iringa, Tabora, Sumbwanga, Musoma na Songea zilipatiwa fedha za kununua magari. Taratibu zote za kununua magari hayo zimekamilika na yataanza kuingia nchini wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha 2005/2006 katika Bajeti yetu tumeweka fedha kwa ajili ya kununua magari kwa Halmashauri za Miji saba na juhud hizi zitaendelea mpaka Miji yote ipate magari ya zimamoto.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa vifaa hivyo ambavyo vinatakiwa kudhibiti majanga kama hayo ya moto vinauzwa kwa bei ghali sana. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa vifaa hivyo vinapunguzwa bei ili kuwawezesha wananchi na makampuni mbalimbali kuweza kuvinunua na kuweka kwenye nyumba zao au kwenye kampuni zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, yale magari ya zimamoto kweli ni aghali sana kuanzia milioni 300, milioni 400 mpaka bilioni moja. Ndiyo maana hata Halmashauri nyingi zenyewe haziwezi kununua. Serikali Kuu ndiyo inayonunua na kuapelekea.

Mheshimiwa Spika, lakini hivyo vifaa vidogo vidogo tatizo si aghali, tatizo tu ni wananchi kuelewa kwamba ni vitu vya muhimu kuna navyo. Uelewa ndiyo tatizo kubwa. Kwa mfano, unaweza kukuta mtu ana gari lenye thamani ya shilingi milioni 60, lakini kifaa cha kuzimia moto cha shilingi 40,000/= ambacho kitamsaidia kuzima moto kama gari lake litawakaa moto hana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii kuwahimiza na kuwaelimisha Watanzania wenzangu kwamba ni muhimu kabisa tuwe na vifaa vyatuzimia moto katika nyumba na katika magari na bei yake siyo kubwa sana ikilinganishwa na thamani ya kile kitu ambacho unacho na unataka kukilinda.

Na. 308

### **Vyombo vyatuzimia OCD**

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA (K.n.y. MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa *OCD* wa Wilaya ya Ngorongoro ni mionganini mwa ma-*OCD* wachache nchini ambao hawana vyombo vyatuzimia:-

- (a) Je, ni ma-*OCD* wangapi nchini ambao hawana vyombo vyatuzimia?
- (b) Kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la Wilaya ya Ngorongoro na mazingira magumu na mauaji ya mara kwa mara yanayosababishwa na ama vita vyatuzimia kikabila au ujambazi unaofanywa na watu wenye asili ya Kisomali. Je, ni lini Serikali itatoa usafiri wa kuaminika kwa *OCD* Wilayani Ngorongoro?

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew – Ole Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ma-*OCD* wote nchini wana magari ila baadhi ya magari ya ma-*OCD* hao yamekuwa makuu kuu na yanahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Kwa mfano hilo gari la *OCD* wa Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, tatizo la vyombo vyatuzimia usafiri vyatuzimia hakika kwa ma-*OCD* wote nchini linatazamiwa kupatiwa ufumbuzi mwaka huu ambapo tayari Serikali imeshanunua magari 215 ambayo yataanza kusambazwa wakati wowote kuanzia sasa.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Pia nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba yale magari ambayo yaliagizwa tangu mwaka jana sasa yanaanza kusambazwa. Tumeambiwa kwamba yataanza kusambazwa.

Kwa sababu ni mwaka mzima yameanza kusambazwa tuambewe ni lini sasa?  
(*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ilikuwa kupata fedha za kununua hayo magari, kazi ambayo imeshakamilika. Kwa hiyo sasa kazi ya kuyasambaza ni kazi ndogo kabisa nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba magari haya yatakuwa katika Wilaya zetu mapema kabisa kabla ya uchaguzi unaokuja. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika kituo hicho cha Ngorongoro ambacho *OCD* wake hana gari basi linafanana kabisa na Kituo cha Kibiti ambacho hakuna gari kabisa na uhalifu wote unatendeka upande huo wa Kibiti kuliko kule Utete. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu magari yaliyokuwa yanataka kusambazwa na Kibiti pia kupeleka gari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, haya matatizo mawili hayafanani kwa sababu Ngorongoro tunashughulika na gari la *OCD* (Mkuu wa Polisi wa Wilaya). Lakini kituo cha Kibiti Mkuu wake pale sio *OCD*. *OCD* yuko Makao Makuu ya Wilaya kule Utete. Kwa hiyo hivi ni vitu viwili tofauti. Sasa hivi tunagawa magari kwa Ma-OCD (Makao Makuu ya Wilaya). Tukimaliza tatizo hilo tunao mpango vile vile siku za usoni kutazama vituo vingine vikubwa ambavyo viko nje ya Makao Makuu ya Wilaya kama cha Kibiti.

Na. 309

#### **Maji ya Ziwa Chipwalapwata**

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME (K.N.Y. MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa, niliiomba Serikali ipeleke wataalam wake kwenye Ziwa Chipwalapwata katika Kijiji cha Kiwengulo kuona uwezekano wa kuyapeleka maji ya ziwa hilo katika Kijiji cha Kiromba na hatimaye kuyasambaza kwenye Tarafa ya Nanyamba na Kata ya Kiromba na Mnima kwa bomba:-

- (a) Je, Serikali imeshafanya hivyo;
- (b) Kama wataalam walipelekwa au la. Je, hatua yake ikoje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D.NTAGAZWA)(K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitekeleza ombi la Mheshimiwa Mbunge kwa kuwapelekea wataalamu wake kwenye Ziwa Chipwalapwata lililoko katika Kijiji cha Kiwengulo Wilaya ya Mtwara Vijijini, ili kuona uwezekano wa kulitumia Ziwa hilo kama chanzo cha maji kwa ajili ya Kijiji cha Kiromba, na vijiji vingine vya Tarafa ya Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, wataalam kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara na Halmashauri ya Mtwara Vijijini walifanya uchunguzi huo kati ya tarehe 17/09/2004 na tarehe 29/09/2004. Uchunguzi huo ulihusu upimaji wa urefu, upana na kina cha Ziwa na ulilenga kujua kiasi cha maji kilichokuwa ndani ya Ziwa hilo. Kadhalika wataalam hao walipima urefu wa Ziwa hilo kutoka usawa wa bahari.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya upimaji uliofanywa yamebainisha kuwa ujazo wa Ziwa Chipwalapwata ni meta za ujazo 1,270,000 tu. Ujazo huu wa maji unaweza kutosheleza mahitaji ya Kijiji cha Kiwengulo pekee chenye watu wapatao 1,700 endapo chanzo hicho kitaendelea kutunzwa vizuri. Vile vile utafiti huo ulibaini kwamba Ziwa la Chipwalapwata liko mita 21 kutoka usawa wa bahari chini kidogo ya usawa wa wastani wa Kijiji cha Kiwengulo, na hivyo maji hayo yatahitaji kusukumwa kwa pampu umbali wa kilomita 2 ili kufika kijijini.

Mheshimiwa Spika, ili kutafuta njia ya kuondoa tatizo la maji katika Kijiji cha Kiromba utafiti wa maji chini ya ardhi ulifanyika mwaka 2003 na kuainisha sehemu ya kuchimba kisima kirefu. Kisima hiki hakijachimbwa kwa sababu Serikali hajapata fedha ya kutekeleza kazi hiyo ili kuwapatia wananchi wa Kiromba maji safi. Vile vile mwaka 2001 Shirika la *CONCERN* lilichimba kisima cha maji katika Kijiji cha Mnima, lakini kisima hiki hakikutoa maji ya kutosha. Serikali kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali, wakiwemo *CONCERN* inaendelea kutafuta vyanzo vya uhakika vya maji kwa ajili ya Kata za Kiromba na Mnima katika Tarafa ya Nanyamba.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamajibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini kwa kuwa Ziwa la Chipalapwata baada ya utafiti imeonekana kwamba halitoshelezi kupatia maji Tarafa ya Nanyamba na kule Mnima. Na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba Tarafa ya Nanyamba huenda wakapatiwa maji kutoka katika Mradi wa Maji wa Makondeko kule Newala. Je, mpango huo Serikali umefikia wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MHE. ARACDO D.NTAGAZWA:** Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi sehemu ya (c) nimesema kwamba Serikali inaendelea kutafuta na kushirikiana na wahisani mbalimbali ili kufanikisha mradi wa kuwapatia wananchi maji safi na salama. Sasa juhudhi hizo zinajumuisha pia uwezekano wa kupata maji na kuwapatia wananchi kutoka Ziwa

Makondeko au Mradi wa Maji wa Makondeko. Kwa hiyo, juhudini za Serikali zinaendelea. (*Makofi*)

Na. 310

### **Matatizo ya Maji Kata ya Shume**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni dhahiri kwamba, Kata ya Shume katika Tarafa ya Mlalo ina matatizo makubwa ya ukosefu wa Maji; na kwa kuwa, Serikali katika kujibu swali langu kuhusu Kata hiyo kupatiwa Maji aliahidi kuchangia shs. 12,000,000/= kwa ajili ya kuwapatia Maji wananchi wa Kata hiyo kwa kuwachimbia visima vifupi kabla ya mpango kabambe wa Maji katika Kata hiyo uitwao *Manolo Group* kuanza:-

- (a) Je, fedha hizo zilitolewa na kupelekwa Lushoto lini?
- (b) Je, ni kweli kwamba, visima hivyo vilichimbwa, na kama jibu ni ‘ndiyo’ ni vingapi, katika vijiji gani kwa majina?
- (c) Je, mradi wa Maji wa *Manolo Group* utaanza katika mwaka huu wa fedha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)(K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Kata ya Shume iliyopo katika Tarafa ya Mlalo ina tatizo kubwa la maji. Kata hiyo yenye wakazi wapatao 4,500 ina mahitaji ya maji ya mita za ujazo 870 kwa siku, wakati maji yanayopatikana au kwa Kiswahili cha sasa yanayozalishwa ni mita za ujazo 158 kwa siku. Uhaba wa maji katika Kata hii unatokana na ongezeko la watu na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji miti ovyo katika maeneo ya chanzo cha maji cha mto mdogo wa Gologolo.

Kutokana na tatizo hilo la maji, Serikali iliahidi kuchangia shilingi 12,000,000 kwa ajili ya kuchimba visima vifupi katika Kata ya Shume kama hatua ya dharura. Fedha hizo zimetumwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto mwezi Juni 2005 na Halmashauri hiyo inakamilisha maandalizi ya kuchimba visima kama Serikali ilivyoahidi. Ni matumaini yangu kwamba vijiji ambavyo vimejiandaa kushiriki katika ujenzi na umilikaji wa miradi vitapewa kipaumbele katika kutumia fedha hizo, ili visima hivyo viweze kuchimbwa haraka na kutunzwa vyema. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kuwa uchimbaji na gharama husika zinazingatia kazi zilizopangwa na kwa ukamilifu sahihi.

- (b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba fedha zilichelewa kupatikana na hivyo kutumwa hivi karibuni, yaani mwezi wa Juni, 2005, visima hivyo havijachimbwa kwa sasa. Uchimbaji wa visima vipyta utaongezea uwezo wa upatikanaji wa maji katika Kata hiyo ambayo tayari inavyo visima vifupi katika vijiji vya Nywelo (2) na Madala (2). Kadhalika, Kata ya Shume inacho chanzo kingine cha maji katika mto mdogo wa Gologolo. Vyanzo hivyo kwa pamoja vinatoa huduma ya maji katika vijiji vya Gologolo, Nywelo, Mkunki, Gemai, Madala na Manolo katika Kata hiyo. (*Makofi*)
- (c) Mheshimiwa Spika, makisio ya kujenga mradi wa maji wa ‘*Manolo Group*’ yanakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi 920 milioni. Kutokana na mahitaji hayo makubwa ya fedha, Serikali haina uwezo wa kugharamia ujenzi wa mradi huo kwa sasa. Lakini Serikali itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wahisani, ili kujenga mradi huo.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwanza majibu ya Waziri ni mazuri kiasi lakini hayako sahihi sana. Kwa sababu Kata ya Shume kwanza haina watu 4,000 ina zaidi ya watu 21,000. Kwa hivyo hilo ni moja kwamba watu ni wengi na hali ya upungufu wa maji ni mkubwa. Sasa swali. Je, pamoja na kwamba Serikali imesema sasa hivi haina fedha inahangaika kutafuta fedha lakini Serikali na Wizara hii inatambua kwamba Kata hii ni sawa sawa na baadhi ya Kata ambazo ziko maeneo kame kabisa katika nchi yetu. Naomba kwa sababu hiyo basi Serikali iongeze jitihada zake za kutafuta fedha kwa ajili ya mradi wa *Manolo Group* ambao nilipojibiwa swali langu la pale majuzi niliambiwa mradi huo ungeweza kuanza mwezi huu wa Julai. Je, Serikali ilikuwa inasema kweli au ilikuwa inasema uongo? (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu takwimu za wakazi wa Kata ya Shume tulivyotoa majibu ya msingi kwamba kuna wakazi 4,500 na Mheshimiwa Mbunge anasema wako wakazi 20,000 tunaweza tukatofautiana katika takwimu au hata linawenza likatokea kosa la uchapaji, hilo la kwanza.Pili, katika majibu yaliyotangulia Serikali iliwhahi kusema mradi huu wa *Manolo Group* ungeweza kuanza kutekelezwa mwezi Julai kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Na kwa kuwa katika jibu letu la msingi tumesema jitihada zinaendelea. Ningependa niseme wakati Serikali inafanya juhudzi za kutekeleza ahadi zake kama tunatarajia kupata msaada kutoka kwa wahisani huwa tunakuwa waangalifu sana tusije tukasema kwa yakini kabla hatujapata fedha kutoka kwa wahisani. Kwa hiyo, kati tulipojibu swali lile na sasa inawezekana kabisa katika Wizara yetu ya Maji na Maendeleo ya Mifugo juhudzi zetu za kupata msaada kwa wahisani zikawa zimefikia mahali pazuri na kwa maana hiyo mradi ukaweza kutekelezwa kwa kipindi hiki na kwa uhakika Serikali ikawa haikusema uongo kama anavyodai. (*Makofi*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Kata ya Shume iko jirani sana na Kata ya Malibwi na matatizo yaliyoko katika Kata hii ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko Kata ya Shume. Na kwa sababu Serikali ilitangaza kwamba kutakuwa na mpango wa Benki ya Dunia hasa kwa ajili ya kufadhili maji. Serikali inapotamka kwamba inatafuta fedha na inajulikana kabisa wananchi wanateseka je, ni kwa nini vijiji hivi na Kata hizi ambazo zina matatizo zisipewe umuhimu wa kwanza katika mpango wa Benki ya Dunia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MHE. ARCADO D. NTAGAZWA:** Mheshimiwa Spika, matatizo aliyoyleza jirani na Kata ya Shume. Mimi napenda nikubaliane naye kwamba yanashabiiyana yanafanana. Anaposema kwamba kutokana na matatizo haya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wetu na Serikali inajadiliana na Benki ya Dunia ili kuondoa tatizo hili kwa wananchi wetu.

Anachosema vipi Serikali itaweka Kata hiyo ya kwake na tatizo hili tuseme kipaumbele ili ufumbuzi upatikane. Ningependa nielezee kwamba kwanza nina hakika kama tuliyokuwa tunasema jana kwamba tunamshukuru sana kiongozi wetu Rais Benjamin Mkapa kwa kutujengea heshima nchi yetu na kukubalika hata kwa vyombo vya kifedha vya Kimataifa kama Benki ya Dunia kukubali kutukopesha. Juhudi zetu zinaendelea na kama hatujafika mahali tukakubaliana tukawekeana mkataba na Benki ya Dunia itakuwa si sahihi kutamka kwamba sasa tunaanza utekelezaji. Tukamilishe majadiliano ya Benki ya Dunia, fedha zipatikane halafu tutaingia kazini kuwatumikia wananchi wetu.

Na 311

### **Kupeleka Umeme Pwaga**

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikuwa na mpango wa kupeleka umeme Pwaga kutokea Iyenge kwa kutumia fedha za ndani; na kwa kuwa, *TANESCO* haina uwezo huo na wananchi wa Pwaga wamejiandaa kikamilifu kuupokea umeme huo:-

- (a) Je, Serikali inao mpango gani mbadala wa kupeleka umeme Pwaga?
- (b) Je, ni lini mpango huo mbadala utaanza kutekelezwa?
- (c) Je, ni lini umeme utasogezwa kutoka Kibakwe kwenda Chamtumile ambako si zaidi ya umbali wa kilomita 2?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa *TANESCO* haina fedha za kupeleka umeme kwenye vijiji vya Pwaga na Chamtamile,. Upelekaji wa umeme hadi Pwaga utagharimu kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa laini ya msongo wa *33Kv (HT LINE)* wa km 20 tokea Iyenge (iliyopo kwenye laini ya Mpwapwa hadi Kibakwe) utagharimu Tshs. 300,000,000.00.
- Ujenzi wa laini ya msongo mdogo (*LV LINES*) wa km 2 utagharimu Tsh. 18,000,000.00.
- Gharama ya kuweka transfoma 2 za ukubwa wa *50kVA* utagharimu Tshs. 7,000,000.00. Jumla ni Tshs.325,000,000.00.Upelekaji wa umeme hadi Chamtumile utagharimu kama:
- Ujenzi wa laini ya msongo wa *33Kv (HT LINE)* wa km 8 (na sio km 2 kama swalila Mheshimiwa Mbunge linavyosomeka) tokea Kibakwe utagharimu Tshs. 120,000,000.00.
- Ujenzi wa laini ya msongo mdogo (*LV LINES*) wa km 2 utagharimu Tsh. 18,000,000.00
- Gharama ya kuweka transfoma 1 za ukubwa wa *50kVA* utagharimu Tshs. 3,500,000.00. Jumla ni Tshs.141,500,000.00.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali kupitia *TANESCO* hivi sasa ina mpango mbadala wa kupeleka umeme katika vijiji vingi nchini kikiwemo Kijiji cha Pwaga kupitia mpango unaofadhiliwa na Benki ya Dunia uitwao *Energizing Rural Transformation*. Sambamba na mpango wa Benki ya Dunia, uundwaji wa taasisi ya kupeleka Umeme Vijijini pamoja na mfuko wake utaunganisha juhudzi za Serikali za kuharakisha kuwafikishia wananchi wengi, hususan waishio vijijini huduma ya umeme kwa ajili ya kuboresha maisha yao pamoja na kuinua uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mpango huo mbadala unatazamiwa kuanza mwakani 2006.

Kama tulivyoeleza hapo awali vivyo hivyo Kijiji cha Chamtumile kitarajie kupata umeme kwa utaratibu wa *ERT* nilioutaja awali.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza namshukuru kwa jibu lake zuri Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ningependa kuuliza dogo la nyongeza. Je, atakuwa tayari basi kusimamia kwamba mradi

huu una-take off na kwamba vijiji nilivyoviomba vitapata umeme kama alivyosema?  
(*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Profesa Mwaga amekuwa akifuatilia sana miradi hii ya umeme kwenye jimbo lake.

Napenda nimthibitishie kwamba kama nilivyosema mradi huu uko kwenye mpango wa *ERT* na ni matumaini yangu kwamba mradi huo utatekelezwa wakati ukifika.  
(*Makofî*)

**GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Kijiji cha Pwaga kiko karibu sana na Kijiji cha Mgoma na Godegode kilomita 8. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja sasa ya kuangalia uwezekano wa vijiji hivyo vyta Godegode na Mgoma navyo vipate umeme?  
(*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Mwaga wanatoka Wilaya moja ya Mpwapwa na kwa kawaida si rahisi kushughulikia upande mmoja bila ya kushughulikia na upande mwingine.

Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii nitambue jitihada za Mheshimiwa Lubeleje pia katika shughulikia masuala ya umeme na mimi naungana naye kwamba ipo busara ya kuangalia uwezekano wa kupeleka umeme kwenye vijiji ambavyo amevizungumzia katika mradi huu wa *ERT*.

Na. 312

### **Mradi wa Umeme – Lupa Tingatinga**

**MHE. LUCAS L. SELELII(K.n.y. MHE. NJELU E. M. KASAKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wataalam wa *TANESCO* walifanya uchunguzi wa kupeleka umeme kwenye Mji Mdogo wa Lupa Tingatinga na kujiridhisha kuwa Mji huo mdogo unafaa kufikishwa huduma ya umeme; na kwa kuwa, mwaka 1999 viongozi wa *TANESCO* walisema kuwa mradi wa kupeleka umeme Lupa Tingatinga ungeingizwa kwenye bajeti yake ya 2000/2001:Je, hadi kufikia sasa hatua gani imefikiwa, na je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa kutokana na uchunguzi uliofanywa na wataalam wa *TANESCO*, mji mdogo wa Lupa Tingatinga unafaa kufikishiwa huduma ya umeme. Mradi wa Lupa Tingatinga unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi milioni 650.

Kazi zitakazofanyika katika mradi huu ni ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 40, ufungaji wa vipoza umeme vinne (4) vyenye ukubwa wa 50 kVA, ujenzi wa laini ya umeme mdogo yenye msongo wa volti 400 yenye urefu wa kilometra 5. Idadi ya wateja watakaopatiwa umeme chini ya mradi huu inakadiriwa kuwa 200. Kazi ya kupeleka umeme Lupa Tingatinga imeanza kwa kufanya upimaji wa njia ya umeme (*detailed survey*) ambapo njia ya umeme wa kilometra 40 kama nilivyosema awali itajengwa.

Kazi nyingine ambazo zimefanyika ni usimamishaji wa nguzo ambazo zimekamilika kwa asilimia 17 pamoja na usimamishaji wa nguzo mpaka kijiji cha Upendo umbali wa kilomita 8. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti na haswa unaoikabili *TANESCO* ujenzi wa mradi huu haujakamilika. Ni matumaini yetu kuwa mara vifaa vya ujenzi vitakapopatikana *TANESCO* itakamilisha ujenzi wa mradi huu.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pia nashukuru majibu ya Naibu Waziri. Lakini Mheshimiwa Kasaka anakubaliana kwamba vifaa na kila kitu kipo tayari, tatizo ambalo lipo ni lori la kusafirishia hivyo vifaa. Sasa je, ni lini hilo lori litapatikana ili kazi hiyo iweze kuendelea kama ambavyo anasema Mheshimiwa Kasaka? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napata taabu kwa sababu Mheshimiwa Kasaka yeye mwenyewe hayupo hapa kusema maneno ambayo Mheshimiwa Selili amesema. Lakini napenda niseme ili rekodi ziwe sawa sawa tatizo sio lori la kupelekea vifaa, tatizo ni kwamba hakuna vifaa na sisi ndio tunaofahamu.

Kwa mfano hakuna *conductors*. Ndiyo maana nimesema naona shida kwamba maneno haya yanazungumzwa kwa niaba ya Mheshimiwa Kasaka. Lakini napenda nirejee tu kwamba mara vifaa vitakavyopatikana ikiwemo hizi *conductors* basi mradi ule utaendelea kama nilivyosema awali.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza suala dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala hili linafanana na jimbo la Lupa na Mheshimiwa Waziri alijibu swalı hapa Bungeni kuhusu kupeleka umeme katika Kijiji cha Malya na Sumve. Nguzo zipo pale zimewekwa tu tatizo ni nini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nilipata nafasi ya kutembelea ujenzi wa mradi wa Sumve/Malya nikielekea Ukerewe kutazama ujenzi wa mradi wa umeme wa Ukerewe.

Ujenzi wa mradi ule ni kweli kwamba nguzo zimeshasimamishwa lakini umekumbana na tatizo hili hili ambalo niliwahi kulieleza hapa Bungeni wiki hii wakati najibu maswali mengine ya vifaa kama *conductors* ambazo nchi nzima vifaa hivi kwa sasa hivi havipo. *TANESCO* wameagiza na mara vifaa hivi vitakapofika nataka niwahakikishie wananchi wa Sumve kwamba mradi ule utaendelea. (*Makofi*)

Na. 313

**Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi  
Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hutoa Taarifa ya Ukaguzi, na kila mwaka hubaini ufujaji, upotevu na wizi wa fedha za Serikali katika Wizara na Idara zake Mikoani na Wilayani:-

- (a) Je, Serikali inatakiwa ichukue hatua gani pale inapobainika upotevu, ufujaji na wizi wa fedha za Serikali unaofanywa na Maafisa Wahasibu?
- (b) Je, ni Maafisa Wahasibu wa Wizara zipi wamebainika kuhusika na wizi huo, ufujaji na upotevu au kuisababishia Serikali hasara ya fedha?
- (c) Je, Maafisa Wahasibu hao, kama wapo wamechukuliwa hatua gani za kisheria kuhusiana na vitendo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Bakari M. Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, inapobainika kuwa kumetokea upotevu, ufujaji au wizi wa fedha, bila kujali cheo cha mtuhumiwa, hatua zinazochukuliwa ni kwanza kuingiza kwenye kumbukumbu taarifa za tukio hilo. Pili, moja kati ya yafuatayo yanaweza kufanywa kutegemea kiwango cha upotevu:-

(i) Afisa Mhasibu kuunda Tume ya Uchunguzi, na ikithibitika mhusika/wahusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kukata kiasi husika kutoka kwenye mishahara yao. Aidha, ikabidi mhusika/wahusika hufukuzwa kazi.

(ii) Kutoa ripoti kwenye vyombo vya sheria, na kufuatilia mwenendo wa kesi hadi hukumu inapotolewa. Kama mhusika ametiwa hatiani, hukosa haki zote kama vile pensheni, kiinua mgongo na kadhalika, ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali zake ili kufidia hasara iliyotokea.

Pale inaposalia hasara licha ya hatua za kuuza mali, kiasi husika huombewa kibali cha Bunge cha kufutwa kutoka vitabu vya Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, mtumishi akishinda kesi, hurudishwa kazini na hasara huwa ni ya Serikali.(b) Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matukio ya wizi katika sehemu mbalimbali Serikali.

Kuna maafisa wa Serikali kutoka Wizara kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, na vile vile Wizara ya Fedha ambao wamehusika na matukio ya ufujaji na wizi.

Aidha, kuna maafisa kutoka katika Taasisi za Serikali ambapo wizi au ufujaji umetokea. Taasisi hizo ni kama vile *LART*, *TRA* na *NMB*. Vile vile kuna maafisa katika Ofisi za Serikali Mikoani ambao wamehusishwa na masuala ya wizi au upotevu ulioisababishia Serikali hasara.

(c) Mheshimiwa Spika, maafisa wanaohusika wamefikishwa katika vyombo vya sheria kama taratibu zinavyohitaji. Aidha, kufuatia matukio hayo maafisa hao husimamishwa kazi hadi hatima yao itakapo julikana kutoka vyombo vya sheria. Katika kipindi hicho tukiwa tunasubiri kuna baadhi ya watuhumiwa hupatwa na matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na maafa au kukimbia nchi.

Panapotokea maafa hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kutambua hasara iliyotokea kufuatia ufujaji au wizi husika na Serikali huchukua hatua za kuripoti hasara hiyo kwenye taarifa inayoletwa hapa Bungeni. Aidha, katika masuala ya wanaokimbia nchi, Serikali hifuata taratibu zilizopo za kuendelea kuwatafuta ikiwa ni pamoja na kutumia huduma za *Interpol*.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa zipo taarifa za uhakika kabisa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba kuna baadhi ya Maafisa Wahasibu ambao wamefanya vitendo vyta kuhujumu uchumina vyta rushwa lakini hatua za kisheria ambazo zimeshachukuliwa dhidi yao hadi sasa.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba inapotokea kwamba Afisa Mhasibu huyo ni Katibu Mkuu wa Wizara Serikali inapata kugugumizi kuchukua hatua za kisheria? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Bakari Mbconde kwa juhudhi anazofanya kuwaendeleza Watani zangu kule Rufiji. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, matukio ya ubadhirifu ama wizi unapotokea, kwanza taarifa ya tukio husika huwa inatolewa. Pili, hatua huwa zinachukuliwa kufuatilia wizi ama upotevu uliofanyika.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mhalifu ama mwizi hata kama akiwa Afisa Mhasibu ama Katibu Mkuu akafanya wizi ama akasababisha upotevu na akaachwa hivi hivi, haiwezekani. Kama Mheshimiwa ana ushahidi atulee na tutaushughulikia kama Serikali mara moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yote ya msingi yamejibowi. Sasa tunaendelea na matangazo kwa siku ya leo ambayo ni haya yafuatayo: -

Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake anaomba niwatangazie Wajumbe kwamba leo tarehe 21 Julai, kutafanyika kikao cha Kamati hiyo saa 4.30 asubuhi, chumba namba 231. Kamati ya pili ni Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mwenyekiti wake; Mheshimiwa John Malecela anaomba niwatangazie Wabunge kwamba Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama watakutana leo tarehe 21 saa 4.30 asubuhi, chumba namba 227.

Baada ya hapo kuna Mheshimiwa Katibu Msaidizi wa Wabunge Wanawake wa CCM, anaomba kuwaarifu Wabunge Wanawake kuwa safari yao ya kwenda Dara es Salaam siku ya Jumamosi, itaanzia hapa Bungeni kwa usafiri uliotolewa na Katibu wa Bunge, saa mbili asubuhi. Ni vizuri nitumie muda huu kusema kwamba, siku hiyo kwa wasi wasi kwamba tutapata mahudhurio ya kutosha, hatukupanga semina yoyote kwa Jumamosi ijayo.

Mwisho wa matangazo, Katibu tuendelee na *Order Paper*. (*Makofii*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 Wizara wa Ushirika na Masoko**

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara inayohusu Wizara ya Ushirika na Masoko na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo; Mbunge wa Bumbuli, iliyojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu tarehe 1 Juni, 2005 na kuyapitisha kwa kauli moja. Kamati ilishiriki katika mchakato wa maandalizi ya Sera na Sheria kwa mwaka 2004/2005. Kamati ilishiriki pia katika warsha ya kukamilisha rasimu ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo pamoja na kupitia Miswada ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Ugagazi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) na Muswada wa Sheria ya Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala (*The Warehouse Receipt System*). Wizara ilifaidika sana na ushauri uliotolewa na Kamati katika kuboresha na kukamilisha sera na sheria hizo. Aidha, ushauri uliotolewa umeiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumelitumikia Taifa letu kupitia Bunge hili Tukufu kwa ushirikiano na ushauri wao mzuri ndani na nje ya Bunge katika kipindi chote cha miaka 10 iliyopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wasemaji walionitangulia kutoa salamu za rambirambi kwako Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kutokana na vifo vya Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi cha mwaka 2004/2005. Marehemu Margareth Bwana; aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, marehemu Abu Towegale Kiwanga aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero, wakiwa kama Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara walitoa michango mingi ya maelekezo ya jinsi ya kuboresha utendaji wetu wa kazi.

Pia, kwa ufuutiliaji wa pekee, marehemu Margareth Bwana alisaidia sana katika jitihada za kutatua tatizo la soko la pareto katika Mikoa ya Iringa na Mbeya. Napenda kuwapa pole ndugu, wanafamilia na marafiki wa Waheshimiwa hao marehemu waliotutangulia mbele ya haki. Vile vile, natoa pole kwa familia ya marehemu Balozi Paul Bomani aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mmoja wa waasisi wa Ushirika na Chama cha *TANU* na CCM. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudhi na jitihada zake

za kuilettea nchi yetu maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii tangu awepo madarakani. Juhudi zake zimeweza nchi yetu kuwa mionganii mwa nchi chache zinazoendelea ambazo ni za mfano wa kuigwa, hususan katika nyanja za utawala bora, mazingira bora ya uwekezaji na biashara, ushirikishaji wa jamii katika kujiletea maendeleo yao, haki za binadamu na mengineyo mengi. (*Makofi*)

Kwa sababu hiyo, Benki ya dunia imeona fahari kuwa mmoja wa wadau walioshirikiana na Serikali na Watanzania katika utekelezaji uliokuwa na mafanikio makubwa ya awamu ya kwanza ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Pia, Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la *Amnesty International* (AI) katika taarifa yake limesifia Tanzania kujali haki za binadamu na utawala bora pia kuwa na mazingira yanayovutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2005. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein; Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa na Kamati Kuu ya CCM kuwa mgombea mwenza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuchaguliwa kwake kuwa mgombea wa kiti cha Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye (Mbunge) kwa hotuba yake nzuri iliyotoa maelezo mazuri kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ya awamu ya Tatu. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kwa hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mengi ya kiuchumi na kijamii, hususan Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Kilimo na Chakula. Nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia masuala ya Ushirika na Masoko wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo na Chakula walipowasilisha Hotuba zao. Michango na ushauri uliotolewa utazingatiwa katika kutekeleza mpango wa Wizara kwa mwaka wa 2005/2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliundwa Novemba 2000. Kabla ya hapo shughuli za Ushirika ziliikuwa chini ya Wizara ya Kilimo na Ushirika, wakati Serikali haikuwa na idara maalum ya kushughulikia masuala ya masoko katika muundo wake.

Masuala muhimu yaliyotekelwa katika kipindi cha mwaka 1995 hadi mwaka 2005 yanayohusu Wizara yangu yanaweza kugawanya katika makundi makuu matatu yaani masuala ya kisera, kisheria na kiutendaji. Aidha, kwa kuzingatia jukumu la msingi la Wizara, maelezo yafuatayo yanalenga katika maeneo yanayohusu maendeleo ya ushirika, uimarishaji na upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo na maendeleo ya watumishi

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 1997 ni Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 1995, ambayo ilisitisiza umuhimu wa Ushirika katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa na katika kuwashirikisha Wananchi kumiliki na kuendesha Taasisi za Kiuchumi. Aidha, katika Ilani hiyo CCM iliahidi kuwasaidia Wananchi kujenga ushirika ulio huru na imara na unaojitegemea na kupiga vita vitendo vyote vyenye nia ya kudhoofisha ushirika. (*Makofi*)

Sera ya Maendeleo ya Ushirika ilitungwa pia kwa madhumuni ya kuipa Sheria ya Ushirika ya mwaka 1991 nguvu na msimamo wa kisera wa Serikali. Hivyo, sera hii ililenga pia katika kusitisiza maamuzi ambayo yalikwishawekwa kwenye Sheria ya Ushirika ya mwaka 1991 pamoja na marekebisho yake ya 1997. Mambo yaliyositisizwa katika sera hiyo ni pamoja na umuhimu wa:-

- (i) Kuheshimu misingi ya ushirika ya Kimataifa;
- (ii) Serikali kuvilinda Vyama vya Ushirika na kuvisaidia kutatua matatizo yake sugu;
- (iii) Kukuza elimu ya ushirika kwa Wananchi na Wanachama;
- (iv) Kuanzisha Vyama vya Ushirika kwenye Sekta mbalimbali; na
- (v) Kuboresha uongozi na uwajibikaji ndani ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 ni matokeo ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Maalum ya Rais ya Kumshauri juu ya Kufufua, Kuimarisha na Kuendeleza Ushirika ya mwaka 2000. Kamati hiyo iliundwa baada ya Kongamano lililoitishwa na Mheshimiwa Rais mjini Mwanza, mwezi Machi, 2000 kujadili kuhusu matatizo ya ushirika na kupendekeza namna ya kuyatatuwa ili kuufanya tena ushirika uwe kweli chombo cha kuwasaidia wanyonge, kuimarisha mapato yao na kuondokana na umasikini.

Kamati hiyo pamoja na mambo mengine ilibaini mapungufu kwenye Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 1997 na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1991 na kupendekeza kuwa zifanyiwe marekebisho ili zikidhi mahitaji ya wakati. Maandalizi ya sera ya mwaka 2002 yalizingatia pia matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, msukumo mkubwa ukiwa ni kuimarisha ushirika ili ufanye shughuli zake kwa ufanisi zaidi na kumudu ushindani ndani ya mfumo wa soko huru. Ilani hiyo ya CCM ilitamka wazi kuwa ushirika ndicho chombo cha uhakika cha ukombozi kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimba madini wadogo wadogo.

Ilani hiyo ilibaini mambo ya kipaumbele ikiwa ni pamoja na kujenga upya Vyama vya Ushirika vya msingi imara, kuimarisha ukaguzi wa Vyama vya Ushirika; kudhibiti

wizi, ubadhirifu na rushwa; kueneza ushirika wa akiba na mikopo, kupanua wigo wa ushirika kwenye sekta mbalimbali na kuimarisha mafunzo ya ushirika.

Kwa msingi huo, Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 imetilia mkazo mambo yafuatayo: -

- (i) Ujasirishaji wa Wanachama katika kuendesha Vyama vyao vya Ushirika;
- (ii) Kuweka mazingira sahihi ya ustawi wa Vyama vya Ushirika vyenye uhai wa kiuchumi na vinavyoendeshwa kibiashara na kwa kujali gharama;
- (iii) Kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Msingi ili viweze kufanya shughuli zake kibiashara na kuweka uhusiano sahihi kati ya Vyama Vikuu vya Ushirika na Vyama vya Msingi, utakaosaidia kuimarisha Vyama vya Msingi na kuwanufaisha wanachama wa vyama hivyo;
- (iv) Kuhakikisha kuwepo kwa viongozi wenyewe ujuzi na uwezo wa kuendesha Vyama vya Ushirika kibiashara na kuwajibika kwa wanachama;
- (v) Kuhamasisha uanzishwaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo pamoja na uundwaji wa vyombo vingine vya fedha vya wanachama wenyewe ili kupanua fursa za upatikanaji wa mitaji;
- (vi) Kutambua na kuunga mkono jitihada za vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji na biashara;
- (vii) Kuhimiza wanawake kuchukua nafasi za uongozi na ajira katika Vyama vya Ushirika;
- (viii) Kuhimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika katika Sekta zote za kiuchumi na kijamii; na
- (ix) Serikali kuvisaidia Vyama vya Ushirika kutatua matatizo yake sugu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Sheria za Sekta, sheria mbalimbali zimeandaliwa na kutungwa kama ifuatavyo: -

Kwanza, marekebisho ya Sheria ya Ushirika (1991) Na. 5 ya 1997. Sheria hii ilifanyiwa mapitio na kurekebishiwa mwaka 1997 sambamba na kuandaliwa kwa sera ya maendeleo ya ushirika mwaka huo huo. Marekebisho hayo ya Sheria yalitilia mkazo mambo makuu yafuatayo:-

- (i) Kuruhusu uundwaji wa Benki za Ushirika zitakazoundwa na Vyama vya Akiba na Mikopo na Vyama vingine vya Ushirika;
- (ii) Kuruhusu Vyama vya Ushirika kuunda *Joint Venture* na makampuni;

- (iii) Kutambua kisheria, misingi ya Ushirika duniani ili vyama viweze kuendeshwa kwa kufuata misingi hiyo na kuwa Wanachama kamili wa Umoja wa Ushirika Duniani (*International Cooperative Alliance*);
- (iv) Kuweka msisitizo katika kuandikisha Vyama vya Ushirika vyenye uhai kiuchumi;
- (v) Kuweka adhabu kwa uongozi wa chama kitakachoshindwa kutoa hesabu kwa wakati; na
- (vi) Kuruhusu kuanzishwa kwa mfuko wa pamoja wa Vyama vya Ushirika kwa kugharamia maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, pili, ni Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003. Sheria hii ilitungwa baada ya kufanya mapitio na marekebisho makubwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1991 na marekebisho yake ya 1997 kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002.

Sheria mpya inawezesha kuwepo kwa mazingira muafaka yatakayoufanya Ushirika ukidhi mahitaji ya wanachama, wadau wengine na umma wa Tanzania kwa ujumla. Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 pamoja na mambo mengine imesisitiza mambo muhimu yafuatayo: -

- (i) Uhai wa kiuchumi wa Vyama vya Ushirika kuwa kigezo cha kuandikisha au kufuta Vyama vya Ushirika katika ngazi zote. Kwa sababu hiyo, sheria inahimiza vyama kuwa na mitaji endelevu ya kutosha kuendesha shughuli zake;
- (ii) Uongozi bora na uwajibikaji. Sheria ya Vyama vya Ushirika ya 2003 inacho kifungu kinachoelekeza matumizi ya maadili ya uongozi kwa menejimenti na viongozi wa Vyama vya Ushirika. Maadili hayo yanadhibiti mianya ya viongozi wabovu kujipenyeza ndani ya vyama. Aidha, huweka mkazo kwenye uteuzi unaozingatia sifa na uwezo wa viongozi watarajiwa na kutoa mamlaka kwa wanachama kuwawajibisha viongozi wabovu;
- (iii) Ili kudhibiti ubadhifuru wa mali za ushirika, Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 imeweka kifungu Na. 93 kinachotoa mamlaka kwa Mrajis kutoa *surcharge* kwa mtumishi ili kufidia hasara ambayo ameisababisha kwa Chama cha Ushirika;
- (iv) Uimarishaji wa Elimu ya Ushirika na Stadi za Biashara. Sheria inakitaka kila chama kutenga fedha kwa ajili ya utoaji elimu kwa wanachama, menejimenti na viongozi wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maendeleo ya Ushirika, Wananchi wamehamasishwa kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika kwa kusisitiza umuhimu wa Vyama vya Ushirika katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini, hususan kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimba madini na wafanyabiashara wadogo wadogo. Uhamasishaji umefanywa kwa warsha na makongamano mbalimbali.

Aidha, uhamasishaji umefanywa kwa njia ya redio, ambapo programu mbili tofauti zinatangazwa na Radio Tanzania Dar es Salaam. Programu moja inayoitwa Jifunze Ushirika inayoandaliwa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi na nyingine inayoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*TFC*) inayoitwa Ujue Ushirika wako. Kwa kutumia uhamasishaji huo, idadi ya Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 4,554 vilivyokuwepo mwaka 1995 hadi kufikia 5,730 mwezi Mei Mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 26. Wakati huo huo Wanachama wameongezeka kwa asilimia 34 kutoka 526,475 hadi 704,160 katika kipindi hicho hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ukosefu wa mitaji na uwezo mdogo wa kukopesheka ni tatizo mojawapo sugu la Vyama vya Ushirika, jitihada zimefanywa ili kuondoa tatizo hili. Jitihada hizo zinaweza kugawanywa katika sehemu kuu mbili; yaani kukuza mitaji ya ndani ya ushirika na kuvizezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo kutoka Benki za Biashara kwa kutoa dhamana. Mitaji ya ndani imekuzwa kwa kuhamasisha wanachama wengi zaidi kujiunga na vyama, kuweka akiba, kulipia hisa na michango inayotakiwa kwa wakati na kuongeza viwango vya hisa. Aidha, uhamasishaji umelenga katika kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Akiba na Mikopo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhamasishaji huo, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*) viliongezeka kutoka vyama 803 mwaka 1995 hadi vyama 921 mwaka 2000 sawa na ongezeko la asilimia 15. Idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia 103.6 na kufikia vyama 1,875 mwezi Mei 2005. Ni wazi kuwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo vimekuwa na mvuto zaidi kwa Wananchi kuliko vyama vya aina nyingine. Katika mwaka mmoja uliopita idadi ya Vyama hivyo imeongezeka kutoka Vyama 1,509 mwezi Mei 2004 hadi Vyama 1,875 mwezi Mei, 2005 sawa na ongezeko la asilimia 24.3 Aidha, idadi ya wanachama wa vyama hivi imeongezeka kutoka 219,345 mwaka 2003/2004 hadi 254,651 mwaka 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 16.3. Hali hii imefanya mitaji ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo kuimarika sana. Hisa na Akiba zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 29.7 mwezi Mei 2004 hadi Shilingi bilioni 44.6 mwezi Mei 2005.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za uchumi imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Hadi kufikia Mei 2005, kati ya vyama 5,730 kulikuwa na vyama vya mazao 2,648, vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 1,875, vya mifugo 132, vya uvuvi 99, vya nyumba 18, vya madini 16, vya viwanda 148, vya umwagiliaji 73, vya usafirishaji 17 na vya walaji 182.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa vyama kupata mikopo kutoka Benki uliimarishwa kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa dhamana ya mikopo kwa biashara ya mazao na bidhaa

za viwanda zinazouzwa nje ya nchi (*Export Credit Guarantee Scheme - ECGS*). Dhamana hii iliyoanza kutumika msimu wa 2001/2002 huwezesha Vyama vya Ushirika na wafanyabiashara binafsi kupata mikopo kutoka Benki za Biashara kwa ajili ya gharama zote za kukusanya mazao kutoka kwa wakulima hadi kuyauza nje ya nchi.

Mafanikio makubwa yamepatikana kutokana na dhamana hiyo. Kwa mfano, katika mwaka wa 2002/2003 Vyama Vikuu vya Ushirika tisa (9) ambavyo vilikuwa havina mitaji ya kukusanya mazao viliwezeshwa kukopa jumla ya Shilingi bilioni 13.19. Vyama hivyo ni Vyama Vikuu vya *ACU, KNCU, KCU, KDCU, ISAYULA, MBOCU, SHIRECU, NCU* na *BCU*.

Aidha, katika mwaka 2003/2004 jumla ya Shilingi bilioni 15.5 ziliidhinishwa. Chama Kikuu cha *KACU* kiliongezeka katika kunufaika na utaratibu huu wa *ECGS* na hivyo kufikisha idadi ya Vyama Vikuu 10 katika mwaka wa 2003/2004. Urejeshaji wa mikopo iliyotolewa ulifanyika kwa asilimia 97.3 hadi 100 kwa mwaka 2002/2003 na kati ya asilimia 84.5 hadi 100 katika mwaka wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa mitaji wa Vyama vya Ushirika na Vikundi vya Wakulima uliongezeka pia kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala kama dhamana. Kwa mfano, katika mwaka 2002/2003 Vyama vya Ushirika viliweza kukopeshwa na Benki za Biashara za *KCB, CRDB* na *EXIM* takribani Shilingi bilioni 4.7 kwa kutumia mfumo huu. Kiasi hicho kiliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 8.9 mwaka 2004/2005. Vyama vya Ushirika vilivyonufaika na mfumo huu ni Vyama Vikuu vya *RUCU* na *MICU* na vya Vyama vya Msingi vya Malindido, Pilikano, Kimuli, Luwaita na Mahenge katika Wilayani Mbanga.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi fulani udhaifu wa Vyama vya Ushirika ultokana na udhaifu wa taasisi zinazohusika na maendeleo ya ushirika, hali ambayo ilifanya Vyama vya Ushirika visipate huduma muhimu kwa viwango na wakati unaotakiwa. Ili kuondoa tatizo hilo, taasisi zimeimarishwa na ubora wa huduma umeongezeka maradufu. Taasisi hizo ambazo ni Idara ya Maendeleo ya Ushirika Wizarani, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) na Chuo cha Ushirika Moshi, zimeimarishwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ushirika hususan katika Halmashauri za Wilaya ilidhoofishwa sana mwaka 1993/1994 ambapo Maafisa Ushirika kadhaa walistaafishwa na wale waliokuwa wanasona Chuo cha Ushirika Moshi kusitishwa masomo yao. Kila Halmashauri ya Wilaya ilibakiza ukama ya Maafisa Ushirika watatu (3) tu bila kujali idadi ya Vyama vinavyotakiwa kuhudumiwa. Hatua hii ilisababisha upungufu wa Maafisa Ushirika takriban 300.

Idara hii iliimarishwa sana pale ambapo Mheshimiwa Rais alipoamua kuunda Wizara Maalum ya Ushirika na Masoko mwezi Novemba 2000. Hatua hii ilikuwa ni utekelezaji wa pendekezo mojawapo la msingi lililotolewa na Kamati Maalum ya Rais ya Kumshauri kuhusu namna ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini. Uundwaji wa Wizara hii ulilenga pia katika kuyaongezea kipaumbele masuala ya

ushirika katika mipango ya Serikali kwa kuiongezea watumishi, bajeti na vitendea kazi. Idara imeongezewa kwa kiasi kikubwa uwezo wake wa kutoa huduma katika nyanja za sheria, uhamasishaji, ukaguzi na usimamizi pamoja na huduma za ushauri wa masuala ya uwekezaji na fedha. Maafisa Ushirika walioko kwenye Sekretariati ya Mikoa na Halmashauri za Wilaya wamepatiwa mafunzo ya kujiendeleza na vitendea kazi na fedha za kufanya shughuli mbalimbali. Jumla ya Shilingi milioni 100 hupelekwa Mikoani na Wilayani kila mwaka kwa ajili hiyo. Aidha, kuanzia mwaka 2002/2003, Wilaya 75 zimepatiwa pikipiki ili kurahisisha usafiri na kuwawezesha Maafisa Ushirika kuvifiki vyama vingi zaidi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) limeimarishwa kwa kutoa fursa na kuwasomesha watumishi wake 44, kuajiri wapya ili kuziba mapengo yaliyokuwepo na kulipatia vitendea kazi. Shirika limewezeshwa kununua magari ya kutosha Makao Makuu na kwenye Kanda zote.

Aidha, Shirika limepatiwa kompyuta kwa kila ofisi ya Mikoa na limewezeshwa kifedha kwa kupewa Ruzuku Maalum na Serikali kuliwezesha kufanya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Ruzuku hii ni muhimu kwa vile wateja wake wakuu yaani Vyama vya Ushirika, kwa muda mrefu hawakuwa na uwezo wa kutosha kulipia ada za ukaguzi. Kwa mfano, hadi kufikia mwaka 2001/2002 *COASCO* ilikuwa inadai Vyama vya Ushirika malimbikizo ya Shilingi 1,652,724,000 kama ada ya ukaguzi. Katika hatua ya uimarishaji wa Shirika, Wakaguzi Wakuu wa Shirika wenye sifa za *CPA* wameongezeka kutoka wawili waliokuwepo mwaka 2000 hadi kufikia 17 mwaka 2005. Wakaguzi wa kawaida pia wameongezeka maradufu katika kipindi hicho. Matokeo ya kuimariika kwa Shirika ni kuwa idadi ya vyama vinavyokaguliwa vimeongezeka kutoka vyama 1,593 mwaka 2000 hadi kufikia vyama 3,040 mwaka 2005 kati ya vyama 4,819 na 5,730 vilivyokuwepo. Hii ni sawa na ongezeko la vyama vilivyokaguliwa kutoka asilimia 33 hadi asilimia 53.

Mheshimiwa Spika, kilichokuwa Chuo cha Ushirika Moshi kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi, mafunzo kwa walimu wake na kukiongezea uwezo wa kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi. Katika vitendea kazi muhimu ni pamoja na magari, kompyuta na vitabu vya kufundishia na vile vya rejea. Aidha, maktaba imeimarishwa na madarasa kupanuliwa ili wanafunzi wengi zaidi waweze kusoma chuoni hapo kwa wakati mmoja. Kwa mfano, idadi ya wanafunzi iliongezeka kutoka 213 mwaka 1995 hadi 721 mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 234.3.

Mheshimiwa Spika, tukio kubwa la kukiimariisa Chuo hicho ni lile la mwezi Aprili mwaka 2004 la kukipandisha hadhi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Kutokana na kuimariisa Chuo hiki, Elimu ya Ushirika inayotolewa kwa wanachama, viongozi na menejimenti ya Vyama vya Ushirika imeimarika. Elimu imetolewa kwa kutumia mbinu ya Elimu ya Ushirika Shirikishi ambayo imewajasirisha wanachama wa Vyama vya Ushirika na kuwafanya wavimiliki vyama vyao na kuwadhibiti viongozi wabovu. Kwa mfano, wanachama wa Vyama vya *SHIRECU*, *KCU*, *KDCU* na *SONAMCU*, kati ya mwaka 2000 na 2005 walijasirishwa na waliweza kuwang'oa madarakani viongozi wabovu waliokaa

madarakani muda mrefu. Elimu pia imesaidia kurejesha imani kuhusu ushirika na hivyo kuwavutia Wananchi wengi kujiunga na Vyama vya Ushirika kama ilivyoelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uongozi mbovu na usiowajibika kwa wanachama ni kikwazo cha muda mrefu cha maendeleo ya Ushirika. Kwa sababu hiyo, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuboresha uongozi na kudhibiti vitendo vya wizi na ubadhirifu wa mali ya ushirika. Hatua kubwa iliyochukuliwa na Serikali katika kuboresha uongozi na uwajibikaji ni kuweka sehemu inayohusu maadili ya viongozi na Menejimenti ya Vyama vya Ushirika kwenye Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003. Sehemu hiyo pamoja na mambo mengine inaelezea sifa zinazotakiwa kwa kiongozi au mwajiriwa wa Chama cha Ushirika. Mianya ya Rushwa na ile ya viongozi wabovu kuipenyeza kwenye Vyama vya Ushirika itaweza kuzibwa kwa kutumia vizuri kipengele hicho cha maadili ya uongozi na menejimenti ya Vyama vya Ushirika. Sehemu hii inasitiza umuhimu wa viongozi kutaja mali zao na kuwa na wadhamini ili waweze kuwajibishwa ipasavyo na kufidia hasara wanayoisababisha kwenye vyama. Utoaji taarifa za ukaguzi kwenye mikutano ya wanachama umetiliwa mkazo pia kwenye Sheria hii ikiwa ni namna ya kuimarisha uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga upya ushirika mkazo mkubwa umewekwa katika kuwa na Vyama vya Ushirika vya Msingi vilivyo imara kiuchumi, vinavyoendeshwa kibiashara na vyenye wanachama wengi wenye elimu ya ushirika ambao watawachagua viongozi wenye sifa za kuongoza ushirika wao. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha Wananchi kujiunga na ushirika na kuviongoza Vyama vyao kwa ufanisi ili kumudu ushindani wanaokabiliana nao katika mfumo wa soko huru na utandawazi. Aidha, mafunzo yametolewa ya ujasirishaji wa wanachama, uimarishaji wa nguvu za uchumi wa vyama ikiwa ni pamoja na kuongeza mitaji kwa kuongeza idadi ya wanachama watakaolipa hisa na kutumia huduma za chama chao kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka 2003/2004, Vyama 11 visivyokuwa na nguvu ya kiuchumi vilifutwa katika Daftari la Serikali vikiwemo Vyama vikuu pamoja na Vyama vya Msingi katika Mikoa na Wilaya mbalimbali. Vyama vilivyofutwa ni pamoja na *MEMACU* (Shinyanga), *KMCU* (Pwani), Chama cha Msingi cha Umeme (Mbinga), Victoria (Tarime), Tupendane na *Mara Farmers* (Mara), pamoja na *Central Marketing* (Mwanza). Vile vile, Vyama Vilele (*Apex*) vya Korosho na Kahawa vilifutwa kwenye Daftari la Serikali hadi kufikia Juni, 2004. Kwa sasa Vyama Vilele vilivyopo ni vya Tumbaku na Pamba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *SACCOS* ni asasi za kifedha kama vile Benki za Biashara zinahitaji kuwepo kwa uendeshaji na usimamizi makini ili ziweze kutoa huduma bora kwa Wananchi na kuchangia katika maendeleo yao. Kwa kuzingatia hilo pamoja na mabadiliko ya Sheria zinazohusika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa miongozo ya uendeshaji wa *SACCOS* kwa lengo la kusaidia *SACCOS* kuboresha uendeshaji na kuziwezesha kuendeshwa kwa misingi ya kibiashara ili ziweze kukidhi mahitaji ya wanachama pamoja na matakwa ya sheria. Miongozo

iliyotolewa ni pamoja na miongozo ya fedha, utendaji na viwango na mifumo ya menejimenti. Hatua hii itawezesha *SACCOS* kuajiri watendaji wenyewe sifa za kutosha, kuimarisha uongozi, uendeshaji na uwajibikaji kwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, huduma zinazotolewa na *SACCOS* kwa wanachama wake zimeendelea kukua kwa kasi mwaka hadi mwaka na hivyo kuwanufaisha wanachama wengi wakiwemo wakulima, wavuvi, wafanyabiashara wadogo wadogo, wafugaji na wafanyakazi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mikopo iliyotolewa na *SACCOS* imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 11.5 mwezi Juni, 2000 hadi Shilingi bilioni 54.1 mwezi Mei, 2005 sawa na ongezeko la asilimia 370.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 ambayo inahimiza juu ya kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika shughuli za Ushirika, Wizara ilifanya uhamashishi vikundi vya wanawake katika Mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma na Lindi. Aidha, wanawake wengi wamehamasika na kuunda *SACCOS* zao. Hadi kufikia mwezi Mei, 2005 kulikuwa na wanachama wanawake takribani 85,456 katika Vyama vya *SACCOS* kati ya wanachama 254,651 sawa na asilimia 33.6 ikilinganishwa na asilimia 16 iliyokuwepo mwaka 2000. Hayo ni mafanikio makubwa ikichukuliwa kuwa hapo awali wanawake wengi walikuwa wanajiunga zaidi kwenye vikundi vinavyoitwa upatu, Kibati na michezo kuliko kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu mafanikio katika maendeleo ya masoko ya mazao ya kilimo katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, ningependa kutaja mambo muhimu yanayoathiri biashara ya mazao ya kilimo na bidhaa zake hapa nchini na katika masoko ya nje. Mambo hayo ni kama yafuatayo:-

(i) Kilimo cha Tanzania kutegemea zaidi wakulima wadogo wadogo wanaozalisha kwa kujikimu;

(ii) Sera ya Soko huria ilianza kutumika mwanzoni mwa miaka ya 1990 kwa lengo la kupanua wigo wa biashara bila kufanya maandalizi ya kutosha kwa Vyama vya Ushirika, Vikundi vya Wakulima na Taasisi za kusimamia taratibu za mfumo huo mpya. Matokeo yake ni kuwa biashara ilifanya bila kufuata vituo maalum, bila kuzingatia vipimo na bila kujali ubora na madaraja ya mazao;

(iii) Mwenendo wa bei za mazao hasa yale yaliyouzwa kama malighafi kwa kipindi kirefu zimekuwa ama zikipungua mwaka hadi mwaka au zikibadilika mara kwa mara hivyo kufanya upangaji mipango madhubuti ya masoko kuwa mgumu;

(iv) Mazao mengi ya Kilimo yamekuwa yakiuzwa Nchi za Nje kama Malighafi bila kuongezwa thamani. Kwa sababu hiyo wafanyabiashara wa Mazao ya Kilimo hawajaweza kunufaika ipasavyo na fursa za upendeleo zilizotolewa na Masoko ya Ulaya, Marekani na mengineyo. Aidha, masharti magumu ya ubora wa viwango, na vikwazo mbalimbali visivyo vya kodi (*Non-Tariff Barriers*) ni sababu nydingine zilizosababisha kushindwa kunufaika na Masoko hayo na

(v) Utoaji wa ruzuku zinazosaidia uzalishaji au uuzaji wa mazao na bidhaa za kilimo katika Nchi ambazo ni masoko ya mazao yetu asilia kama pamba na kahawa umefanya mazao yetu yashindwe kushindana kwa faida kwenye masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tatu katika kuboresha hali ya Masoko na kuhakikisha kuwa masoko ya uhakika yanapatikana ni pamoja na hatua zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa biashara ya mazao, Serikali imerekebisha sheria zilizounda Bodi za Mazao kwa kuweka bayana majukumu mbalimbali ya wadau katika Sheria hizo. Marekebishi hayo yalifanyika mwaka 2001 na 2002. Katika marekebishi ya Sheria hizo, Bodi za Mazao zimepewa jukumu la kusimamia kanuni na taratibu zinazohusu uzalishaji, usindikaji na biashara ya mazao ambapo Sekta Binafsi pamoja na Vyama vya Ushirika, imepewa jukumu la kibiashara.

Sambamba na mabadiliko hayo matumizi ya mnada wa elekroniki kwa zao la Kahawa ulianzishwa na utaratibu wa kuzuia mfanyakibashara mmoja kuwa na leseni zaidi ya moja mfululizo kwenye mchakato wa biashara nje ya nchi ulianzishwa. Hali hii iliongeza ushindani pamoja na kudhibiti ukiritimba na hivyo kuchochaea kuongezeka kwa ubora na bei ya bidhaa kutoka Tanzania zilizouzwa nje. Serikali itaendelea kufanya rejea ya kazi na muundo wa Bodi za mazao ili kuboresha tija na ufanisi wake. Hii ni pamoja na kutathmini umuhimu na uwezekano wa kuanzisha Bodi ya mazao mchanganyiko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali ya usimamizi wa masoko itaimarika zaidi baada ya kuanza kutumia Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ambayo imekwishaandaliwa. Maelezo zaidi ya Sera hiyo yapo katika sehemu inayofuata ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikikusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko na bidhaa za kilimo na mifugo kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi ya kibiashara. Taarifa hizo zinasambazwa kupitia redio, magazeti, majorida na mawasiliano ya moja kwa moja. Aidha, Wizara imekuwa ikitoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wakusanyaji wa taarifa za masoko (*Market Monitors*) na kuwapatia vitendea kazi. Kwa mfano, kati ya mwaka 2003 na 2005, Wizara imetua pikipiki 20 na kompyuta 16 kwa wakusanyaji wa taarifa walioko kwenye miji mikuu ya mikoa Tanzania Bara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao ndani na nje ya nchi. Tafiti hizo ni pamoja na Mapitio ya Mahitaji ya Taarifa za Masoko ya Mazao yaliyofanyika mwaka 2004 na Tathmini ya Gharama za Ununuzi na Uuzaji wa Mazao na namna ya kuzipunguza inayoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imehamasisha Sekta Binafsi kutumia fursa mbalimbali za Masoko hususan za Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na Soko la

Marekani (*AGOA*). Ili kunufaika ipasavyo na fursa hizi, jitihada kubwa zimefanywa katika kuwaelimisha wakulima kuzalisha mazao yao kibiashara kwa kuzingatia mahitaji na masharti ya Soko, hususan katika ubora, madaraja na ufungaji (*packaging*).

Mheshimiwa Spika, Serikali imewawezesha pia wafanyabiashara kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ya Kibiashara na kushiriki kwenye maonyesho mbalimbali ya Kimataifa. Kwa mfano mwaka 2003, Serikali iliwezesha Kampuni kadhaa za Mboga mboga, Maua, Matunda na Viungo kushiriki kwenye maonyesho ya Kimataifa yaliyofanyika Rostock, Ujerumani. Ushindi wa Medali kadhaa kwenye maonyesho hayo ulidhihirisha kuwa bidhaa toka Tanzania zinao ubora unaokubalika kwenye masoko ya Ulaya. Wafanyabiashara waliweza pia kujifunza na kuelewa umuhimu wa kuzingatia viwango vya kimataifa katika ubora na ufungaji wa bidhaa. Aidha, wakulima wadogo wadogo wa mboga mboga walijifunza kuwa wakitaka kunufaika na masoko hayo inawapasa kujiunga na wakulima wakubwa katika kilimo cha mikataba (*Contract Farming*). Mikataba hiyo tayari imeanza katika Mikoa ya Arusha na Tanga. Ushiriki kama huo ulifanyika tena Moscow, Urusi mwaka 2004 ambapo, Wizara ya Ushirika na Masoko iliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye maonesho ya *World Food Expo-2004*. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuwapata wanunuvi wa mafuta ya mawese kutoka Urusi ambaa walitembelea Tanzania kufanya taratibu za biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mwaka 2004 Serikali iliwezesha Wafanyabiashara kadhaa wa mazao ya kilimo na mifugo kushiriki kwenye kongamano la kuhamasisha na kuvutia wawekezaji kuja Tanzania lililofanyika Midrand, Afrika ya Kusini. Kutokana na kongamano hilo wawekezaji kutoka Visiwa vya Re-Union wameonyesha nia ya kuwekeza kwenye uzalishaji wa Kuku na Chakula cha Mifugo Mkoani Kilimanjaro. Kwa kupitia Mradi wa Kuendeleza Masoko Vijijini (*Rural Markets Development Project*) unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa, miundombinu ya masoko imeimarishwa. Mradi huu umetekelizwa katika Wilaya za Kongwa, Morogoro Vijijini na Mvomero. Shughuli kubwa iliyofanywa ni pamoja na ujenzi wa masoko imara, barabara na daraja zinazounganisha wakulima na masoko.

Moja ya mafanikio makubwa ya mradi huu ni Ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mahindi katika Mji mdogo wa Kibaigwa, ulioko Wilaya ya Kongwa. Masoko mengine yaliyojengwa kwa mpango huu ni pamoja na masoko ya matunda katika vijiji vya Tawa na Kinole, Wilaya ya Morogoro na Soko la Matunda na Mboga mboga lililojengwa Nyandira, Wilaya ya Mvomero. Ujenzi zaidi wa miundombinu ya masoko na Barabara unafanywa kupitia Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme - AMSDP*). Programu hii ilioanza mwaka 2002 ni ya miaka 7 na inafadhiliwa na IFAD, ADB na Serikali ya Ireland. Programu hii inatekelezwa katika Wilaya 36 za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Malengo ya programu hii ni kutengeneza Barabara za vijijini zenye jumla ya urefu wa kilometra 1,136, madaraja 115, makalvati 575 na kujenga masoko 20.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo kasumba kwa Watanzania ya kupenda bidhaa kutoka nchi za nje hata kama zina ubora wa chini kuliko zinazozalishwa hapa nchini.

Hali hii inaongeza ugumu wa kupata masoko ya uhakika kwa bidhaa zetu. Ili kuondoa tatozo hili ni muhimu Watanzania wakahamasishwa kupenda na kuthamini bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Umuhimu wa kuimarisha soko la ndani umesitisitiza mara kwa mara na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mfano katika hotuba yake aliyoitoa Mjini Songea wakati wa ufunguzi wa soko la kisasa Mjini Songea tarehe 30 Aprili, 2005, alisema: "Watanzania wajenge utamaduni wa kutumia bidhaa wanazozalisha. Licha ya kuwa Watanzania watajijenega uwezo wa ushindani wa kibashara ndani na nje ya nchi, lakini watakuwa wanawaongeza nguvu na ari ya uzalishaji wa bidhaa hizo. Rai yangu kwenu ni moja tu nayo ni kuwaomba muwe na mwelekeo wa kula kile tunachozalisha sisi wenyewe na tusikimbilie vile vinavyotoka nje....."

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza uhamasishaji wa Watanzania kupenda na kutumia kwa wingi bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Uhamasishaji huo pamoja na mambo mengine umehusu uendeshaji wa Kongamano la Kitaifa kuhusu suala hili lililofanyika mwezi Oktoba mwaka 2004. Katika mbinu zinazotumika katika uhamasishaji ni kuzingatia ubora katika uzalishaji ili walaji wavutiwe na ubora wa bidhaa badala ya uzalendo tu. Maduka makubwa ya vyakula (*Supermarkets*) yamehamasishwa na yamekubali kununua bidhaa kama matunda, mboga mboga, bidhaa za mifugo na nafaka zinazozalishwa hapa nchini. Fursa nyingine kubwa inayotumika ni kuwashirikisha wakulima, Vyama vya Ushirika na Vikundi vya wazalishaji kwenye maonyesho ya sikuu ya wakulima (Nane nane). Sherehe hizi zinazofanyika kila mwaka Kitaifa, Kikanda na Kimkao hutoa fursa nzuri ya washiriki wa maonyesho kuona na kuvutiwa na bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Aidha, kwa njia ya mashindano, wazalishaji hujifunza mbinu za kuboresha bidhaa zao ili ziweze kukubalika kirahisi na wateja.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuimarisha masoko zilizoelezwa hapo juu zimeleta mafanikio katika uimarishaji wa mauzo ya mazao asilia. Kwa ujumla kumekuwa na ongezeko kwenye mazao yote makuu katika kipindi hicho cha miaka kumi isipokuwa kwa zao la korosho, kahawa na mkonge. Kwa mfano, mauzo ya pamba yalionegezeka kutoka tani 221,148 mwaka 1995/1996 hadi kufikia tani 261,000 katika mwaka 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Hali kadhalika mauzo ya tumbaku yalionegezeka kwa asilimia 20 kutoka tani 28,598 hadi tani 35,777, chai iliongezeka kwa asilimia 66 kutoka tani 93,771 hadi tani 155,786 katika kipindi hicho hicho.

Mafanikio yameonekana pia katika bidhaa zitokanazo na mifugo ambapo mauzo yameongezeka pia. Kwa mfano, mauzo ya ngozi nje ya nchi yalionegezeka kutoka vipande milioni 2.1 mwaka 2000/2001 hadi milioni 3.2 mwaka 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 52.4. Hata hivyo thamani ya mauzo hayo ilipungua kwa asilimia 30 hadi kufikia Shilingi bilioni 4.0 mwaka 2004/2005 kutoka Shilingi bilioni 5.7 mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, dhana ya Utawala Bora inayohusu uwazi, uwajibikaji wa watumishi kwa umma, ushirikishwaji, kujali matakwa ya nchi, kuzingatia utawala wa sheria na haki za binadamu, Wizara iliazimia kuleta mabadiliko yanayolenga utoaji wa

huduma kwa umma kwa ufanisi zaidi. Wizara ililenga katika kuhakikisha kwamba watumishi wote wanawajibika ipasavyo na kufuata kanuni, sheria na taratibu zilizowekwa katika utumishi wa umma. Aidha, Wizara ililenga katika kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanakuwa na maadili mema na kujua wajibu wao. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: -

- (i) Watumishi wote wa Wizara kupatiwa mafunzo kuhusu Maadili ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na vita dhidi ya rushwa;
- (ii) Kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali kwa kuweka kumbukumbu za masijala ya wazi na siri katika kompyuta na
- (iii) Kuunda Kamati ya Ajira ya Wizara ambayo inashughulikia ajira zote za watumishi kwa uwazi zaidi pamoja na nidhamu na upandishwaji vyeo.

Pamoja na mafanikio haya, Wizara imeendelea kushughulikia maendeleo ya watumishi, hususan upandishwaji vyeo na mafunzo. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara iliwardhamini Maafisa Ushirika wapatao 338 katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu vikiwemo Chuo cha Ushirika Moshi, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kuwaongezea sifa na ujuzi. Wengi wa Maafisa Ushirika waliodhaminiwa ni wale walioko katika Halmashauri za Wilaya. Vile vile, elimu na uhamasishaji wa kupiga vita rushwa na kuhusu janga la Ukimwi imeendelea kutolewa katika semina za watumishi wote na Baraza la Wafanyakazi.

Mnamo mwezi Novemba, 2002 Wizara ya Ushirika na Masoko ilikuwa mionganoni mwa Wizara kumi na tatu (13) zilizozindua rasmi Mkataba wa Huduma kwa Wateja (*Client Service Charter*). Lengo kuu la mkataba huu ni kukuza uelewa wa upatikanaji na ubora wa huduma zitolewazo na Wizara. Hili limesaidia Wananchi kuelewa shughuli za Wizara, namna ya kuwasiliana, viwango vya huduma zinazotakiwa na jinsi ya kutatua matatizo yanapojitokeza. Aidha, Mkataba huu umesaidia umma katika kuzijua haki zao na pia unatoa uwazi zaidi katika mawasiliano na kutoa malalamiko yao pale ambapo wanaona hawardhishwi na huduma za Wizara. Kwa kifupi Mkataba huu ni chombo cha kuleta mabadiliko Serikalini yanayolenga kuboresha utendaji wa kazi na uwajibikaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirika na Masoko ilipoundwa ilikuwa na jumla ya watumishi 82 tu. Idadi hii ya watumishi haikuweza kutosheleza mahitaji ya Wizara. Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wake kwa kushughulikia ajira zote mpya zilizoidhinishwa mwaka hadi mwaka. Kufikia mwaka 2004/2005 Wizara ina jumla ya watumishi 152 katika fani mbalimbali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliwezesha Maafisa Ushirika 88 kuajiriwa ili kupunguza tatizo la upungufu wa Maafisa Ushirika Mikooni na Wilayani. Lengo ni kuajiri maafisa Ushirika 300 ili kukidhi mahitaji. Nachukua nafasi hii kutoa rai kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuajiri Maafisa Ushirika wa kutosha ili tuweze kuimarisha na kuujenga ushirika mpya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara yangu ilipanga kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyolenga kuimarisha na kuendeleza huduma muhimu za ushirika na maendeleo ya masoko. Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa kiasi kikubwa. Pamoja na mafanikio katika shughuli za kawaida za kila siku za kiofisi, kiutawala na zinazohusu maslahi ya watumishi, mafanikio makubwa ni sera, sheria na mipango.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa, wakulima, wafanyabiashara na wasindikaji wanakabiliwa na matatizo mbalimbali katika shughuli za masoko ya mazao ya kilimo. Hata hivyo hakuna mwongozo wa kisera unaoelekeza namna ya kuyatatu. Kwa vile umuhimu wa masoko ya uhakika katika kuondoa umaskini unasisitizwa kwenye mikakati ya Kitaifa kama Mkakati wa Kupunguza Umaskini (*Poverty Reduction Strategy*) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Wizara iliona ni vema sera ya masoko ya mazao ya kilimo iandaliwe. Kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, Wizara imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Sera hiyo (*Agricultural Marketing Policy*) mwezi Mei, 2005. Rasimu hiyo ipo tayari kwa kujadiliwa na kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ina mwelekeo (*vision*) wa kuwepo na mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo ulio madhubuti, thabiti na wa haki. Lengo lake kuu ni kuboresha utendaji wa mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo na kukuza ushiriki wa wadau katika kutumia vizuri fursa za masoko ili kuwa na masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo na bidhaa zitokanazo na mazao hayo. Mambo muhimu yanayotiliwa mkazo katika sera hiyo ni pamoja na yafuatayo: -

- (i) Kuimarisha Taasisi, Sheria na Kanuni zinazosimamia masoko ya mazao ya kilimo;
- (ii) Kuongeza uwingi na ubora wa mazao kufikia viwango vinavyohitajika na masoko makuu;
- (iii) Kukuza usindikaji wa msingi (*Primary processing*) kwa lengo la kuyaongezea thamani mazao na bidhaa kabla ya kuuzwa;
- (iv) Kukuza soko la ndani na la nje kwa njia mbalimbali za uhamasishaji na uwezeshaji;
- (v) Kuchochea na kusaidia uwekezaji katika miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na magilio na masoko (*Market centres*) ya hadhi ya Kimataifa, barabara na madaraja yanayounganisha wazalishaji na masoko;
- (vi) Kuimarisha utafiti, pamoja na ukusanyaji na usambazaji wa taarifa muhimu za masoko ya mazao kwa faida ya wadau wote;

- (vii) Kuwezesha Sekta binafsi kupata mitaji, kutumia fursa za kibiashara za kikanda na kutumia mbinu mbalimbali zilizopo za masoko kwa gharama nafuu na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ukaruzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) lilianzishwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 1982. Sheria hiyo iliainisha majukumu ya *COASCO* ambayo ni kusimamia na kukagua hesabu za Vyama vya Ushirika. Kutokana na marekebisho katika sera za uchumi ambayo yamesababisha kuwa na sera na sheria mpya ya maendeleo ya ushirika, majukumu hayo yamebainika kutokidhi mahitaji ya ushirika chini ya mfumo wa uchumi uliopo. Kutokana na mabadiliko hayo Sheria iliyoanzisha Shirika la Ukaruzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) ilipaswa nayo ifanyiwe marekebisho ili kuliwezesha shirika kushiriki ipasavyo katika kutekeleza Sera na Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika. Kwa hivyo, sheria ilifanyiwa marekebisho na kuitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2005.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya ya Sheria yameliongezea Shirika la *COASCO* majukumu yafuatayo: -

- (i) Kusimamia kazi za ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, ambavyo kwa Sheria mpya ya Ushirika ya mwaka 2003, vinaweza kukaguliwa na makampuni binafsi ya ukaguzi;
- (ii) Kufanya utafiti katika masuala yahusuyo Vyama vya Ushirika na kutoa ushauri kwa Serikali;
- (iii) Kutoa huduma za ukaguzi nje ya Vyama vya Ushirika, ikiwa ni pamoja na vikundi vyenye mwelekeo wa ushirika (*Pre-Cooperative Groups*) ambavyo vinatambuliwa na Sheria mpya ya Ushirika ya mwaka 2003 na
- (iv) Kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinatekeleza Kanuni na Maadili ya Viongozi wa Vyama vya Ushirika, kama zilivyofafanuliwa na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni utaratibu ambao unawawezesha wakulima wadogo, kuitia Vyama vya Ushirika au Vikundi vyao, kutumia mazao yao kwenye maghala kama dhamana ya kupata mikopo. Mfumo huu hutumia stakabadhi za maghala zinazotolewa na mwendesha ghalazinakuwa na hadhi na thamani kama zilizonazo Nyaraka za Fedha (*Negotiable Instruments*).

Kwa sababu hiyo mfumo huu hutoa fursa kwa wakulima na wafanyabiashara wasiokuwa na dhamana za mali zisizohamishika, kutumia mazao yao kama dhamana. Faida nyingine za mfumo huu ni: -

- (i) Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa na hivyo kuongeza uhakika wa chakula na kipato kutokana na hifadhi bora. Hivi sasa kati ya asilimia 30 hadi 40 za mazao ya chakula inapotea baada ya kuvuna kutokana na hifadhi hafifu;

- (ii) Kupunguza athari za miporomoko ya bei. Utekelezaji wa mfumo utawezesha wakulima kuweka mbinu endelevu za kuhimili mporomoko wa bei kama Bima na kinga ya Bei (*Price insurance and hedging*);
- (iii) Kuwawezesha wakulima kufanya biashara ya mazao yao bila kulazimika kuyapeleka sokoni na hivyo kuongeza na kuimarisha ushindani wa mazao hayo katika soko la ndani, Kikanda na Kimataifa;
- (iv) Kuwawezesha wakulima kuhifadhi mazao yao kwa usalama na muda mrefu na hivyo kuyauza wakati ambao bei ni nzuri au wanapohitaji kuyauza. Mkulima anayehifadhi mazao yake na kuyauza bei zinapokuwa nzuri, hupata faida kubwa kuliko wanaouza mara tu baada ya kuvuna bila kuzingatia mwenendo wa bei na
- (v) Kusaidia kuongeza ubora na matumizi ya viwango kwa mazao yanayouzwa katika masoko ya ndani, Kikanda na Kimataifa kwa vile yanahifadhiwa katika maghala yaliyoidhinishwa na yanayosimamiwa na sheria.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2002/2003 mfumo huu ultumika kwa majoribio katika maeneo yanayolima Kahawa na Pamba kuitia Mradi wa Kuendeleza Masoko ya Kahawa na Pamba chini ya ufadhilli wa Mfuko wa Kuendeleza Mazao.

Wakati wa majoribio hayo ilibainika wazi kuwa ili kuwepo na ufanisi zaidi wa mfumo wenye inahitajika kuwepo sheria ya kusimamia, kwa kuainisha majukumu, wajibu na haki za wadau wote wakuu. Kwa sababu hiyo Serikali kwa kushirikiana na wadau ilitunga Sheria ya Stakabadhi za Mazao Na. 10 ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2005.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala itasaidia kuongeza imani kwa taasisi za fedha kutoa mikopo kwa kutumia stakabadhi za mazao kwenye maghala kama dhamana. Kwa hiyo, Benki nyingi zitashiriki kutoa mikopo kwa wakulima. Hali hii itaongeza ushindani wa kutoa huduma bora zenye ufanisi na zenye riba nafuu. Aidha, Benki za *CRDB, KCB* na Exim zinazotoa mikopo hiyo kwa sasa zinaonyesha kuwa mfumo huu unafaa kuliko kutumia mali zisizohamishika pekee na hivyo zimeanza kutekeleza mfumo wa Stakabadhi za Maghala bila kuhitaji udhamini kutoka kwa Wasimamizi wa Dhamana (*Collateral Managers*), bali wanatumia udhamini unaotolewa na Mwendesha Maghala. Mbinu hii imepunguza gharama za kusimamia mikopo na woga wa hassara kwa mikopo inayotolewa na benki hizo. Hali hii imefanya riba zinazotozwa chini ya mfumo huu kupungua hadi asilimia 12 ikilinganishwa na zile zinazotozwa nje ya mfumo ambazo ni asilimia 19 au zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kulega lega kwa Ushirika kwa muda mrefu na kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa wanachama wake na pia kutokana na mabadiliko makubwa katika mbinu za kufanya biashara duniani, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Ushirika nchini imeandaa Programu Kabambe ya

Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini. Chimbuko la Mpango huu Kabambe wa Mageuzi ya Ushirika ni Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002. Sera hii inazingatia kero na matatizo ya kihistoria ya Vyama vya Ushirika na inakusudia kujenga mfumo wa ushirika ambao ni endelevu na unaokidhi mahitaji ya wanachama ya kiuchumi na kijamii. Aidha, programu hii imelenga kuwawezesha wanachama kuvidhibiti na kuviendeleza vyama vyao kadri ya mahitaji yao, ikiwa ni pamoja na kupambana na kuondoa matatizo sugu yanayovikabili Vyama vya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Spika, Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini iliyozinduliwa rasmi mwezi Desemba 2004 ni mkakati rasmi wa utekelezaji wa Sera mpya ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002. Kwa sababu hiyo malengo yake makuu ni kutekeleza mambo yaliyotiliwa mkazo kwenye sera hiyo kama yalivyotajwa hapo juu. Malengo maalum ya programu hii ni:-

- (i) Kuhimiza na kuwzesha kuibua mfumo wa Ushirika ambao msingi wake ni Vyama vya Ushirika vya Msingi na wanachama;
- (ii) Kuhamasisha kuwepo kwa Viongozi wa Ushirika wanaowajibika kwa wanachama na ambao ni wabunifu kibiashara na watendaji wenye elimu na uzoefu wa biashara za kisasa;
- (iii) Kujasirisha wanachama kwa kuwawezesha kupata elimu na stadi zinazohitajika ili waendeleze vyama vyao;
- (iv) Kuhimiza na kuhamasisha uanzishwaji/uendelezaji wa Vyama vya Ushirika vyenye nguvu za kiuchumi na endelevu;
- (v) Kuhimiza na kuwzesha mabadiliko makubwa katika mfumo wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na Benki za Ushirika ili vyombo hivyo viwe chanzo cha mitaji endelevu ndani ya Ushirika;
- (vi) Kuhamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa aina mbalimbali kulingana na mahitaji ya wanachama, jamii na Taifa na
- (vii) Kuimarisha uwezo wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika, Taasisi na Asasi mbalimbali zinazohusika na maendeleo ya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini unalenga kuibua Ushirika wenye sura mpya wa karne ya 21. Ushirika ambao utaendeshwa kibiashara kulingana na mahitaji ya wanachama wake kwa kuzingatia mazingira ya soko na utandawazi. Programu hii imeweka msukumo wa kipekee katika kuwajasirisha wanachama ili waweze kuwa wabunifu na wenye kuthubutu kutumia ipasavyo fursa mbalimbali zinazojitokeza katika soko. Ushirika huu ambao hauna budi kuongozwa na viongozi wenye sifa na upeo wa kutosha katika masuala ya biashara, uliasisiwa kwa mara ya kwanza mwaka 2000 katika Kongamano la Kitaifa la Wanaushirika ambalo Mwenyekiti wake alikuwa Rais Benjamin

William Mkapa. Wizara yangu imeyafanya kazi mawazo ya Kongamano hilo na kuandaa Programu ya Ushirika ili kuwawezesha wanachama kuleta mabadiliko yanayohitajika ndani ya vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu hii umeanza katika maeneo kadhaa. Kwa mfano, kuhusu uongozi bora, zoezi la kufanya uchaguzi kwenye Vyama vya Ushirika kwa misingi ya Sheria mpya ya Vyama vya ushirika Na. 20 ya mwaka 2003 lilianza mwezi Mei 2005, katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga na Mara. Zoezi hilo litaendelea katika mikoa mingine na linatarajiwa kukamilika mwezi Machi mwaka 2006. Aidha, mafunzo kwa waraghbishi 294 watakaojasirisha wanachama wa Vyama vya Ushirika kote nchini yamekwishatolewa. Waraghbishi hao wataanza kazi yao katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu mchakato wa mpango wa wanaushirika wa kuanzisha Benki ya Ushirika ya Kitaifa. Kazi ya upembuzi yakinifu wa kuanzisha Benki ya Ushirika ya Kitaifa iliyokuwa inafanywa na Mshauri Mwelekezi ilikamilika na taarifa kutolewa mwezi Juni, 2005. Katika mchakato huo wadau walishirikishwa kwenye warsha iliyofanywa Oktoba, 2004 na walikubaliana juu ya masuala muhimu yakiwemo Muundo wa Benki, ukusanyaji wa fedha za mtaji na utaratibu wa kuanzisha benki hii. Mpango huu unafuatia juhud za Wanachama zilizofanywa katika Mikoa ya Kilimanjaro na Kagera ambapo Benki za *Kilimanjaro Cooperative Bank (KCB)* na Kagera *Farmers Cooperative Bank (KFCB)* zimeanzishwa. Benki hiyo itaongeza upatikanaji wa mitaji yenye masharti nafuu kwa Vyama vya Ushirika kuliko ilivyo hivi sasa. Taratibu za kuanzisha Benki hiyo zitakamilika katika mwaka wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji Wananchi kuunda Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali umeendelea vizuri. Jumla ya Vyama 268 vimeanzishwa katika mwaka 2004/2005, ambapo 210 (sawa na asilimia 78) ni Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*). Vyama vingine ni pamoja na Vyama vya Umwagiliaji 44 na Mifugo 14.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha maandalizi ya Kanuni za Vyama vya Ushirika mwezi Julai 2004. Hatua hii iliiwezesha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 kuanza kutumika tarehe 1 Agosti, 2004. Ili Sheria iweze kuwafikia Wadau muhimu na waweze kuitekeleza, Wizara ilichapisha na kusambaza kwa wadau nakala 5,000 za Sheria na nakala 2,000 za Kanuni za Vyama vya Ushirika. Mionganoni mwa Wadau waliopewa nakala za Sheria na Kanuni ni Washauri wa Ushirika wa Mikoa, Maafisa Ushirika wa Wilaya, Viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika na wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*).

Chini ya Programu ya Kitaifa ya ujasirishaji wa Wanachama (*Member Empowerment in Management of Cooperatives (MEMCOOP)*) Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi ilitoa mafunzo kwa waraghbishi 22 kutoka Wilaya mbalimbali. Waraghbishi hao watasadidu kutoa elimu ya Ushirika Shirikishi kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Wizara imeendelea kuwapatia vitendea kazi Maafisa Ushirika katika Halmashauri za Wilaya ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Wizara imepeleka Mikoani na Wilayani Shilingi milioni 111 kwa ajili ya kazi za uhamasishaji, uimarishaji na uendelezaji Vyama vya Ushirika. Aidha, fedha hizo zinatumika katika usimamizi wa uchaguzi wa viongozi wa vyama, ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Pia, Wizara imenunua hivi karibuni pikipiki 19 ambazo zimepangwa kupelekwa katika Wilaya za Monduli, Biharamulo, Kibondo, Rombo, Rungwe, Ulanga, Kilosa, Geita, Rufiji, Bukombe, Iramba, Nkasi, Tunduru, Nzega na Handeni kusaidia kuimarisha shughuli za Ushirika. Wizara imepeleka Wilayani jumla ya Pikipiki 51 katika kipindi cha miaka minne (4) iliyopita. Aidha, pikipiki 2 zilipelekwa Mikoani na 3 zimebakia Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika zimeendelea kuimarishwa kwa kuliwezesha Shirika la *COASCO* kufanya kazi yake. *COASCO* ilipewa Shilingi 526,852,300 kwa ajili ya matumizi mengine. Kufuatia uwezeshaji huo shirika lilifanikiwa kukagua hesabu za Vyama 3,040 kati ya Vyama 5,730 vilivyokuwepo mwaka 2004/2005. Hii ni sawa na asilimia 53.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufuatilia na kuhakiki matumizi ya mikopo iliyotolewa kwa Vyama vya Ushirika. Katika mwaka uliopita wa 2004/2005, kwa mfano, Wizara ilihakiki matumizi ya fedha za mikopo katika Vyama vya *KNCU*, *ACU*, *KDCU*, *BCU*, *NCU*, *KACU*, *SHIRECU*, *MICU*, *RUCU*, *MBOCU* na *ISAYULA*. Vyama vinavyoshughulikia kahawa viliweza kurejesha mikopo ya benki bila matatizo na kwa wakati. Vyama vinavyoshughulikia pamba vilikumbwa na tatizo la mwenendo mbaya wa bei katika soko la dunia. Hali hii inatokana na kushuka kwa bei ya pamba ambapo gharama za kukusanya pamba na malipo ya mwanzo kwa mkulima ilikuwa kwenye makisio ya kuuza pamba nyuzi kwa dola za Marekani 60 kwa ratili, lakini kwenye soko iliuzwa kwa dola za Marekani 0.37 kwa ratili. Tofauti hii ya bei imeviacha vyama katika hali mbaya ambapo vingine vimeuza mali za kudumu (*SHIRECU*) kulipa mikopo na sehemu nyingine (*BCU* na *NCU*) imebidi Serikali iingilie katika kuwanusuru wakulima. Aidha, Wizara imehimiza kuanza kutumika kwa kanuni za Maadili ya Uongozi ndani ya Vyama vya Ushirika ambazo zimewesha upatikanaji wa viongozi kwa kufuatia sifa zao katika elimu, ujuzi, mwelekeo na dira, uadilifu, uwazi, uwajibikaji kwa wanachama na bila kuwa na ubinafsi. Vile vile, umewekwa muda maalum wa uongozi ndani ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, fanikio mojawapo kubwa katika utatuvi wa migogoro ya Vyama vya Ushirika ni muufaka uliofikiwa kuhusu mgawanyo wa mali zilizokuwa chini ya Washirika. Mgogoro huo ambao umekuwepo kutoka mwaka 1996 ulikuwa kati ya Vyama Vikuu vya Ushirika vya Tanzania Bara na Vyama vya Ushirika vitano vya Zanzibar kupitia *Cooperative Union of Zanzibar (CUZA)*. Kwa ushirikiano kati ya Wizara yangu na Wizara ya Kilimo, Mazingira na Ushirika ya Zanzibar, Mgogoro huo sasa umehimitishwa kwa makubaliano yaliyofanyika Bagamoyo tarehe 8 Mei, 2005. Migogoro mingine iliyotatuliwa ni pamoja na: -

- Mgogoro wa kiwanja kilichopo Ilala kilichokuwa kinagombaniwa baina ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*TFC*) na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (*SCCULT*);
- Mgogoro uongozi wa Chama cha Ushirika wa Mazao Madibira cha Mbeya na *SACCOS* ya Madibira uliohusu chama cha mazao kuchelewa kulipa mkopo takriban Shilingi milioni 120 walizokopeshwa na *SACCOS*.
- Mgogoro wa Chama cha Ushirika wa Madereva wa Taxi Ubungo, kuhusu viongozi watatu wa zamani kung'ang'ania madaraka na kutaka kuhamisha ofisi ya chama nje ya eneo la chama, Kituo cha Mabasi Ubungo bila ridhaa ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko kwa lengo la kuwasaidia wazalishaji, wafanyabiashara na walaji kufanya maamuzi muafaka. Taarifa hizo zinazohusu mazao makuu ya chakula na mifugo, zimekuwa zikisambazwa kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam, Magazeti, Majarida na mawasiliano ya moja kwa moja kupitia barua. Ili kuimarisha ukusanyaji wa taarifa na takwimu maafisa husika walipatiwa mafunzo na vitendea kazi.

Aidha, kwa kupitia mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme (AMSDP)*) maafisa wawili kutoka Wizarani walidhaminiwa mafunzo ya muda mfupi nchini Afrika Kusini kujifunza namna ya kuimarisha ukusanyaji wa taarifa. Aidha, Maafisa Watatu walipatiwa fursa ya mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa mifumo ya taarifa za masoko ya mazao katika nchi za Afrika ya Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakamilisha maandalizi ya tovuti ambayo itawezesha wazalishaji, wafanyabiashara na walaji wa mazao na bidhaa za kilimo kupata taarifa za masoko wanazohitaji kwa urahisi na kwa wakati muafaka kwa kutumia mtandao wa kompyuta. Aidha, tovuti hiyo itaongeza na kurahisisha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali.

Vilevile, Wizara inakamilisha taratibu za makubaliano kati yake na Kampuni ya Simu za Mikononi ya *Vodacom Tanzania Limited* ili taarifa za masoko ziweze kusambazwa kwa njia ya ujumbe wa maneno. Pamoja na juhudhi hizo, Wizara pia inafanya majadiliano na vituo vya Radio Binafsi, hususan *Radio One* na *Radio Free Afrika* ili navyo vitumike kusambaza taarifa za masoko.

Ili kuimarisha uchambuzi na hifadhi ya taarifa za masoko, Wizara imeanza kutumia programu mpya ya kompyuta iitwayo *AgriMarket*. Kwa kuzingatia umuhimu wa programu hii, Wizara kwa kuanzia imetoa mafunzo kwa maofisa 14 ambao hukusanya taarifa za masoko katika miji mikuu ya mikoa ya Tanzania Bara kati ya maofisa 20 waliopatiwa kompyuta. Mafunzo ya kukusanya, kuchambua na kusambaza

taarifa za masoko yalitolewa kwa wakusanyaji wa taarifa za masoko ya mazao wapatao 72 kutoka Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutoa vitendea kazi kwa wakusanyaji wa taarifa za masoko 72 kutoka katika Halmashauri za Miji na Wilaya ili kuboresha ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko ya mazao. Vitendea kazi vilivyogawiwa ni pamoja na kompyuta 14 ambazo tayari zimeanza kutumiwa katika kuhifadhi taarifa za masoko katika miji mikuu ya mikoa. Kompyuta nyingine 6 zitagawiwa kwa watoa taarifa za masoko baada ya kupatiwa mafunzo ya kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Viwanda na Biashara imeendesha warsha mbili za kuelimisha na kuhamasisha wadau juu ya fursa za biashara za mazao ya kilimo zinazotokana na Itifaki ya Umoja wa Forodha kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo imeanza kutekelezwa mwezi Januari 2005. Warsha hizo zilifanyika kikanda katika miji ya Mwanza na Zanzibar.

Warsha ya Jijini Mwanza ilihuisha wajumbe kutoka mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga na Mara. Wajumbe walioshiriki katika warsha ya Zanzibar walitoka katika mikoa ya Tanga, Pwani, Morogoro, Dar es Salaam na mikoa yote ya Tanzania Visiwani. Wizara itaendelea kuelimisha wadau mbalimbali katika mikoa iliyobaki kuhusu kanuni na taratibu za masoko na biashara za mazao ya kilimo kwa nchi za nje chini ya ushirikiano wa Jumuiya mbalimbali, ili waweze kuzitumia fursa zinazojitokeza kutokana na makubaliano mbalimbali ya kibiashara (*Regional and International Trade Agreements*).

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa mazao ya biashara asilia katika mwaka 2004/2005 umeongezeka ukilinganishwa na wa mwaka 2003/2004. Aidha, wastani wa bei ya mkulima (*producer price*) umeongezeka, isipokuwa kwa pamba mbegu. Katika mwaka 2004/2005 ununuzi wa kahawa uliongezeka kwa asilimia 31.6 hadi kufikia tani 54,460 ikilinganishwa na tani 41,369 zilizonunuliwa mwaka 2003/2004. Ongezeko la ununuzi huo linatokana na kuanza kuimarika kwa bei ya kahawa katika soko la dunia kufuatia miaka mingu ya maporomoko ya bei ya zao hilo katika soko la dunia. Kwa sababu hiyo, bei ya kahawa aina ya arabica inayozalishwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya na Ruvuma) iliongezeka kutoka wastani wa Shilingi 350 kwa kilo msimu wa 2003/2004 na kufikia wastani wa Shilingi 683 kwa kilo msimu wa 2004/2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 95.

Bei ya kahawa ya aina hiyo hiyo inayozalishwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha iliongezeka kutoka Shilingi 500 kwa kilo hadi kufikia Shilingi 875 kwa kilo katika msimu wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 75. Kwa upande wa kahawa aina ya robusta, bei ya mkulima iliongezeka kutoka Shilingi 180 kwa kilo msimu wa 2003/2004 hadi kufikia wastani wa Shilingi 240 kwa kilo ikiwa ni ongezeko la asilimia 33. Ununuzi wa kahawa uliongezeka kutoka tani 41,369 katika mwaka 2003/2004 hadi kufikia tani 54,460 katika mwaka 2004/2005.

Aidha, kahawa iliyouzwa nje ya nchi iliongezeka kutoka tani 33,536 ambayo iliingiza Dola za Marekani milioni 2.2 katika msimu wa 2003/2004 na kufikia tani 35,026 ambazo ziliingiza Dola za Marekani milioni 3.51 katika msimu wa 2004/2005. Jumla ya tani 2,633 za kahawa ziliuzwa moja kwa moja nchi za nje (*direct exports*) ikilinganishwa na tani 724 zilizouzwa katika mfumo huo msimu wa 2003/2004. Mauzo hayo yaliingiza Dola za Marekani milioni 6.6.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa zao la pamba katika msimu wa 2004/2005 ulikuwa ni wa kihistoria kwani uliongezeka kwa asilimia 144 na kufikia tani 341,588 za pamba mbegu toka tani 139,756 katika msimu wa 2003/2004.

Aidha, hadi kufikia Aprili 2005, mauzo ya pamba nyuzi yalifikia tani 79,259 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 87 ikilinganishwa na mauzo ya tani 38,412 yaliyoingiza Dola za Marekani 42,208 katika msimu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, bei ya zao la pamba kwa wakulima iliathiriwa na kuporomoka kwa bei ya zao hilo katika soko la dunia kutoka wastani wa Dola za Marekani 1.54 kwa kilo ya pamba nyuzi msimu wa 2003/2004 hadi wastani wa Dola za Marekani 1.08 kwa kilo msimu wa 2004/2005 ikiwa ni anguko la asilimia 30.

Kushuka huku kwa bei ya pamba katika soko la dunia kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hilo ambapo jumla ya tani milioni 26.13 za pamba nyuzi zilizalishwa msimu wa 2004/2005 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 23.24 milioni. Ongezeko la ununuzi kwa mazao mengine ilikuwa kama ifuatavyo: Kahawa 45%, tumbaku 41%, mkonge 12%, chai (8%) na korosho 2%. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko la uzalishaji wa korosho kutoka takriban tani 80,000 katika mwaka 2003/2004 na kufikia tani 81,600 katika mwaka 2004/2005, jumla ya tani 71,920 za korosho zilinunuliwa kutoka kwa walizalishaji katika msimu wa mwaka 2004/2005. Wakulima walilipwa wastani wa Shilingi 750 na Shilingi 600 kwa kilo korosho za daraja la juu (*standard grade*) na daraja la chini (*under grade*). (*Makofî*)

Aidha, jumla ya tani 70,668 za korosho ghafi ziliuzwa nje ya nchi katika msimu wa mwaka 2004/05 ikilinganishwa na tani 76,771 katika msimu wa mwaka 2003/2004. Kiasi kikubwa cha korosho (98%) ziliuzwa nje kama korosho ghafi na India imekuwa mnunuzi mkuu wa korosho kutoka Tanzania. Wastani wa bei ya kuuzia korosho nje ya nchi katika msimu wa 2004/2005 ulikuwa Dola za Marekani 950 kwa korosho za daraja la juu na Dola za Marekani 750 kwa korosho za daraja la chini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kiasi cha korosho kilichouzwa nje kupungua, mapato ya fedha za kigeni yaliongezeka kwa asilimia 27 kutoka Dola za Marekani milioni 51.2 katika mwaka 2003/2004 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 65 katika mwaka 2004/2005. Hali hii inaashiria kwamba bei ya korosho katika soko la nje iliimarika katika msimu wa 2004/2005 ikilinganishwa na msimu wa 2003/2004. Kiasi cha korosho zinazobanguliwa ni kidogo sana ingawa uuzaji wa korosho unaleta faida zaidi ikilinganishwa na uuzaji wa korosho ghafi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 bei ya wastani ya majani mabichi ya chai imekuwa Shilingi 90 kwa kilo. Hata hivyo, wanunuzi wamekuwa wanatoa kati ya Shilingi 65 hadi 115 kwa kilo ya majani mabichi ya chai. Mauzo ya chai katika soko la ndani yaliongezeka kutoka tani 3,225 katika msimu wa 2003/2004 hadi kufikia tani 3,782 katika msimu wa 2004/2005. (*Makofi*)

Thamani ya chai iliyouzwa ilikuwa Shilingi bilioni 8.9 na 10.8 katika vipindi hivyo sawia (*respectively*). Wanunuzi wakubwa wa chai katika soko la ndani ni *Tanzania Tea Packers Limited* (TATEPA), *Tanzania Tea Blenders (2001) Limited* (TTBTL) na *International Packers Ltd.* Usindikaji wa chai nao uliongezeka kutoka tani 30,529 katika mwaka 2003/2004 na kufikia tani 31,996 katika msimu wa 2004/2005. Kampuni ya *Unilever (T) Limited* ilizalisha zaidi ya asilimia 35 katika vipindi vyote viwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 mauzo ya chai nchi za nje yalipungua kutoka tani 22,106 na kufikia tani 17,372. Mapato kutokana na mauzo hayo yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 27.5 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 20.9. Wastani wa bei ya chai katika masoko ya nje ulipungua hadi kufikia dola za Marekani 1.2074 kwa kilo kutoka Dola za Marekani 1.2446 kwa kilo. Kiasi kikubwa cha chai ya Tanzania huuzwa kuititia mnada uliopo Mombasa Kenya. Mauzo ya moja kwa moja katika nchi ya Uhlanzi, Uingereza, Pakistan na Singapore yanachukua kiasi kukubwa cha chai inayozalishwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa zao la pareto umeendelea kuwa wa kiwango kidogo kutokana na matatizo ya upatikanaji wa soko lenye uhakika nchi za nje ambako takriban pareto yote inayozinduliwa nchini. Ununuzi wa maua ya pareto umepungua kutoka tani 649 katika msimu wa 2003/2004 hadi kufikia tani 240 katika msimu wa 2004/2005. Aidha, bei ya pareto ya daraja la kwanza imebaki kuwa Shilingi 360 katika misimu yote miwili. Kwa kiasi kikubwa, uhaiifu wa soko la pareto ulimwenguni umetokana na kuwepo na ushindani wa bidhaa igiza (*synthetics*) ambazo zinatengenezwa kwa gharama nafuu zaidi. Mwenendo wa soko hilo unaonyesha kuwa pareto itapata soko katika miaka ya karibuni baada ya kuridhiwa kwa mikataba ambayo inaelekeza kupunguza na hatimaye kusitisha matumizi ya bidhaa igiza. Aidha, jitihada za kuwekeza katika kiwanda kitakachosafisha sumu ya pareto (*Refinery*) na hivyo kutengeneza dawa zitakazotumika moja kwa moja, siyo tu kutaongeza thamani ya pareto itakayozalishwa nchini bali pia itaongeza ajira katika sekta ya pareto. Kiwanda kinachozindua Pareto (*TPPMCL*) tayari kimeandaa mpango wa kujenga kiwanda cha kusafisha sumu ya Pareto. Aidha, Serikali itasaidia kwa kuweka mazingira yatakayoharakisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa sukari uliongezeka hadi kufikia tani 229,617. Katika kufikia lengo hilo, ununuzi wa miwa kutoka kwa wakulima wa nje (*out growers*) uliongezeka kutoka tani 669,609 katika mwaka 2003/2004 hadi kufikia tani 751,727 katika mwaka 2004/2005. Bei ya kununulia miwa kutoka kwa wakulima iliongezeka kidogo sana katika kipindi hicho yaani kutoka Shilingi 22,328 hadi Shilingi 22,635 kwa tani kwa wakulima wa Kilombero. Wakulima wa Mtibwa walipata ongezeko la kutoka Shilingi 18,000 hadi 18,500 kwa tani katika vipindi hivyo sawia. Mauzo ya sukari nchini

yalikuwa tani 207,339 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 380,411. Thamani ya mauzo ya sukari hiyo nchini ilikuwa Shilingi bilioni 111.6. Uuzaji wa sukari nje ya nchi ulipungua kutoka tani 22,723 katika mwaka 2003/2004 hadi kufikia tani 22,278 katika mwaka 2004/2005. Kwa kiasi kikubwa sukari hiyo iliuzwa katika jumuia ya Ulaya kufuatia makubaliano na mikataba ya soko la upendeleo. Kwa wastani bei ya sukari iliyouzwa nje ilibakia kuwa Dola za Marekani 494 kwa tani katika misimu yote miwili. Jumla ya Dola za Marekani milioni 12.6 zilipatikana kutokana na mauzo ya sukari nje ya nchi katika mwaka 2004/2005. Kufuatia kuanzishwa kwa mpango maalum wa kuongeza ufanisi na faida kwa Wazalishaji wa Sukari, Jumuiya ya nchi za Ulaya, immeanzisha utaratibu wa kuisaidia nchi yetu kuuza sukari nyingi zaidi na kwa bei ya juu katika nchi za Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya maua na mboga mboga nchi za nje iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 13.7 katika kipindi cha mwaka 2003/2004 na kufikia Dola za Marekani milioni 14.3. Ongezeko hili ni takriban asilimia 5.2 na kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa uwungi na ubora ambaa unaambatana na kufuata masharti ya uzalishaji na pia bei za bidhaa hizo katika soko la dunia. Ili kupunguza gharama za usafirishaji wazalishaji na wauzaji wa mboga mboga na maua wanakamilisha taratibu za kupata ndege itakayosafirisha bidhaa hizo moja kwa moja badala ya utaratibu wa hivi sasa wa kuitopia Kenya.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alivyoeleza wakati akitoa hotuba ya Bajeti ya Wizara yake, msimu wa kilimo wa 2004/2005 umeonyesha mwelekeo mzuri katika upatikanaji wa mazao ya chakula ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2003/2004. Hali hiyo inajidhihirisha wazi zaidi kwa kuangalia mwenendo wa bei za mazao ya chakula katika msimu wa mwaka 2004/2005. Kwa mfano, bei ya gunia la mahindi la kilo 100 katika jiji la Dar es Salaam ilikuwa ni wastani wa Shilingi 16,500 katika mwezi wa Aprili 2005 ikilinganishwa na Shilingi 24,500 katika mwezi Aprili, 2004. Katika jiji la Arusha bei ya gunia la mahindi la kilo 100 katika mwezi Aprili 2005 ilikuwa Shilingi 19,000 ikilinganishwa na wastani wa bei ya Shilingi 26,000 katika mwezi Aprili, 2004. Bei ya mchele katika Jiji la Mwanza ilikuwa Shilingi 50,000 kwa gunia la kilo 100 katika mwezi Aprili, 2005 ikilinganishwa na Shilingi 57,500 katika mwezi Aprili, 2004 kwa kiasi hicho cha mchele. Kwa ujumla mwenendo wa bei za mazao makuu ya chakula umekuwa ni wa kuridhisha na hivyo kuwezesha Wananchi wengi kumudu upatikanaji wake wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 uuzaji wa mahindi nje ya nchi ulikuwa jumla ya tani 139,204 zenye thamani ya Shilingi bilioni 17.1 ikilinganishwa tani 49,040 zenye thamani ya Shilingi bilioni 8.1 katika mwaka 2004. Kiasi kidogo cha mauzo ya mahindi katika mwaka 2004 kilitokana na upungufu wa uzalishaji mahindi nchini kutokana na ukame. Kufuatia hali hiyo ya ukame, mahindi yaliyoingizwa nchini yaliongezeka kutoka tani 20,713 yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.5 katika mwaka 2003 hadi kufikia tani 82,288 yenye thamani ya Shilingi bilioni 18.9. Uuzaji wa mchele nje ya nchi katika mwaka 2004 pia ulipungua hadi kufikia tani 508 zenye thamani ya Shilingi milioni 125.5 ikilinganishwa na tani 5,037 zenye thamani ya Shilingi milioni 671 zilizouzwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ununuzi na uuzaaji wa mazao makuu ya chakula uliendelea kukabiliwa na tatizo la uduni wa miundo mbinu ya masoko, hususan barabara za vijijini, magulio au vituo vya kuuzia na kununulia pamoja na jitihada za Serikali na Halmashauri za kujenga masoko na magulio ya mazao hayo. Hali hii imesababisha kuwepo kwa gharama kubwa za kununua na kuuza mazao na pia sehemu kubwa ya mazao kuharibika kabla au baada ya kufikishwa sokoni. Aidha, wafanyabiashara wadogo wa mazao ya chakula wameendelea kukabiliwa na ukosefu wa mitaji ya kufanya biashara zao. Hata hivyo, katika siku za hivi kumekuwa na ongezeko la usindikaji wa nafaka na hivyo kuongeza thamani na maisha (*shelf life*) ya mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mifugo yetu pamoja na mazao yake kukosa viwango vya ubora vya masoko ya Kimataifa kutokana na kuwepo kwa magonjwa na hivyo kutegemea zaidi soko la ndani, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha bidhaa hizo ziweze kuuzwa katika masoko ya Kimataifa. Nchi yetu tayari inauza mifugo katika nchi za Ghuba na Visiwa vya Comoro (Ngazija). Katika mwaka 2004 uuzaaji wa mifugo nje ya nchi umeliingizia Taifa jumla ya Shilingi milioni 209.4 ikilinganishwa na Shilingi milioni 327.6 zilizopatikana katika biashara ya mifugo nchi za nje mwaka 2003. (takwimu za TRA).

Aidha, kwa kuwa sekta ya mifugo hutegemea kwa kiasi kikubwa soko la ndani ambalo linazidi kukua, Serikali kuitia mradi wa Kuendeleza Masoko ya Mifugo nchini (*Tanzania Livestock Marketing Project (TLMP)*) imeendelea kuendeleza miundombinu ya masoko ya mifugo na pia kuhamasisha matumizi ya bidhaa za mifugo zinazozalishwa hapa hapa nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, takwimu za uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku msimu wa 2004/2005 haukubadilika sana ikilinganishwa na uzalishaji wa nyama msimu wa 2003/2004. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 20 wakati uzalishaji wa mayai uliongezeka kwa asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2004/2005, ununuzi wa ngozi za za ng'ombe, mbuzi na kondoo uliongezeka kwa asilimia 4 ikilinganishwa na msimu wa 2003/2004. Pamoja na ongezeko hilo, mapato ya wafugaji kutokana na ngozi hizo yalipungua kwa asilimia 15. Kiasi cha mauzo ya ngozi nje ya nchi katika kipindi hicho kilishuka kwa asilimia 7 ingawaje mapato yaliyotokana na mauzo hayo yaliongezeka kwa asilimia 61.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni Mradi wa Kuendeleza na Kuboresha biashara na masoko ya mazao ya Pamba na Kahawa. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Mazao (*Common Fund for Commodities (CFC)*) pamoja fedha za hapa. Mradi unajihusisha pamoja na mambo mengine na kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala kama dhamana ya kupata mikopo (*Commodity Warehouse Receipt System*). Katika mwaka 2004/2005 kwa kuitia uratibu

wa mradi huu Benki za *CRDB*, *EXIM* na *KCB* zilitoa mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 8.6 kwa utaratibu wa dhamana hizo kwa zao la kahawa. Aidha, Benki ya *CRDB* ilitoa mkopo ya Shilingi 220,000,000 kwa zao la pamba. Fanikio jingine kubwa la mradi huu katika mwaka 2004/2005 ni kushiriki kwa mafanikio ya utungaji wa Sheria inayohusika ya Stakabadhi za Mazao kwenye maghala kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuendeleza Masoko ya Mazao Vijijini uliotekelizwa chini ya ufadhilli wa wa Serikali ya Ufaransa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ultakiwa kukamilika tarehe 31 Desemba, 2004. Hata hivyo, kutokana na kutokamilika kwa baadhi ya vipengele vya mradi na pia kutoa muda wa kutosha wa uangalizi na kufuatilia ubora wa kazi za ujenzi kabla ya kukabidhiwa rasmi, Serikali zote mbili zilikubaliana kuongeza muda wa miezi sita ili kukamilisha Mradi huu tarehe 30 Juni, 2005. Utekelezaji wa Mradi huu umekamilisha mambo yafuatayo: -

- (i) Ujenzi wa Soko la mahindi katika Mji Mdogo wa Kibaigwa na barabara yenye urefu wa mita 800 kwa kiwango cha lami inayounganisha soko hilo na barabara kuu ya Dodoma – Morogoro;
- (ii) Ujenzi wa masoko ya matunda katika Vijiji vya Tawa na Kinole katika Wilaya Morogoro;
- (iii) Ujenzi wa soko la matunda na mboga mboga la Nyandira katika Wilaya Mvomero;
- (iv) Ujenzi wa barabara zenyе urefu wa kilomita 39.2 katika maeneo yanayounganisha masoko ya Nyandira, Tawa na Kinole;
- (v) Ujenzi wa madaraja makubwa mawili kwenye mito ya Mbezi na Manga na ukarabati wa daraja moja la mto Mvuhu;
- (vi) Uimarishaji miundo mbinu ya umwagiliaji na upatikanaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani katika Kijiji cha Nyandira;
- (vii) Ujenzi wa vituo vya mafunzo kwa wakulima na wafanyabiashara katika maeneo ya Kibaigwa, Kinole na Tawa na ukarabati wa kituo cha mafunzo katika Kijiji cha Nyandira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilika kwa ujenzi huu, yamejitokeza matatizo madogo ya utendaji katika baadhi ya masoko hayo, hususan katika soko la Kimataifa la Mahindi Kibaigwa yamejitokeza masoko mengine yasiyo rasmi kuzunguka soko hilo. Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Dodoma imeishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kuzifanyia mapitio sheria za kununua na kuza mazao katika masoko hayo ili kuhakikisha kuwa ununuzi wa mazao unafanyika katika

soko lililojengwa ili kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao zinafuatwa (matumizi ya vipimo rasmi, ubora). Mapitio ya sheria hizo yamekwisha fanywa.

Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme*) ambayo ni ya miaka 7 katika mikoa 8 itakayohusisha Wilaya 36 umeanza kuzaa matunda katika baadhi ya vipengele. Hii ni pamoja na: -

Uandaaji wa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo. Kwa kiasi kikubwa maandalizi ya Sera hii yalifanywa kupitia programu hii. Kama ilivyoelezwa hapo awali maandalizi ya sera hii yamekamilika, na rasimu ya sera hiyo ipo katika hatua ya kujadiliwa na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri.

Kujasirisha Wakulima na Wafanyabiashara wa Mazao na Bidhaa za Kilimo na Kuwaunganisha na Masoko. Utekelezaji wa kipengele hiki cha Programu ulianza mwaka 2003/04 kwa kuhusisha Wilaya nane (8) za Babati, Arumeru, Hai, Muheza, Mufindi, Songea Vijijini, Mbeya Vijijini na Sumbawanga Vijijini. Moja ya malengo makubwa ya kipengele hiki ni kuimarisha vikundi vya wakulima, wasindikaji na wafanyabiashara ili hatimaye kuviunganisha na masoko.

Programu kwa kuzihusisha taasisi zisizo za Kiserikali ilitoa mafunzo kwa vikundi 157 vya uzalishaji, 16 vya wasindikaji na 22 vya wafanyabiashara katika Wilaya hizo 8 Aidha, kutokana na uhamasishaji wa Programu hii, idadi ya Wanachama wa *TCCIA* iliongezeka kwa asilimia 36 toka 346 hadi 471 katika Wilaya hizo. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na mchanganuo wa masoko ya mazao na stadi za biashara.

Utekelezaji wa kipengele cha uimarishaji wa miundombinu ya masoko ulizinduliwa rasmi mwezi Mei, 2004 baada ya taratibu za upatikanaji wa fedha kutoka *ADB* kukamilika. Uboreshaji wa barabara zilizoteuliwa na Halmashauri husika umeanza katika Wilaya za Babati, Arumeru, Hai, Muheza, Mbeya Vijijini, Sumbawanga Vijijini na Songea Vijijini. Ukarabati wa maghala umeanza katika Wilaya za Sumbawanga Vijijini, Mbarali na Babati. Maandalizi ya ujenzi wa masoko katika Wilaya za Babati, Arumeru, Hai, Muheza, Mbeya Vijijini, na Sumbawanga Vijijini yako katika hatua za mwisho.

Programu hii inaimarisha huduma za kifedha kwa kuwezesha Mfumo wa Stakabadhi za Mazao katika maghala kutumika. Programu hii inajielekeza zaidi katika kuainisha na kujenga maghala ambayo yanaweza kutumika kwenye mfumo huo. Programu imekwishakagua na kuthibitisha ubora wa maghala 84. Kwa kuanzia maghala manne yameteuliwa na kuanza kutumika yakiwemo mawili (2) Wilaya ya Babati, moja (1) Wilaya ya Mbarali na moja (1) Wilaya ya Sumbawanga. Programu hii inakamilisha pia taratibu za kuwezesha Vyama vya Ushirika vya Akiba na mikopo vitumike kwenye mfumo huu wa kutumia stakabadhi za mazao kwenye maghala kama dhamana ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirika na Masoko katika mwaka 2004/2005 iliendelea kutekeleza masuala muhimu yafuatayo yanayohusu maendeleo ya watumishi na uboreshaji wa mazingira ya kazi kama ifuatavyo: -

- (i) Wizara imeendelea na mpango wake wa kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake, ambapo jumla ya watumishi 125 wa Wizara walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali hapa nchini na nchi za nje ili kuwapatia uzoefu na ujuzi zaidi. Aidha, katika kipindi hiki, watumishi watano (5) walidhaminiwa na Wizara katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili. Pia, Maafisa Ushirika 159 walidhaminiwa na Wizara kwa Mafunzo mbalimbali katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vyuo vingine nchini;
- (ii) Katika kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi Wizara imeshughulikia ajira za watumishi mbalimbali ili kujaza nafasi zilizo wazi. Jumla ya watumishi 21 wameajiriwa Wizarani katika mwaka wa 2004/2005;
- (iii) Wizara pia imeendelea na zoezi la kuwapandisha Vyeo watumishi na kuwathibitisha kazini. Kwa kipindi hiki jumla ya watumishi 18 walipandishwa vyeo;
- (iv) Wizara imeendelea kuendesha Mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa ngazi zote kuhusu dhana ya Utawala Bora inayohusu uwazi na uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kuzingatia utawala wa haki na sheria. Jumla ya watumishi 120 wa Wizara na Maafisa Ushirika 100 wa Halmashauri za Wilaya walipatiwa mafunzo hayo;
- (v) Katika kipindi cha 2004/2005, Wizara pia imehusisha Sekta Binafsi katika utoaji huduma (*Private Sector Participation*) kwa kuingia Mikataba na Sekta Binafsi katika kutoa huduma ya usafi wa ofisi na mazingira yake;
- (vi) Wizara iliendelea kuimarisha Ofisi za watumishi wa Wizara kwa kununua vitendea kazi mbalimbali na samani kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi;
- (vii) Mapambano dhidi ya Janga la Ukimwi yaliendelea na Wizara imetayarisha mkakati wake wa miaka mitatu kuhusu mapambano dhidi ya janga hili. Semina fupi kwa watumishi wa Wizara kuhusu janga hili ulifanywa pia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Wizara ya Ushirika na Masoko ilitengewa jumla ya Shilingi 11,403,061,500 kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 7,336,242,500 zilikuwa za Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengine) na Shilingi 4,066,819,000 zilikuwa za Matumizi ya Maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2004 jumla ya Shilingi 7,161,742,406 fedha za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimetolewa na kiasi cha Shilingi 7,156,848,132.74 zimetumika, sawa na asilimia 97.6 ya fedha zilizoidhinishwa. Kwa

upande wa Bajeti ya Maendeleo jumla ya Shilingi 3,147,783,104 zimetumika. Kati ya fedha hizi Shilingi 169,300,000 ni fedha za ndani na Shilingi 2,978,483,104 ni fedha za nje. Aidha, katika mwaka wa 2004/2005 Wizara ilipewa na kutumia nyongeza ya Shilingi 642,340,308 kwa matumizi maalum. Kati ya fedha hizo Shilingi 524,000,000 ziliwu ni kwa ajili ya kulipa madai ya wakulima, Shilingi 20,000,000 kwa ajili ya kupambana na vita ya dhidhi ya rushwa na Shilingi 98,340,308 kwa ajili ya nyongeza ya mishahara ya Shirika la *COASCO*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara itaendelea na juhudzi za kujenga ushirika mpya wa karne ya 21 na kuendeleza masoko ya mazao ya kilimo kwa kuzingatia mabadiliko ya sera za kijumla za uchumi pamoja na sera na sheria za sekta. Aidha, mpango huu wa kazi umeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Bajeti ya Serikali (*Medium Term Expenditure Framework (MTEF)*) kwa kipindi cha 2005/2006 - 2007/2008 uliotolewa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha. Mpango huu pia umezingatia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Kazi zilizopangwa kutelezwa zimeainishwa katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, kwenye eneo la Sera, Sheria na Mipango, Wizara itafanya kazi zifuatazo:

- (i) Kuandaa Mkakati wa kutekeleza Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ya mwaka 2005;
- (ii) Kuendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka wa 2002, Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka wa 2003 na Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo;
- (iii) Kuandaa Kanuni na Taratibu (*Rules and Regulations*) za Sheria ya kusimamia Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao kwenye Maghala (*The Warehouse Receipt Act No.10 of 2005*) ili kuwezesha Sheria hiyo ianze kutekelezwa kwa ufanisi;
- (iv) Kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme - ASDP*) kwa kuainisha miradi ya maendeleo, hususan Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo katika Wilaya (*District Agricultural Development Plans (DADPs)*);
- (v) Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuandaa Mkakati wa Kudhibiti Ukimwi kwa Sekta ya Kilimo;

- (vi) Kufanya mapitio ya muundo wa Wizara na kuurekebisha ili ukidhi mahitaji ya wakati, hususan katika kutekeleza Programu kamambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini na katika kutoa huduma za kisasa zinazohitajika kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ushirika ni muhimu katika kutekeleza MKUKUTA kwa vile inagusa asilimia kubwa ya Watanzania walio wazalishaji, wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo wanaotegemea kilimo. Ili kufanikisha azma hiyo katika eneo hili Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yafuatayo:

- (i) Kuendeleza mchakato wa kuchagua viongozi wapya katika Vyama vya Ushirika wenye sifa na maadili kulingana na matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003;
- (ii) Kukamilisha utaratibu wa kuanzisha Benki ya Ushirika ya Taifa (*National Cooperative Bank*);
- (iii) Kuendelea na utekelezaji wa programu kamambe ya Kurekebisha Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika (*Cooperative Reform and Modernisation Programme*);
- (iv) Kuendelea kuvikutanisha Vyama vya Ushirika na Benki za Biashara kwa lengo la kuviwezesha kupata mikopo kwa ajili ya kuendeshea shughuli muhimu, hususan ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wakulima. Pia, kuimarisha mitaji ya ndani ya Vyama vya Ushirika kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhamasisha Wanachama kuongeza hisa, kuanzisha na kuimarisha *SACCOS* na kuweka utaratibu mzuri wa matumizi ya sehemu ya ziada ya mwaka;
- (v) Kwa kushirikiana na wadau wengine Wizara itaendelea kuhamasisha Wananchi kwa kasi zaidi katika kuanzisha Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Lengo ikiwa ni kuhamasisha jamii kuhusu Ushirika kama chombo cha kumkomboa mwananchi/mkulima/mfanyakazi na mfanyabiashara mwenye kipato kidogo katika kupunguza umaskini. Mkazo utawekwa kwenye shughuli za uvuvi, uchimbaji madini, ufugaji, umwagiliaji maji mashambani na viwanda vidogo vidogo vya usindikaji;
- (vi) Kwa kutumia Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Hesabu za Vyama vya Ushirika (*COASCO*) kuendelea kutekeleza programu ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na kuhakikisha kuwa taarifa za ukaguzi zinawasilishwa kwa wanachama wote kama inavyotakiwa kwa wakati;
- (vii) Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu Sokoine cha Kilimo kuendelea kutoa elimu ya Ushirika shirikishi kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuwajasirisha ili wamiliki na kuviendesha vyama vyao;

- (viii) Kuendelea kutoa miongozo ya uendeshaji ili kusaidia kuboresha utendaji wa Vyama vya Ushirika, hususan Vyama vya Msingi;
- (ix) Kutoa mafunzo ya upangaji mipango ya bajeti katika Wilaya na Vyama vya Ushirika yenyenye mtazamo wa ushiriki wa kijinsia kwa watendaji wa ngazi zote;
- (x) Kuendelea kuwawezesha maafisa Ushirika Wilayani kutekeleza kazi zao ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo na vitendea kazi kama vile pikipiki na kompyuta;
- (xi) Kuendelea kuratibu kazi ya kuhuisha muundo na uendeshaji wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*Tanzania Federation of Cooperatives*) na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (*Savings and Credit Union League of Tanzania (SCCULT)*). Kazi hii ambayo imeshaanza inafanywa na Washauri Waelekezi na inatarajiwaa kukamilishwa mwezi Septemba, 2005. Kazi hii itaviwezesha Vyama hivi kufanya shughuli zao kwa ufanisi kwa kuzingatia mwelekeo wa ushirika mpya tunaotaka kuujenga; na
- (xii) Kuunda Baraza la Ushauri la Kitaifa (*Natural Advisory Council*) ambalo kazi zake zitakuwa ni pamoja na kutoa ushauri katika masuala ambayo yataleta sura mpya katika uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Aidha, ushauri huo utatolewa kwa Serikali na wadau ili waweze kuufanyia kazi katika mchakato wa kuboresha uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Baraza hilo litaundwa na Wajumbe kutoka kwenye Asasi/Taasisi za Ushirika, hususan Idara ya Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika cha Biashara na Stadi za Biashara, Moshi na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa masoko ya mazao na bidhaa za kilimo siyo tu utaongeza kipato cha wakulima bali pia utachochea uzalishaji zaidi wa mazao na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Kwa sababu hiyo Wizara itayapa kipaumbele mambo yafuatayo katika kukuza soko la mazao ndani na nje ya nchi: -

- (i) Kuendelea kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za ushirika na masoko, kwa kuzingatia mahitaji ya wadau/watumiaji;
- (ii) Kutoa elimu kupitia warsha/semina, katika kuhamasisha wakulima, wazalishaji na wafanyabiashara wadogo wadogo jinsi ya kutumia taarifa mbalimbali za masoko ili kuendeleza kuuza/kununua mazao kulingana na mahitaji ya soko;

- (iii) Kuelimisha na kuhamasisha wakulima na wazalishaji juu ya matumizi ya vipimo sahihi wakati wa kuuza mazao kwenye magilio na vituo/masoko ili kuepuka udanganyifu;
- (iv) Kuhamasisha na kuwezesha wakulima, wasindikaji na wafanya biashara juu ya umuhimu wa kusindika mazao kabla ya kuyauza ili kuongeza ubora na thamani. Lengo likiwa ni kupata bei nzuri, masoko ya uhakika na kuongeza ajira; hususan kwa mazao ya pamba, korosho, matunda na nafaka;
- (v) Kuwezesha Halmashauri za Wilaya kuwa na vitendea kazi vya kukusanya, kuchambua na kutunza taarifa za masoko katika maeneo yao. Vitendea kazi hivi ni pamoja na vifaa vya kukusanya takwimu/taarifa, vyombo vya usafiri na kompyuta. Hatua hii itawezesha kujenga benki za takwimu za masoko ambazo zitatumika kwa manufaa mbalimbali;
- (vi) Kuendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali na kutoa elimu ya kanuni na taratibu za masoko ya nchi mbalimbali za nje, hususan nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Amerika na nchi za Umoja wa Ulaya kwa wafanyabiashara ili waweze kuzizingatia kwa urahisi wanapoamua kufanya biashara katika masoko ya nchi hizo;
- (vii) Kuendelea kufanya tafiti za gharama za kuuza na kununua mazao (*Marketing costs*) kwa lengo la kupendekeza njia za kupunguza gharama zisizo za lazima;
- (viii) Kuratibu na kufanya tathmini ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya masoko katika sehemu maalum. Tathmini itaanzia na ujenzi wa soko la mboga mboga na matunda katika mji mdogo wa Segera na soko la nafaka na bidhaa mchanganyiko katika mji mdogo wa Makambaku;
- (ix) Kuendelea na juhudzi za kuimarishe soko la ndani kwa kuunda Kamati Maalum ya kushughulikia uimarishaji huo. Mambo muhimu ya kuzingatia na Kamati hiyo ni kuwa na sehemu maalum ambapo taarifa za masoko ya mazao na bidhaa za kilimo zitapatikana kila wakati. Hii ni pamoja na kuwa na *Agribusiness Directory* na sehemu za kudumu za Maonyesho ya Mazao na Bidhaa za Tanzania (*Permanent Display Centres*);
- (x) Kuandaa utaratibu bora wa kuendesha na kusimamia miundo mbinu ya masoko ikiwa ni pamoja na kutathmini uwezekano wa kutumia Kampuni maalum za Menejimenti;
- (xi) Kuendelea kuratibu shughuli za vikundi na taasisi zisizo za Kiserikali (*NGOs, CBOs* na Makampuni) zinazojishughulisha na ununuza, usindikaji na uuzaji wa mazao na bidhaa za kilimo, zikiwemo zile

zinazowaunganisha wakulima na masoko kwa kutumia kilimo cha mikataba (*contract farming*); na

- (xii) Kuendeleza mazungumzo yaliyokwishaanza na Makampuni makubwa ya nchi za nje kwa lengo la kufanya nao biashara ya moja kwa moja kwa kuanzia na mazao ya Pamba, Kahawa, Chai na Korosho. Kwa mfano, mazungumzo yataendelea na Kampuni ya Migros na *Cooperative Marketing Chain* ya Uswisi kwa ajili ya bidhaa mbalimbali na Makampuni ya Pakistan kwa ajili ya Chai na Makampuni ya Uhlanzi kwa ajili ya Korosho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kuratibu, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ifuatayo: Mradi wa Kuendeleza na Kuboresha Biashara ya Pamba na Kahawa (*Coffee/Cotton Marketing Development and Trade promotion Project*). Katika mwaka wa 2005/2006 kazi zifuatazo zitatekelezwa chini ya mradi huu: -

- (i) Kukamilisha taratibu za kisheria, uhamasishaji na kutoa mafunzo kwa wadau ili kuwezesha matumizi ya Stakabadhi za Mazao yaliyopo ghalani kama dhamana ya mikopo kutoka katika vyombo vyta fedha.
- (ii) Kuendeleza juhudini za kuimarisha ubora wa mazao ya kahawa na pamba.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Systems Development Programme (AMSDP)*) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wengine katika maeneo yafuatayo: -

- (i) Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa kutekeleza Sera ya Masoko ya Mazao.
- (ii) Kupitia na kuboresha Sheria, Kanuni na Taratibu za ununuzi wa mazao ili zikidhi mahitaji mbalimbali ya mfumo wa soko uliopo hivi sasa;
- (iii) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko kwa kuongeza wigo wa taarifa hizo;
- (iv) Kuvijengea uwezo vikundi vya uzalishaji, usindikaji na vya wafanyabisha kwa lengo la kuviunganisha vikundi hivyo na masoko maalumu; na
- (v) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya masoko katika Wilaya ambazo programu hii itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006 Wizara itatekeleza kazi zifuatazo kuhusu maendeleo ya watumishi: -

- (i) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi (*in-house*) kwa watumishi wa ngazi zote yakiwemo ya kikazi na yale ya kupiga vita rushwa na UKIMWI sehemu za kazi;
- (ii) Kuendeleza watumishi kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;
- (iii) Kuendelea kushughulikia ajira za watumishi, upandishwaji vyeo na kuthibitisha kazini watumishi wa Wizara;
- (iv) Kuimarisha utendaji kazi na upimaji wa malengo (*Performance Management System*) kulingana na maelekezo ya programu ya uimarishaji wa utumishi wa umma; na
- (v) Kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika utoaji huduma (*Private Sector Participation*) kwa kuingia mikataba na Sekta Binafsi katika kutoa huduma ya ulinzi na mapokezi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara yangu katika juhudzi za kuendeleza Ushirika na Masoko. Kwanza, napenda kuzishukuru nchi za Norway, Ufaransa, Kenya na Afrika ya Kusini. Vile vile, napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zikiwemo Benki ya Dunia, *International Cooperative Alliance, ILO, ICO, IFAD, ADB, CFC, UNCTAD* na *UNOPS*. Pamoja na shukrani hizo napenda kuwaomba waendelee kutusaidia kwani bado tunahitaji sana misaada yao.(*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ninayoiwasilisha leo hii imeandaliwa kwa ushirikiano wa watumishi wa Wizara ya Ushirika na Mosoko. Nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko; Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa. Mheshimiwa Chibulunje katika kipindi chote cha takriban miaka 4½ amenipatia msaada mkubwa sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kila ulipotakiwa kuniwakilisha ndani na nje ya nchi. Aidha, amekuwa mwepesi kujifunza mbinu za utekelezaji kila ilipobidi.

Nawashukuru pia Dr. Ladislaus Komba, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Wizara, Wakuu wa Taasisi iliyo chini ya Wizara, *COASCO*, Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Viongozi wa Bodi za Mazao, Viongozi wa Vyama vya Ushirika na wa vikundi vya uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali kwa kazi nzuri wanayofanya kwa pamoja katika kuimarisha na kuendeleza ushirika na masoko. Vile vile, tunawashukuru wadau wote wengine wanaoshughulika na biashara ya mazao ya kilimo na mifugo na bidhaa nytingine ndani na nje ya nchi. Aidha, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.(*Makofisi*)

Kwa kuwa huu ndio mwaka wa mwisho wa Serikali ya Awamu ya Tatu na wa Bunge hili, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais

Benjamin William Mkapa, kwanza kwa kunitua kuwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Kumshauri kuhusu Masuala ya Ushirika ya mwaka 2000 na pili kwa kunitua na kunipa fursa ya kuitumikia nchi yangu kama Waziri wa Kwanza wa Wizara mpya ya Ushirika na Masoko katika karne ya 21. Namshukuru pia kwa kuwa mstari wa mbele katika kuutetea na kuuimarisha ushirika hasa kwa kurejesha Wizara ya pekee ya Ushirika na Masoko baada ya hatua hii kupendekezwa na Kamati yake Maalum ya kumshauri kuhusu masuala ya Ushirika. (*Makofi*)

Napenda kuwashukuru vile vile Marais wetu wa Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ambao waliniamini kwa kunipa majukumu mbali mbali ya ujenzi wa Taifa letu. (*Makofi*)

Napenda kuwashukuru Wananchi wa Mkoa wa Kagera ambao walinchagua kwa mara ya kwanza kuwa Mbunge wao (Mjumbe wa Legco) mwaka 1957 kuwakilisha Mkoa uliojulikana kama *East Lake Province* na wakati huo huo kunipa nyadhifa za *General Manager* wa *BNCU (Bukoba Native Cooperative Union)* na Mwenyekiti wa *Bahaya District Council*, nyadhifa zote tatu kwa wakati mmoja. Nawashukuru pia Wananchi wa Jimbo la Karagwe, Kagera kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa miaka 10 mfululizo. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, lakini siyo kwa uzito, napenda kumshukuru Mke wangu na Mbia wangu wa kudumu katika maisha Mheshimiwa Janet Bina Kahama; Mbunge wa Viti Maalum CCM ambaye amenitunza, kuniangalia na kuniongoza kwa kipindi cha miaka zaidi ya 40 na anaendelea kufanya hivyo nikiwa katika madaraka mazito ya uongozi.

Kwake sina zawadi ya kumpa inayolingana na yote aliyonifanyia isipokuwa kumwahidi kuendelea kumpenda kwa moyo wangu wote na kumpa uaminifu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 7,681,937,900 ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yanayotarajiwa kufanya katika mwaka wa 2005/2006. Kati ya fedha hizo, Shilingi 7,170,437,900 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida pamoja na mishahara na Shilingi 511,500,000 ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo. Kati ya Fedha za Maendeleo, Shilingi 169,000,000 ni fedha za hapa nchini na Shilingi 342,500,000 ni fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. OMAR S. CHUBI (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITU WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa

Spika, naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni Na.81 (1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara, Kamati ilizingatia vipengele vifuatavyo kuhusu Fungu 24: -

- (i) Dira/Mwelekeo wa Wizara kuhusu Ushirika na Masoko Nchini.
- (ii) Majukumu ya Wizara.
- (iii) Taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya mwaka 2004/2005.
- (iv) Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya mwaka 2004/2005.
- (v) Maeleo kuhusu mapato na matumizi ya kawaida pamoja na fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005.
- (vi) Maeleo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida na miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kuitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na ushauri uliotolewa wakati wa bajeti ya mwaka 2004/2005, tunapenda kuipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali ilizofikia katika kutekeleza ushauri wa Kamati. Pia, Wizara imeweza kutekeleza kwa ufanisi malengo ya shughuli ilizojipangia. Ni matumaini ya Kamati kuwa juhudi hizo zitaendelezwa ili kupata mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Ushirika nchini pamoja na kuendeleza masoko ya ndani na nje ya nchi, Wizara pamoja na Mashirika yake kwa mwaka 2005/2006 inaomba fedha chini ya Fungu 24 kama ifuatavyo, fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 7,170,437,900/=, fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 511,600,000/= na jumla ni shilingi 7,681,937,900/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuitia na kuchambua mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii na kuridhika na kazi zinazotekelzwa, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao: -

Kwanza Serikali ijenge masoko makubwa ya Kimataifa hususan sehemu za mipakani ambapo wakulima wataweza kuuza mazao yao na hivyo kuiongezea kipato. Mfano wa soko la Kimataifa la Mahindi la Kibaigwa katika Wilaya ya Kongwa ni mwanzo mzuri na juhudi za kujenga masoko ya Segera (Tanga) na Makambako (Iringa) ziendelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kupata utaalam wa masoko ya Kimataifa, viongozi na watendaji watembelee masoko ya namna hiyo yaliyopo nchi nyingine kama Afrika Kusini ambako kuna soko kubwa la Kimataifa la mazao ya kilimo ya chakula kama viazi, mboga mboga na matunda ya Tshwane, Pretoria. (*Makofî*)

Pia Serikali iweke fedha za kutosha ili kuwezesha Tanzania kushiriki kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa sehemu mbalimbali duniani ili kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini na kupata masoko ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, utata uliopo kati ya Sheria ya Ushirika ambapo Maafisa Ushirika wanatakiwa kuwajibika kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika unakinzana na hali ya mabadiliko (*Reforms*) yanayotekelizwa na Halmashauri za Wilaya na Miji kuhusu Watumishi. Utaratibu huu unawafanya Maafisa Ushirika kuwajibika kwa Halmashauri wanazofanyia kazi na mara nyingine kuacha kufanya kazi walizoajiriwa.

Kamati inashauri kuwa ili tuweze kufufua Ushirika nchini, ni vema Maafisa hawa wafanye kazi zao za taaluma ya kueneza Sera na Mikakati ya Kuondoa Umaskini kuitia Ushirika wa Kawaida na wa Vyama vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) lijitangaze ili liendane na hali ya sasa ya ushindani na kwa mujibu wa Sheria mpya ya Shirika hilo iliyopitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2005. Aidha, Shirika hilo ambalo kwa juhudhi za Wizara na Bodi ya Wakurugenzi limeanza kupata watalaan wazuri, lipatiwe fedha za kununulia zana za kisasa za kufanya kazi kama kompyuta na kompyuta ndogo (*Laptops*).

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukushukuru kwa mara nyingine tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa George Clement Kahama, Mbunge na Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mbunge na Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, Katibu Mkuu wa Wizara Dr. Komba na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo kwa maandalizi mazuri ya taarifa zilizohitajika katika zoezi hili la kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo na pia kwa ushirikiano wao mzuri na Kamati hii kwa wakati wote. Mfano wa ushirikiano mzuri sana wa Wizara hii na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara unafaa uigwe na Wizara nyingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spka, napenda niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge amba ni Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara amba walichangia kikamilifu wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii. Napenda kuwatambua Wajumbe hao amba ni hawa kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Mbatia, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo,

Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ismail Ivvatta na Mheshimiwa Stephen Kazi.

Wengine ni Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Hebert Mntangi, Mheshimiwa Freeman Mbwe, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Sumri Mohammed, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha Mheshimiwa Semindu K. Pawa na Mheshimiwa Christopher Wegga.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani nyingi kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo yoyote. Vile vile, napenda kumshukuru Ndugu Aggrey Nzowa kwa kuhudumia Kamati kwa bidii wakati wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ili waweze kujiandaa, Waheshimiwa wanne watakaochangia mwanzoni ni Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Robert Mashala na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala.

**MHE. AISHA P. MAGINA – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kifungu cha 43 (5) (c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kupoteza mwakilishi wao Bungeni, Mheshimiwa Hayati Abu Towagale Kiwanga na familia ya Mzee Bwana, kwa kufiwa na ndugu yao mpendwa Mheshimiwa Hayati Margareth Bwana. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Balozi George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Ndugu Dr. Komba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirika na Masoko na timu yake ya wataalam waliosaidiana kuandaa Bajeti hii inayolenga kuinua ushirika Tanzania na kuboresha masoko ya mazao ya wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, kwa ajili ya kuwasilisha bajeti nzuri ya mwaka 2005/2006 ya Wizara hii, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba bado kuna maeneo yenye mapungufu ambayo yanahitaji jitihada madhubuti ya kuyaboresha ili kuleta ufanisi kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imepewa majukumu mengi yakiwemo ya kuendeleza asasi za ushirika na masoko kwa kuandaa, kusambaza, kusimamia sera na mifumo ya sheria kwa hali ya juu ya kitaalam na kwa njia ya ushirikishaji. Ushirika

unaoongeleta hapa ni ule ambao watu wote waliuzoea ambao ulikuwa ushirika wa mazao kama vile pamba, kahawa, korosho, chai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ushirika huu ulianza kwa hiari ya wakulima wa mazao hayo. Ushirika huu ulikuwa wa maana sana na ulifanya mengi ya kimaendeleo kwa wakulima wanachama. Wakulima kwa kupitia ushirika huo waliweza kuuza mazao yao bila kupunjwa. Ushirika ulikuwa unafanya kazi kwa kufuata kanuni za uendeshaji na ulikuwa unaendeshwa kwa faida. Kutokana na mapato yao wanaushirika waliwekeza katika shughuli za maendeleo kama vile majengo, shule, hospitali na kadhalika na wanachama wote walikuwa wanafaidika na huduma zitokanazo na vitu hivyo vyote.

Mheshimiwa Spika, faida kubwa iliyoletwa na Vyama vya Ushirika ni kusaidia watu kupata elimu. Vyama vya Ushirika vilikuwa vinatoa ruzuku kwa wanafunzi ili kujikimu na maisha wakati wakisoma. Hali hii ilichangia watu kutoka sehemu mbalimbali kuelimika sana na maisha yao yaliboreshwaa sana. Ushirika huu ulishamiri vizuri maeneo ya Kagera, Kilimanjaro, Ruvuma, Mbeya, Mwanza na kadhalika. Watu wengi wa sehemu hizi walipata fursa ya elimu kwa kusaidiwa na Vyama vya Ushirika na ndiyo zinazoongoza kuwa na wasomi wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, ushirika wa mazao ulikuwa na *centre* moja iliyomsaidia mkulima au mwanaushirika kuuza mazao yake na bila kupunjwa, ushirika huu ulionekana kama kweli ni ushirika wa wananchi ambaa ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sababu zake inazozijua ilivunja ushirika uliokuwa kwa faida ya wananchi wengi ambaa ulikuwa unaanzia chini kwenda juu, badala yake imeleta Taasisi ya Kiserikali ambayo haina malengo ambayo wanaushirika walikuwa wanajivekea. Ushirika ulioletwa na Serikali ni wa kiimla ulijengwa na mameneja ambaa walikuwa mawakala na kuvunja na kufilisi mali za ushirika. Kwani kila kitu kilichoengwa na kuendelezwa na ushirika sasa hakipo badala yake mali za wanaushirika zimehamishiwa mikononi mwa watu wachache ambaa waliitwa mameneja na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, leo, Serikali inajitahidi sana kuzungumzia uimarishaji wa ushirika ambaa yenye ilishiriki kuuvunja, lakini kwa sura nyingine kabisa. Ushirika wa leo siyo ule wa jana uliowasaidia wasomi wengi wakiwemo baadhi ya Wabunge kupata elimu. Ushirika wa sasa siyo wa mazao kama tuliuza. Ushirika huu ni wa kuiga kutoka nchi za nje hususan Sweden. Ushirika wa leo ni wa *SACCOS* na *SCCULT* ambaa unafaidisha vikundi vidogo vidogo vinavyopatikana zaidi mijini ambapo hali za watu ni bora kuliko za wale wa vijijini. Ushirika huu pia unawahu watumishi wa umma wenye kipato cha kueleweka wanaoanzisha, wana vikundi vya *savings and credit*.

Mheshimiwa Spika, ushirika huu unaengua kundi kubwa la wakulima ambaa wengi wanapatikana vijijini na hauna manufaa kwa watu hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirika na Masoko sasa ni wakati muafaka kurejea na kujenga ushirika wa mazao kuliko ushirika wa *SACCOS and SCCULT*,

*SAVING AND CREDIT.* Ukiangalia, katika hotuba ya Waziri mara nyingi amezungumzia kuimarika kwa ushirika wa *SACCOS* kuliko ushirika wa mazao ambao ulikuwa unasaidia wakulima walio wengi na mazao yao. Tungependa Wizara ya Ushirika na Masoko ijikite zaidi kuwaelimisha wananchi juu ya ushirika na faida zake. Ushirika wa mazao uanzie kwenye vijiji na siyo mijini tu. Wanaushirika wasilazimishwe kujiunga na kuuza mazao yao kwa vyama vikuu vya ushirika ambao ni wa kiimla zaidi kuliko hiari yao wenyewe. Tunaamini wanaushirika *at primary level* kama wataungana watatengeneza kanuni na taratibu zao za kununua na kuuza mazao yao. Tubadili mfumo wa ushirika ambapo wakulima wa mazao wataunda ushirika, watanunua mazao, watayasindika na kuyauza kwa bei nzuri zaidi. Tuachane na mtindo wa sasa wa wanaushirika kuuza mazao kwenye Chama Kikuu ambacho kimeelemewa na gharama kubwa za kiundeshaji (*over head costs*).

Mheshimiwa Spika, jukumu lingine la Wizara hii ni kutafuta masoko ya mazao yote ya wakulima. Hii ni pamoja na kuandaa soko la ndani la mazao na kuimarisha bei ya mazao. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa wakulima wanazalisha kwa gharama ndogo na kwa wingi na kuuza kwa bei nzuri. Kuwe na bei ya kuanzia ambayo wanunuzi wa mazao ya wakulima lazima wazingatie na kuheshimu wakati wa kununua mazao hayo na wasinunue chini ya hapo. Leo hii wakulima wanapunjwa mazao yao, wanalamika kupitia Wabunge wao lakini Serikali bado inaendelea kuwadanganya wakulima huku ikiwakumbatia wafanyabiashara hao. Kwa sasa imefikia hali ya wafanyabiashara kupuuza na kutoheshimu hata maagizo ya viongozi wa Serikali pindi itokeapo hali ya kuwapunja wakulima.

Mheshimiwa Spika, wanunuzi hao wa mazao ya wakulima hawaheshimu kabisa maagizo yatolewayo na Serikali, kumekuwepo na ukiukwaji wa taratibu za ununuzi wa mazao uliofanywa na Serikali. Wafanyabiashara hawa wamekuwa wakinunua mazao ya wakulima kwa bei ya chini sana ambayo haina thamani halisi ya mazao. Hali hii inasababisha wakulima kupunjwa haki zao na kukwamisha mikakati ya kupunguza umaskini. Wafanyabiashara wamekuwa wakijitajirisha kwa jasho la wakulima bila huruma.

Mheshimikwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa agizo hapa Bungeni kwamba wakulima wa pamba waliokuwa wamepunjwa warejeshewe haki zao, lakini hakuna kilichoteklezwa mpaka sasa. Ushahidi unaonyeshwa katika swali la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba la tarehe 14 Julai, 2005 la Ushirika na Masoko pamoja na majibu yaliyotolewa hapa Bungeni, kama hawakutii amri ya Waziri Mkuu hamwoni kuwa wafanyabiashara hawa wanaidharau Serikali?

Mheshimiwa Spika, pamoja na wafanyabiashara kuonyesha dharau na kutotii amri zitolewazo na viongozi wa juu, Serikali bado inaendelea kuwaruhusu wafanyabiashara hao kuendelea kununua mazao hayo kwa bei wanayotaka wenyewe. Kwa kufanya hivyo kambi ya upinzani inaona ni sawa na kuwasaidia wafanyabiashara hao kuendelea kuwanyanyasa na kunyima haki za wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Serikali imekuwa ikisingizia kuwa biashara ya mazao ni maelewano. Sisi kambi ya upinzani tunasema hivi tukiingia madarakani, wote wale ambao wanawadhulumu wakulima tutawachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kifungo, kwani kupunja wakulima na kukaidi amri ya Serikali kuwalipa fedha ya mapunjo ni wizi na wanastahili adhabu. Kwa sababu Serikali iliyopo, kwa kuitia Wizara hii, hamjawachukulia hatua zozote, tunaamini mko pamoja na wafanyabiashara hao kuwadhulumu wakulima nanyi mnastahili adhabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaasa kuwa maagizo ya Serikali lazima yatekelezwe na yaheshimiwe na siyo kubembelezana, vinginevyo hali hii ikiendelea Serikali itatawaliwa na kundi dogo la wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi kwa Serikali ni kuwazuia wafanyabiashara hao wa mazao wasinunue mazao ya wakulima na kuwanyang'anya leseni za kufanya biashara hiyo. Pia Bunge litunge sheria kali ili kuwabana wanunuzi wa mazao wasiolipa wakulima au kuwapunja na ichukuliwe kuwa ni kosa la jinai na wanastahili kushitakiwa na kuadhibiwa mbele ya vyombo vya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Sir George Kahama, kwa uamuza wake wa busara na wa kuigwa wa kuamua kutogombea tena Ubunge. Utumishi wa Mzee wetu huyo katika Taifa letu umeacha kumbukumbu pepu. Kila mahala alikotumika Mheshimiwa Kahama, ameacha alama ya utumishi wake. Sio siri kwamba mradi wa nyumba za maghorofa za CDA alioubuni na kuusimamia miaka hiyo ya nyuma, bado unakidhi matakwa ya mji bora na endelevu kuliko zilivyo nyumba zinazojengwa hivi sasa barabara ya kwenda Dar es Salaam zinazoonekana kama makambi ya wakimbizi. Tunakupongeza sana mzee wetu na mwenyezi Mungu akuzidishie afya ili Taifa liendelee kutumia uzoefu wako kiushauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, pamoja na Kamati nzima ya Uongozi wa Kambi kwa imani walijokuwa nayo kwangu, kunichagua kuwa mmojawapo wa Baraza lake la Mawaziri Vivuli. Nashukuru sana kwa hilo na natumai malengo na mategemeo aliyokuwa nayo kwangu mimi katika kuiwakilisha Kambi nimefanya kadri ya uwezo wangu na kama nimeteleza naomba nisamehewe. Natoa pongezi kwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani kwa kazi nzuri ya kuwa *watch dog* kwa Serikali. (*Makofi*)

Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Chama changu cha Wananchi (*CUF*) chini ya Mwenyekiti wetu Profesa Ibrahim Lipumba, Katibu Mkuu, Maalim Seif Sharif Hamad, pamoja na Baraza Kuu la Uongozi la *CUF* kwa kunipa msamaha mimi na Mheshimiwa Adelastela Mkilindi kutokana na matatizo yaliyokuwa yametokea, baada ya kuridhishwa na mwenendo wetu ndani na nje ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Wabunge wote wa Chama cha CUF kwa utetezi wao dhidi yetu. Nasema ahsanteni sana. Tunaahidi kuwa tutafanya kazi na matokeo yatakuwa wazi. Hatutapoteza matumaini yenu kwetu. (*Makofi*)

Mhehsimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa kazi aliyoifanya na ushirikiano alionipa pindi nilipohitaji ushauri wake, aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati kwa ushirikiano walionipa. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mnaifanya kuliongoza Bunge hili Tukufu, kadhalika nimshukuru Katibu wa Bunge na watendaji wote kwa kuweza kubeba majukumu yao vizuri na kuweza kutulea vizuri sisi Wabunge kwa kipindi chote ambacho tumekuwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha na namuunga mkono Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya awali asubuhi hii kuchangia kwenye hoja ya Mheshimiwa George Kahama, katika Bajeti yake ya Wizara ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umekuwa ukituendesha hapa ndani kwa ufanisi wa hali ya juu na kutoka kwako tumejifunza mengi ambayo binafsi nimetajirika kama Mbunge pia. Pili ningependa kwa dharti kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwanza kwa utumishi wake uliotukuka, kwa kweli kama ambavyo amemalizia kusema baadhi ya maneno alioyasema Msemaji wa Upinzani nakubali kabisa ingawa mengine sikubaliani nayo.

Lakini niseme tu kwa kifupi kwamba ni utumishi uliotukuka na unafaa na wa kuigwa na kwa kweli niseme tu huyu ni akiba ambayo naamini tutaendelea kuitumia hata katika kustaafu kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Naibu wake kijana wa Kigogo, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya alipokuja kwa sisi baba zake huko Tabora alitusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii Dr. Komba, kwa jinsi ambavyo ametoa uongozi na pamoja na wataalam wake wameendelea kutusaidia kwa karibu kabisa na tumaani kwamba tutaendelea kupata mafanikio chini ya uongozi wao.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze kipekee Mheshimiwa Waziri, kwa kutusaidia sisi watu wa Tabora pale ambapo chama chetu cha *WETCU* ambayo ni *union* ya vyama vyetu vya msingi vya wakulima wa tumbaku kilipokuwa kimeingia kwenye matatizo makubwa ya madeni ambayo kilikuwa kwenye hatari ya kafilisika kabisa.

Mheshimiwa Waziri alitusaidia kwa kweli kwa kiwango ambacho ameokoa kabisa hiyo *WETCU* na mimi namshukuru kwa dhati kabisa na wakulima wote wa Mkoa wa Tabora wakulima wa tumbaku wanakuletea salaam za kukutakia mafanikio mema kabisa katika maisha yako na kwa jinsi ambavyo umewasaidia wanakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue na mimi nafasi, sina uhakika kama nitaongea tena katika Bunge hili la Bajeti. Napenda nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru familia yangu, mke wangu mpenzi Enighenja, kwa msaada na uvumilivu mkubwa ambao amenipatia pale ambapo nimekuwa nikizunguka huku na kule katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge. (*Makofi*)

Napenda pia niwashukuru na niwapongeze watoto wangu Debra na James *Junior*, kwa uvumilivu wao mkubwa pamoja na kuwa saa nyingine hawakuelewa kwa nini niwe nazunguka kwa kiwango hicho. Lakini hata hivyo wameni-*encourage* sana na nawashukuru sana. (*Makofi*)

Napenda niwashukuru wazazi wangu na wananchi wote wa Jimbo la Tabora Kaskazini kwa jinsi ambavyo wamenipatia ushirikiano na kunifanya niwe Mbunge ambaye naamini nimeiva sasa kuchukua majukumu makubwa zaidi. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Uyui na Ofisi nzima ya Wilaya na kwenye Kata zote 12 za Tabora Kaskazini, napenda niwashukuru sana kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana kwa karibu na kwa uongozi ambao umeniwezesha kufanya kazi vizuri sana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2000-2005.

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, nimshukuru sana Msaidizi wangu Bwana Said Shaban Ntahondi ambaye kwa kweli amefanya kazi kubwa sana iliyonisababishia niwe na ufanisi mkubwa hata pale ambapo sikuwa jimboni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nzungumzie sasa mazao makubwa mawili ambayo yapo katika jimbo langu la Tabora Kaskazini. Mazao yenyewe ni pamba na tumbaku. Hili la pamba kwanza napenda kwa mara nyingine tena tuwashukuru sana Wizara kupitia Bodi kwa kutusaidia sisi Wilaya ya Uyui kuanza kulima pamba, huu ni msimu wa pili, tunalima pamba na pamba yenyewe ni nzuri aina ya *UK 90*.

Mheshimiwa Spika, walituambia kwamba mbegu hii inatoa pamba ya ubora mkubwa kwa hiyo bei nayo inatakiwa kuwa kubwa. Kwa kweli hilo halijaonekana sana katika kipato cha wakulima wetu. Hilo napenda kwa kweli nililet kama swalii na wataalam wapo hapa. Nafikiri watatoa maelezo ya kukidhi. Kwa sababu wakulima wetu wamekaa wakisubiri wameona wamelipwa na pengine wamelipwa chini kuliko ambavyo walitarajia au hiyo nyongeza ambayo ilitarajiwa wala haikuonekana kabisa *against* zile aina zingine za pamba.

Hili tatizo ni nini hasa? Lakini katika msimu wa kwanza wa mwaka jana ambapo ilikuwa ndiyo mara yetu ya kwanza kulima pamba, tulifanya kazi nzuri. Lakini tukapata

matatizo ya kuuza pamba. Hatimaye kwa juhudini kuanzia Bodi yenye kazi ya Pamba na hatimaye uongozi wetu wa Wilaya tulifanikiwa kupata mnunuzi anayeiwa *KACU*. Lakini kumbe tumeingia kwenye matatizo makubwa kwa kumleta huyu *KACU*. Sasa huyu bwana ametuingiza kwenye madeni makubwa, wakulima wetu wanaendelea kudai kiasi cha milioni 42. Hizo ni hela nyingi sana kwa wakulima wa Jimbo la Tabora Kaskazini hasa kwa sababu ndiyo mara ya kwanza walikuwa wameingia kwenye kilimo hiki cha pamba. Wangependa kwa kweli wajengewe imani kwamba wanajaliwa kama ambavyo walisaidiwa kupata haya masoko au tuseme kupata hawa wanunuzi. Basi hebu waendelee kupewa msaada. Sasa walipwe peza zao. *KACU* kwa kweli wana matatizo makubwa na nasikia sijui wanafilisika, sina uhakika. Lakini najua wana matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, uhakika kwamba *KACU* watalipa sidhani kama upo. Lakini nataka niseme kwa sababu ninaamini Serikali ina mpango wa kusaidia wakulima wanaoingia kwenye matatizo ya namna hii na kwa kuwa *KACU* ni Chama cha Ushirika na siyo mtu binafsi, naomba basi Serikali ichukue mzigo huu, pesa zenyewe ni milioni 42 ndiyo kwa Serikali naweza kusema si kiasi kikubwa sana. Lakini kwa wakulima wangu, ni pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri na watu wake hebu watusaidie. Nafahamu kuna mipango ya aina mbalimbali wanaweza wakatusaidia katika kuhakikisha kwamba wanalipwa, basi walipwe. Maana yake sasa wameanza hata kusema kwamba wanaweza hata wasipige kura sawa sawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, basi tunaomba, lakini kimsingi kwa kweli nataka niseme si kwamba kwa sababu tunaogopa watapiga kura vinginevyo, hapana, na sidhani kwamba watafanya hivyo, kwa sababu wanafahamu Chama cha Mapinduzi siku zote kipo nao. Napenda kwa kweli niombe kwa dhati kabisa hebu hili litatuliwe na lifike mwisho na ikiwezekana mwezi huu au mwezi unaokuja tumalize, walau kwa taarifa ambazo zinaaminika halafu baadaye walipwe kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie kidogo kuhusu mnunuzi aliyepo au wanunuzi waliopo msimu huu, wanatoa pesa. Lakini ndiyo niseme kwanza nafikiri kuna wasiwasi kwamba pesa zinazotolewa hazilingani sana na pesa ambazo zinatarajiwa kwa zao na ubora ambao tunaupata katika hii aina ya mbegu. Lakini bado niseme kwamba sasa hivi na wakulima wenye wameanza kuwa na wasiwasi na hili wamenituma. Wanasema hivi wameanza kuona kwamba hii pamba inapochukuliwa inapelekwa inachanganywa na pamba aina nyingine kwenye zile *ginneries* ambazo wanaweza kufanya *ginning*.

Sasa wana wasiwasi kwamba mbegu itakayorejeshwa tena inaweza isiwe ni ile ambayo inatakiwa kulimwa kwenye Wilaya yetu. Sasa hili nafikiri tuliwahi kulizungumza mwaka jana lakini na wao wakulima sasa wameliona. Sasa naomba hebu tusaidiane katika hili. Sijui Mheshimiwa Waziri atasema nini kuhusu uhakika ambao unatakiwa kupewa wakulima wetu kwamba mbegu ni ile ile aina ile ile ndiyo itakayorejea na si mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, napenda niliache hilo la pamba hapo lakini niendelee na lingine. Katika pongezi zangu kwa kweli nilistahili kumtaja kipekee pia Mrajisi wa Vyama Daktari Ndugu, kwa kazi nzuri anayoifanya. Lakini nataka nikumbushe tena sisi Tabora tumekuwa na tatizo kwa kweli la mtu wa kusajili vyama. Hili tatizo mbona linaendelea bila mwisho na nilidhani ni tatizo dogo sana. Kiutaratibu wa kiutendaji tuliambiwa kwamba nyaraka zinaweza zikatayarishwa basi kama sisi hatuna mtu ambaye anastahili kufanya huo usajili walau zipelekwe katika Mkoa wa jirani, labda Shinyanga, ambako nafikiri Afisa ambaye ana ruhusa ya kufanya usajili yupo.

Lakini mimi nimeshindwa kuelewa kitu gani kinachoendelea. Tuna vyama vingi ambavyo vina-*qualify* kupata usajili. Lakini haya mambo yanazunguka zunguka tu. Hebu naomba tupewe msaada unaoeleweka sasa katika hili. Kwa sababu watu wameamua kujiunga kwenye vyama vya msingi vya ushirika wanaamini katika ushirika lakini sasa wanazungushwa na watu ambao walitakiwa kwa kweli kuwapatia msaada mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nihadie kwenye zao la tumbaku. Kilimo cha tumbaku kinachofanyika Tabora kimsingi ni kilimo cha makubaliano ambapo mnunuzi anakuja anafanya makubaliano na wakulima kwamba atakopesha, atawaleta hiki na hiki na wao watampatia zao lile na atakata na marejeo atawapatia kama pesa yao. Sasa katika kukubaliana wanakubaliana na vitu vingi sana.

Mheshimiwa Spika, hapa nina karatasi ambayo inaonyesha makubaliano hayo yaliyofikiwa kwenye Halmashauri ya Tumbaku ambako bei zimeainishwa kabisa. Lakini nasikitika kusema kwamba hakuna maelezo ya kutosha kabisa kutoka kwenye hii karatasi nyingine ya ziada ambayo ni ya Kampuni ya Tumbaku (*TLTC*) na hii karatasi imechapwa kutoka kwenye *printer* yao kwenye *computer* tarehe 25 Juni, 2005, ikionyesha bei zingine tofauti kidogo na zile ambazo zimekubaliwa.

Ningependa baadaye niwapatie nakala ya hii ili watusaidie Wizara kuelewa ni kitu gani hasa kimetokea. Lakini tu niseme kwa mfano, *Cotton twine* ambayo ilikuwa imekubalika kwamba *unit price* ingekuwa shilingi 3,000 sasa hawa katika hili chapisho la tarehe 25 Juni, 2005 *unit price* ni shilingi 4,000.

Mfano mwengine, *New Hessian Cloth* hawa *TLTC* sasa wanasema ni shilingi 670 *per unit price* wakati kwenye makubaliano yaliyosainiwa na wao wenyewe *TLTC* wakiwa wameweka sahihi, napenda hili kwa kweli nilisemee kama uthibitisho kwamba hapa naona kuna *Managing Director Mr. Hugh Thacker* wa *TLTC* ambaye ameweka sahihi yake. Sasa kwenye hii *New Hessian Cloth* wanataka shilingi 670 kwa *unit price* wakati ilikuwa shilingi 560. Hivyo hivyo kwenye *Sisal twine* ilikuwa imekubalika shilingi 300 kwa *unit price*, sasa wao wanataka shilingi 429. Hii nimeitumia kama mfano.

Lakini nafikiri hapa kuna kitu siyo cha kawaida, ningependa wakati mwengine pamoa na ukweli huu ambao ningependa kwa kweli nikupatie Mheshimiwa Waziri baadaye ningependa kama ambavyo na Sheria yenyewe inaagiza kwamba Bodi iwe inafanya kila mara iwe inapitia pitia haya mambo ili kuelewa kwamba ile *regulatory*

*power* ambayo wanayo inafanya kazi vizuri na hakuna mtu anayemwonea mwingine katika hili soko. Kwa kweli hili naomba lifanyiwe marekebisho ni pesa nyingi sana ambazo wanaweza kupoteza wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumzie tatizo hususan chama cha msingi cha tumbaku kinaitwa Msimba, kwenye Kata ya Usagali kwenye jimbo langu la Tabora Kaskazini. Hawa waliletewa barua na Bodi kwamba wamevuka malengo ya *projections* ambazo walikuwa wamezitoa, ambapo hawa wanasema malengo yalikuwa ni kuzalisha kilo 117,000.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenye nimeona mkataba ambao ulikuwa umesainiwa ni kwamba walikuwa na malengo ya kuzalisha kilo 226,000. Sasa utaangalia kwamba unapokuwa umepeleka sokoni kilo 117,000 bado upo mbali sana chini ya lengo lako, *you are under the target by more than 100,000 kg's.*

Sasa hawa wamepelekewa barua kwamba kwa kuwa wamezidisha viwango hivyo ambavyo vilitarajiwa basi masoko yanositishwa kwao. Sasa kwanza nataka nii-*question* busara ya kufanya kitendo hiki. Ile ni tumbaku ambayo imefanyiwa kazi na wakulima. *Decisions* za namna hii kwa kweli zinakatisha tamaa. Hata kama mnataka kukwepesha utoroshaji, kitu ambacho na mimi nakubaliana kabisa kwamba utoroshaji wa tumbaku ni kitendo cha aibu. Wakulima lazima tukionee aibu, tujifunze kuwa waaminifu, tuuzie kwenye Ushirika ambako tulikopea, nakubaliana kabisa.

Mheshimiwa Spika, *measures* lazima zichukuliwe lakini siyo za namna hii. Kwa nini basi msiruhusu tu tumbaku ikauzwa halafu ile pesa ambayo iko kwenye swali kubwa ikawa *retained*. Mimi sioni kitu gani kilikuwa kikubwa, hapa kuna maelezo nitampatia Mheshimiwa Waziri baadhi ya nakala za barua ambazo ninazo hapa. Inashangaza kabisa kwamba kitu cha namna hii kinaweza kutokea. Sasa katika utetezi wao watu wa Bodi wanajificha ficha tu kwenye mambo ambayo nadhani lazima waone aibu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba niseme kwamba naunga hoja mkono na watusaidie. Ahsante sana. (*Makofji*)

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kweli niseme tu kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana. Ukiisoma na kama itafuatiwa, itasimamiwa na kutekelezeka ni hotuba nzuri inaleta matumaini makubwa kwa wakulima wa ngazi mbalimbali na katika vita ya kuondoa umaskini nasema, kama Wizara hii ingesimamia sera zake na sheria zake na ingesimamia hotuba hizi kwa kweli mkulima mdogo na mkubwa wangekuwa na maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi katika awamu hii ya tatu kwa kazi kubwa sana ambazo kwa kweli mwenye macho ataona, asiyé na macho utamaliza viberiti, maana yake utamulika haoni. Mwenye masikio hata kama ni mikutano na hotuba za Mawaziri na kila mahali utasikia. Sasa kama husikii hata tungeimba nyimbo nzuri hutaweza kuzifurahia.

Sasa wapo ambao wanasema Serikali hii haijafanya lolote. Lakini sisi tuendelee kuwaambia tunafanya, tusibishane nao. Maana yake utapoteza muda kubishana na mtu ambaye haelewi, labda kutoka nyumbani ameambiwa wewe kakatae tu kila kitu. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa hata angekuja Yesu akamwambia mimi muumba wako, nataka nikupeleke mbinguni, hapana. Sasa atabaki hapa ataungua na moto. Kwa hiyo, mimi nasema tutaendelea kuwahubiria wenzetu wasioona na wasiosikia maendeleo yanayofanyika na tunasubiri hata Ilani zao za uchaguzi sijui zitasema nini. Maana yake wana kazi, kero nyingi ambazo kwa kweli zilikuwa zinawasumbua wananchi zimejibiwa na Serikali na zinaendelea kujibiwa kwa ufasaha sana. Sasa tunasubiri watakuja na Ilani ain na misemo ain. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, walikuwa wanasema shule hazifundishiki, sasa tuna walimu. Tuna majengo mazuri na sekondari zipo. Walikuwa wanasema barabara hazipo, sasa zinatandikwa mpaka kila mahali, maji na kila sekta. Mimi nasema nitazungumzia Wizara hii katika maeneo makubwa mawili. Kwanza ushirika.

Mheshimiwa Spika, ziko sera nzuri kabisa ambazo Mheshimiwa Waziri amezzungumza humu za Ushirika. Lakini ushirika unaozungumzwa humu ni wa maneno siyo matendo, siyo hali halisi iliyoko kule kijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unaposema unaimarisha ushirika, unaongeza mitaji, unaongeza wanachama, lakini wako wapi. Ushirika wenyewe uko wapi? Nitazungumzia sasa hivi msimu wa pamba umefunguliwa tangu tarehe 8 Juni. Vyama hivi vikuu vya ushirika vinavyonunua mazao haya havijapata hela. Havijaanza kununua. Juzi nilisikia *SHIRECU* imepata bilioni 2.5. Lakini ziko wapi, watanunua lini?

Sasa na majibu mengine ya Mawaziri wetu hapa yanatushangaza. Jana liliulizwa swalii zuri sana hapa. Mkulima yule atajuaje bei yake ya kuuza. Mheshimiwa Waziri amejibu kama ametoka Ulaya, kwamba kuna *internet* tutaangalia bei. Huyu mkulima tunazungumzia Wilaya hazijapata umeme, Wilaya hazijapata umeme. Sasa hii tovuti na *internet*, mkulima, tena Mheshimiwa wa Chilonwa, Chilonwa kweli kuna *internet* huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbona karanga naona Wagogo wanazungusha hapa, hawajui soko la *internet* huko. Tunasema haya mambo tusiyapeleke, tusijivue sisi, tukaawaacha wakulima wetu. Tunawajua kabisa wakulima wetu walivyo. Wako wapi, wana upeo gain na wana mtazamo gani. Ni lazima kwa kweli Serikali isimamie hasa mazao makubwa, yako mazao lazima tu Serikali isimamie wakulima wetu hawajafikia mambo ya kwenda kwenye *internet*, hawajajua kutafuta soko la dunia sijui likoje na nini. Lazima Serikali isimamie.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba sasa hivi linanunuliwa kwa bei ya ajabu sana na bila kuimarisha ushirika hawa wakulima watakata tamaa. Hawawezi wakalima tena. Wanunuzi binafsi hawa wanazungumzia kwenye kupanga bei ya kwenda kununua kwa wakulima. Leo tukanunue shilingi 180 kesho tukanunue shilingi 200 na kwa uongo tu

kwamba bei ya soko ya dunia imeteremka, imeteremka wapi na kwa sababu mkulima huyu hajui hata gharama ya kuzalisha kilo moja ya pamba. Tuna Maafisa Kilimo, tuna Maafisa Ushirika, kwenye Wilaya zetu, lakini hawafanyi hata kazi ya kumjulisha mkulima wewe hapa tunakadiria wastani wa kuzalisha kilo moja ya pamba ni shilingi kadhaa kwa kilo.

Kwa hiyo, ukiuza kwa bei hii kwa mnunuzi, utakuwa umepata faida au hasara. Tuna watu wa Bodi ya Pamba kila Wilaya. Lakini wao ni kukamata tu watu, huyu amechanganya pamba na mahindi, huyu sijui mbegu zisizo na manyoya, sijui kuna vinyozi wa mbegu wapi wamewekwa huko, ni mambo ya ajabu sana. Hawafundishi, hawaelekezi, hawasimamii.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa kweli kwa zao hili la pamba katika misimu miwili hii, nimepata shida sana, tangu Januari mpaka Desemba, unazungumzia pamba tu, tangu wanalima, wanaanza kupanda, huyu anakamatwa tena, mbegu zisizo na manyoya, wewe mbegu zenyne manyoya, mbegu za namna gani, tatizo. Kwenda kwenye kupalilia, umechanganya mahindi na pamba, tatizo. Mpaka unauzu, mpaka unakata miti, mpaka unakwenda kuuza pamba kule yaani ni tatizo.

Sasa Wizara yetu iko wapi, inasema nini dawa ni ushirika, dawa ni ushirika lakini ushirika upi, ushirika tunaouhitaji ni ushirika wa vyama vyaa msingi unapozungumzia sijui *NYANZA*, *SHIRECU* hizo ni *appex ambazo* hazina wanachama huku. Kama tungekuwa na vyama vyaa msingi huku *SHIRECU* isingezungumza hata wanunuzi binafsi wangefutika hapa. Lakini kila siku tunazungumza tuhame *SHIRECU*, *NYANZA* ndio unachozungumzia Waziri, vyama vyaa msingi una mkakati gani? Sisi kama wanakijiji katika kijiji A, tuna chama chetu cha msingi watu tuwe wanachama kuwe na *seed money* kutoka Serikalini, kwamba mtu anapokwenda kuuza pamba yake katika chama A ni mwanachama anaandikwa kwanza tutaondokana na zoezi la kuibwa hata kwenye mizani zao hizi zimeshapunja tayari karibu kilo kumi. Sasa akipima pale apewe angalau *token money* angalau ya kuondoka nayo, ndio ningelewa tunashida ya kuimarisha ushirika.

Mheshimiwa Spika, sasa *process* zingine zingeendalea kusaidiwa na Wizara mpaka wana-ginne pamba mpaka wanakwenda kuuza. Waziri jana anasema bei ya kuuzia soko la dunia senti 44, hapana ni senti 48 ya dola kwa ratili jana soko la dunia hilo. Sasa wewe sijui nani anakushauri na mimi najua tatizo sio la Waziri, washauri wake ni wabaya sana huko kwenye Wizara huko kuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilizungumza kwenye bajeti hapa kwamba wako watumishi wa Serikali wamepelekwa pale *SHIRECU* kusimamia *SHIRECU* meneja mkuu sijui na bwana fedha wale ni wachuna ngozi, imechunwa *SHIRECU* imebakia *skeleton*. Wamekwenda pale *SHIRECU* ilikuwa inadaiwa katika madeni yote milioni 300 na kitu, leo kuna deni la bilioni 1.5 na mali zote zinazwa. Sasa tutafanya nini ilikuwa na magorofa, ilikuwa na magodauni, ilikuwa na magari, ilikuwa na ma-ginnery yote hoi na yuko meneja pale tangu mwaka jana Mheshimiwa Waziri alisema hawa wanaondoka mara moja lakini wako mpaka sasa, washirika wamechagua meneja, hakabidhiwi huyu mtu wenu mliyepeleka pale mnajua ninyi muondoeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, anafanya nini pale, hataki kukabidhi kwa nini? Mpaka ale mifupa ya *SHIRECU* ndio ashibe, aondoke au tuwajuaje ninyi? Kila kitu kimeuzwa na deni linaongezeka la *SHIRECU* na katika maazimio ya mukutano mkuu wa tarehe 30 Aprili, 2005 uliazimia kuuza baadhi ya mali na kulipa madeni ya wafanyakazi. Wafanyakazi hawajalipwa mishahara ya miezi 22, hivi unategemea mfanyakazi afanye nini lakini yuko Waziri tu na Naibu wake wanatembea na magari aina ya mashangingi wala hawana shida kabisa na wataalam chungu mzima kule wengine sijui ushirika wa wapi mnajifunza jamani ninyi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa *SHIRECU* wanadai bilioni moja na wala hawana shida ya kuendelea kukaa *SHIRECU*, bilioni 1.8 kwa hiyo, *godown* la *SHIRECU* la Kurasini lilikuwa linatathminiwa kuuzwa bilioni 2, lakini yametokea mambo sijui mambo gani na zile hela zingeelekezwa kulipa wafanyakazi kwanza hawa, kuna mapunjo ya mshahara, kuna mafao kuna nini hawajalipwa hawawezi kufanya kazi hawa. Sasa kama hatuwezi kuwajali wafanyakazi, kweli unaweza kuendesha ushirika, unasema unajenga ushirika huo. Walipeni waondoke, huyu mnunuzi aliyenunua amelipa milioni 450 katika bilioni 1.8 sasa milioni 450 analeta *cheque* tena mpaka izunguke benki ndio iwe *cleared* ndio zionekane hela, tunafanya nini hata mikataba ya uuzaji wa mali za *SHIRECU* haufuatwi.

Kwa kweli mimi nataka kusema kwa kweli sasa tunaelekea kubaya, mnatupa maswali magumu ya kujibu kwenye kampeni, unaenda kwenye kampeni lakini kuna maswali magumu ya kujibu na ninyi mtajibu kwani nyie hamgombei? Namna gani ninyi? Pole sana maana yake nini ninyi hamwendi kujibu huko, kama mnatuacha tupambane wenyewe sawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa nasema iko kazi ya kufanya Mheshimiwa Waziri, Serikali lazima isimamie soko la pamba, bei ya pamba kwanza tujue gharama ya kuzalisha kilo moja ya pamba mbegu, ili hata kama nauza najua napata hasara au faida na mimi nawatangazia wakulima wasiuze haraka pamba. Huu msimu wa kutangaza sijui utaanza mwezi wa sita wapi nchi hizi za Malawi, Zambia, Zimbabwe hawatangazi msimu unakuwa ni *continuous* mwaka mzima, pamba inaiva mwezi wa nne inaenda inauzwa inajiniwa sasa unasubiri mpaka wa sita, wa saba, nchi za Brazil na zenyewe karibu zinauza pamba, na wale ni wakulima wakubwa wale kwa hiyo wata-*float* kwenye soko la dunia bei inateremka wakulima wetu wanapata soko la chini, lakini tungefanya tu ni miezi kumi na mibili, pamba mwenye kuivisha mwezi wa nne, mwezi wa tano, mwezi wa ngapi akauze na hawa ma-*ginneries* sawa wangepanga wangeingia mikataba ya kuza marobota yao mapema, sasa sisi tutasema sijui mpaka tukague nini mpaka tutembelee mashamba, mpaka pamba inakomaa mkulima hawezi kuvuna pamba isiyokomaa. Sasa ninyi mnampangia aelewii, ninyi hamlimi hata pamba lakini mnakuwa wajanja kuwaingilia wakulima kwa nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa wa Masoko, hao wanunuzi kila siku tunasema hapa wanakaa wanapanga meza moja, lakini Wizara hata tukiuliza maswali hapa wakionekana tutawashughulikia, waonekane wapi hapa Bungeni au wapi hawa watu

wanapanga wanapunja wakulima tunauliza maswali hapa mnasema wakionekana waonekane wapi ninyi mko wapi sasa?

Mheshimiwa Spika, sasa maombi mawili, kwanza hapo *SHIRECU*, mimi nilikuwa nataka kuazimia tuunde Kamati ikaangalie *SHIRECU* ilipofikia sasa, tangu hii timu ya Serikali ilivyokwenda imekuta kitu gani na sasa hali ya *SHIRECU* ikoje, *pathetic*. Sasa nina maombi haya kwamba sasa Serikali iende *SHIRECU*, kwanza huyo meneja wa Serikali aondoke kesho, sasa anaanza na msimu mwингine wa nini watu wametajirika tu kununua majumba, magari na nini mali ya *SHIRECU*, wafanyakazi hawalipwi. Ombi la pili wafanyakazi washughulikiwe, walipwe hela yao hata kama ni kutoka kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri kabisa Wizara ipangue mpangilio wa bajeti ikalipe wafanyakazi wa *SHIRECU*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine bei ya pamba isimamiwe na Serikali, hatuwezi tukaondoa Serikali katika kusimamia bei ya pamba, lazima isimame. Lingine vyama vya msingi viimarishwe, itoke hata bajeti mimi nasema Mheshimiwa Rais anayekuja asimamie Wizara hii kwa makini sana, ashughulikie atoe hela ya kutosha tukaimarishe ushirika kule.

Sasa la mwisho nasema Wizara hii iweze kufuatilia mwendo wa masoko mbalimbali kama Serikali iungane pamoja, kwa sababu hii pamba kuiza kama pamba tu haiwezekani, viwanda iingie pale ifanye viwanda vidogo vidogo vya kuongeza ubora, sasa tunazungumza kwenye vitabu tu, lakini kila siku, hivi sasa tunasema eti ni *value added* ya *product* hii unafikiri ukizungumza kwenye bajeti kwenye kitabu kizuri mmekipamba na picha safi kabisa unafikiri ndio unatengeneza nyuzi, chukua hatua sasa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba zinatufurahisha tu tunaondoka hapa tunacheke kumbe hamna kitu kule, watu wetu wanazidi kupata matatizo makubwa kabisa Mheshimiwa Waziri sitaki niseme sana lakini naomba niwaombee wenzangu wote wanaokwenda kugombea mkashinde na hata wapinzani mje wachache hivi hivi, kwa sababu mbu wachache ni wazuri kwa dereva wa safari ndefu ili asisinzie, *a few mosquito's are very good for along safari driver*, lakini *too many mosquitos* watampa malaria, ataugua, atashindwa, ataangusha gari na ninyi muendelee kuja wachache hivi hivi ili msitupe shida tuendelee kuitisha bajeti zetu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema naunga mkono hoja hii, ni nzuri lakini inahitaji usimamizi na utekelezaji, asante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanne watakaofuatia baada ya hawa wa sasa ni Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Profesa Daimon M. Mwaga na Mheshimiwa Mwanne I. Mcemba.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze sana na nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa uamuzi wake wa kuunda Wizara ya Ushirika na Masoko. Uamuzi huu una lengo la kuimarisha nguvu ya wananchi wetu wawe na uwezo zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzo, hawakuwa na chombo cha kuwasemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nizungumzie hali ya ushirika nchini kwa mujibu wa maelezo yaliyokuwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hali ya ushirika nchini ni mbaya ukilinganisha na hotuba ilivyokuwa inaeleza na hali ya ushirika nchini ni mbaya kwa sababu ushirika nchini hauna usimamizi unaotakiwa. Kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa 51 anaeleza ni jinsi gani Serikali imeshughulika katika hali ya uimarishaji ukaguzi wa mahesabu ya ushirika. Lakini vyama 5,730 ambavyo viko nchini ni vyama 3,040 tu ambavyo tayari vimekaguliwa. Kwa hiyo, kuna tofauti ya vyama 2,330 viko wazi, havijakaguliwa na wakati huo unatoa taarifa kwamba vyama vya ushirika na ukaguzi umeimarishwa na hili ndio chimbuko kubwa ambalo linachangia vyama vyetu vya ushirika vishindwe kufanya vizuri. Vyama vingi nchini vimekuwa vikiijidesha vyenyewe bila hata kuhusisha wenye mali kwa maana ya wanachama, na hali hii inachangiwa kwa sababu ya ukaguzi hafifu uliopo.

Mheshimiwa Spika, mimi natoa wito kwa Wizara hii ya Ushirika na Masoko ijaribu kuimarisha vyama vyetu vya ushirika na hasa vya msingi kwa kuwaajiri maafisa ushirika amba watadhibiti mwenendo wa vyama vya ushirika. Huko nyuma tulikuwa na wakaguzi amba walikuwa wanakidhi haja, walikuwa wanahakikisha kila robo mwaka wanapokea taarifa ya maendeleo ya chama cha ushirika. Lakini leo unaposema umeimarisha ushirika huku kuna *gap* la vyama 2,330 havijakaguliwa, ina maana hakuna kitu ambacho kwa kweli unaweza ukakisema kwamba ufanisi umepatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie vile vile vyama vyetu vikuu vya ushirika, vyama vya ushirika kwa kweli ni kimbilio la wanyonge. Lakini badala yake vimegeuka vyama hivi hata wakulima wetu wanaviona kama vitanzi vyao, vyama hivi vimekuwa vikinunua mazao ya wakulima lakini vinashindwa kuwalipa. Mimi nina mfano hai katika jimbo langu la Bukombe, wananchi wa Bukombe wanakidai chama cha ushirika cha *CACU* zaidi ya milioni 120 kwenye msimu wa mwaka 2004/2005. Hali hii imetusumbua sana viongozi wa Bukombe. *DC* wa Bukombe amehakikisha kwamba wanunuzi hawa anawaita mara kwa mara, anawaagiza wawalipe wakulima, lakini bahati mbaya sana utekelezaji mpaka leo wakulima hawa hawajalipwa. Sasa tunaomba Wizara kama ndio msimamizi mkuu wa ushirika na kwamba ndio chombo peke ambacho kimeundwa kwa ajili ya kuhakikisha wakulima wanatendewa haki basi wahakikishe kwamba wakulima hawa wanalipwa haki yao na chama cha ushirika cha *CACU*.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nizungumzie malalamiko ambayo yanatolewa na wananchi wa kata moja ya Iyogelo. Bodi ya pamba ni chombo cha Serikali, na bodi ya pamba kwa nia njema kabisa ina utaratibu wa kutenga maeneo ya kulima pamba mbegu kwa ajili ya mbegu na kata ya Iyogelo ni moja ya kata ambazo zimebahatika kutengewa maeneo ya kulima pamba mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa pamba zaidi. Lakini bahati mbaya sana zoezi hili limewaathiri sana wananchi na

wakulima wa kata ya Iyogelo kwa sababu hawatendewi haki na wanunuzi ambao wameteuliwa na bodi ya pamba. Bodi ya pamba mara baada ya kutenga eneo ilibidi vile vile iteue wanunuzi watakao nunua pamba hii kwa ajili ya mbegu. Lakini wanunuzi hawa wamekuwa wakiritimba wakubwa, wanawapunja sana wakulima hawawapi bei inayotakiwa, na wanunuzi wengine hawaruhusiwi kwenda kununua pamba hiyo kwa sababu ni *special* kwa ajili ya mbegu.

Sasa ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba inawatendea haki wakulima wa kata ya Iyogelo ili iwape uhuru wa kuuza pamba yao kwa wanunuzi wengine ili nao waweze kunufaika na bei kama wanavyopata wakulima wengine. Vinginevyo itakuwa kama ni adhabu kwao kuteuliwa kama eneo la kuzalisha mbegu za kupanda lakini bei wanayopewa kwa kweli hailingani na wakulima wengine wanayoipata.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nitumie nafasi hii ya pekee kabisa kuzungumzia suala la watumishi wa *union* ya SHIRECU ninaimani kabisa Mheshimiwa Waziri malalamiko haya anayo, tena ni ya muda mrefu, inasikitisha unaposema kwamba unaimarisha ushirika na huku watendaji wanosimamia uboreshaji wa ushirika hawalipwi chochote. Watumishi hawa wanazaidi ya miaka sita sasa hawajalipwa haki zao za msingi kabisa ikiwa pamoja mishahara, malupulupu na haki zingine.

Kama alivyosema Mheshimiwa Danhi Makanga, watumishi hawa wanaidai SHIRECU bilioni 1,915 sasa mimi ningependa tu kuitia bajeti hii Mheshimiwa Waziri atoe tamko ni jinsi gani anashughulikia malalamiko ya wafanyakazi wa SHIRECU kuhusu haki zao. Kwa sababu hata mkutano mkuu wa *union* ulikaa na kukubaliana kwamba wafanyakazi hawa walipwe haki zao pamoja na kupunguzwa kwa sababu *union* ya SHIRECU inajientesha kwa hasara, ina maelfu ya watumishi ambao wapo tu lakini hawafanyi kazi, hawazalishi chochote Serikali ipo inasaidia vipi kuhalikisha kwamba *union* ya SHIRECU inakuwa hai kwa kupunguza watumishi. Kwa sababu bila kupunguza watumishi *union* ya SHIRECU itaendelea kuwa mufilisi.

Kwa hiyo, naomba Serikali itoe tamko hapa kwamba inashughulikia vipi tatizo la wafanyakazi wa SHIRECU kuhusu haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa nia njema kabisa Serikali iliamua kubadilisha uongozi wa SHIRECU, uongozi wa SHIRECU uliondolewa ukachaguliwa uongozi mwingine halali, uongozi ambao uko mpaka leo. Lakini vile vile yawezekana ilikuwa ni nia njema Serikali vile vile ikapeleka menejimenti yake, kule kuna *General Manager* ambaye ameteuliwa na Serikali, sio wa kuajiriwa na wana ushirika, na sera ya ushirika inasema ushirika unajiamulia mambo yake wenyewe, ikiwa ni pamoja na kuajiri watumishi. Lakini kwa sababu ya nia nzuri ya Serikali pengine ni kwenda kuisaidia SHIRECU.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanaushirika wa Shinyanga nasema menejimenti hii haijasaidia lolote katika *union* ya SHIRECU, na badala yake SHIRECU sasa ni mufilisi, ninaomba menejimenti hii iondolewe kwa sababu haiwajibiki kwenye Halmashauri halali ambayo imechaguliwa na wanaushirika wa Shinyanga. Halmashauri hii haina kauli kwa menejimenti ile kwa sababu ni menejimenti ambayo imepelekwa na Serikali. Naomba Serikali ii toe menejimenti hii ili kuipa haki sasa Halmashauri ambayo

ipo kihalali kutafuta menejimenti mpya ambayo itawajibika kwenye Halmashauri hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, udhaifu upo mkubwa tu ambao kwa kweli unasababu za msingi za kudai menejimenti hii iondolewe. Mpaka sasa wameshindwa hata kukusanya mapato ya *union* yanayotokana na ukodishaji wa viwanda, vinu vya pamba vya *SHIRECU* vinakodishwa, lakini *union* hii inakosa hata hela ya matumizi kwa sababu menejimenti iliyopo nayo imejiingiza kwenye dimbwi la kuhujumu. Kuna vipuli vingi vimeuzwa pale kama alivyosema Mheshimiwa Danhi Makanga, ukienda pale unasikitika. Watu wamenunua mashangingi kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri ninaomba haya mambo mawili atoe kauli na pale mimi niko tayari kuunga mkono hoja kwa mujibu wa taarifa ya bajeti hii kwa kweli bajeti nzuri kama itasimamiwa kama ilivyoandalialiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema asante sana. (*Makofî*)

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ya Ushirika na Masoko. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kazi kubwa ambayo alikabidhiwa ya kufufua ushirika na kuweka mifumo ya kuweza kupatikana masoko ya uhakika ya mazao yetu. Kusema kweli kazi aliyopewa Mheshimiwa Waziri ilikuwa ngumu kwa sababu kwanza ilikuwa ni Wizara mpya kwa hiyo kitu cha kwanza alitakiwa aanze kujenga mifumo, na katika masuala ya utawala hakuna jambo ngumu kama kuweka mfumo. Unapoweka mfumo unaweza ukafanya kazi vizuri, unaweza usifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukichunguza Wizara hii kwa kipindi kirefu Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wamefanya kazi kubwa ya kuweka mifumo na sasa kwa taratibu tunaanza kuona mafanikio ya kazi kubwa na ngumu ilivyofanyika ya ka mifumo ya kuboresha ushirika na masoko, si kazi nyepesi hata kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba nisema kwamba mchango wangu wa leo utaongozwa na mtizamo ufuatao:-

Hivi sasa bei anayopata mkulima wa kahawa ni chini ya asilimia 50 ya bei ya kahawa mnadani. Itakuwa jambo la busara na la hekima kama Serikali na wadau wengine wa kahawa wakipunguza au kufuta kabisa baadhi ya makato kwenye bei ya kahawa, ili mkulima apate zaidi ya asilimia 75 ya bei ya kahawa mnadani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia jedwali namba 8 (a) na 8(b) utagundua kwamba kuanzia msimu wa 2001/2002 mkulima wa kahawa alipata wastani wa asilimia 35 ya bei

ya kahawa mnadani, na msimu wa 2001/2002 mkulima wa kahawa alipata asilimia 11 ya wastani wa bei ya kahawa mnadani, na mwaka 2002/2003 mkulima wa kahawa alipata asilimia 25 ya bei ya kahawa ya mnadani, na mwaka 2002/2003 mkulima wa kahawa akapata asilimia 33 ya bei ya kahawa ya mnadani na mwaka 2003/2004 mkulima wa kahawa akapata asilimia 23 ya bei ya kahawa ya mnadani na msimu wa 2004/2005 pamoja na ukweli kwamba anachopata mkulima anaokimepanda, lakini ukifanya mahesabu ukweli ni kwamba mkulima wa kahawa sasa anapata asilimia 26 ya bei ya kahawa mnadani.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia Kenya naUganda, mkulima wa kahawa anapata zaidi ya asilimia 65 ya bei ya kahawa mnadani, na ndio maana utakuta baadhi ya wakulima wa kahawa wa Kagera wanaona ni bora wauze kahawa yao Uganda, wanaona ni bora wauze kahawa yao kwingineko kuliko kuitisha kahawa yao kwenye vyama vya msingi, na mimi nimekuwa nikisema siku zote kwa kuwa tuko kwenye *globalization* si dhambi kwa mkulima wa kahawa akaiza kahawa yake kokote kule ambako ataona kwamba atapata bei nzuri, si dhambi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini yako maswali ya kujiuliza inakuwaje mkulima wa Tanzania anapata chini ya asilimia 35 ya bei ya kahawa mnadani, lakini mkulima wa kahawa wa Uganda anahakika wa kupata zaidi ya asilimia 60 ya bei ya kahawa ya mnadani. Tulishajiwekea malengo huko nyuma kwamba tufanye kinachowezekana hapa Tanzania walau mkulima wa kahawa apate zaidi ya asilimia 75 ya bei ya kahawa ya mnadani.

Lakini hadi sasa hatujafanikiwa kuafikiwa kiwango hicho, kwa hiyo tunayokubwa mbele yetu ya kuhakikisha tunachukua jitihada za makusudi za kuhakikisha walau basi mkulima wa kahawa apate zaidi ya asilimia 60 ya bei ya kahawa mnadani, si kazi nyepesi ni kazi ngumu lakini lazima tuwe na malengo, ili tukifanikiwa tuseme tumefanikiwa na tukishindwa tuijulize kwa nini tumeshindwa. Sasa naomba niishauri Serikali izigatie yafuatayao ili walau tuweze kufikia asilimia 60 ya bei ya kahawa ya mnadani.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nichukue nafasi kuipongeza Tanzania *Coffee* bodi kwa kazi nzuri wanayofanya , na nilikuwa na ziara hivi karibu walinikaribisha vizuri wakanionyesha shughuli zao wanazozifanya, na kwa kweli hapo kabla mimi nilikuwa siungi mkono kuwepo kwa chombo hiki nilifikiri haufanyi kazi yoyote ya maana lakini baada ya ziara ile nimeridhika kabisa kabisa kwamba chombo hicho ni muhimu na kazi wanayofanya lazima Serikali iwaunge mkono kwa asilimia mia moja ili kuweza kuendelea kufanya kazi hiyo, na kwa sababu hiyo na baada ya kuwa nimeridhika na kazi inayofanywa na *TCB*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi Wabunge ndio tunaamua fedha ziende wapi na zisiende wapi nashauri Serikali katika bajeti zijazo ihakikishe inatenga fedha kwa asilimia mia moja za kuweza kuendesha *TCB* na kwa sababu hiyo hakuna haja ya kuendelea kukata asilimia moja kwa bei ya mkulima na badala yake Serikali ibebe

jukumu la kuendesha *TCB* kwa asilimia mia moja, kwa sababu kazi inayoifanya ni kwa niaba ya Serikali na ni kwa manufaa ya sekta ya kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la pili, mkifanya hivyo tutasaidia kuongeza ile asilimia moja tunayokata kwa mkulima kwenda *TCB* itarudi kwa mkulima, lakini vile vile hiyo asilimia moja aitoshi kuendesha *TCB* Serikali ikitenga fedha za kutosheleza, basi *TCB* wataweza kufanya kazi yao vizuri na kwa sababu hiyo mkulima ataweza kunufaika na Serikali itaweza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TCB* inaundwa kwa Sheria ya Bunge, hakuna sababu ya Serikali kushindwa kutenga fedha kwa asilimia mia moja za kuendesha *TCB* na kwa kuwa bei anayopata mkulima ni ndogo, ni chini ya asilimia 35, hakuna haja ya kuendelea kukata asilimia moja kwa ajili ya kuendesha *TCB*. Tukiweza kuzingatia hilo, *TCB* itaweza kufanya kazi vizuri lakini hata mkulima ateweza angalau kupata asilimia zaidi ya 60 ya bei anayopata mnadani. Huo ni ushauri wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 Waziri wa Fedha kwa mbwembwe na kwa staili ya aina yake aliliambia Bunge hili kwamba *VAT* katika kukoboa kahawa katika magunia, katika kuhifadhi kahawa, inafutwa. Tulishangilia sana, tukapiga makofi.

Mheshimiwa Spika, lakini uchunguzi wangu leo hii mwaka 2004/2005 katika Bajeti ya 2005/2006 sio kweli kwamba *VAT* imefutwa. Sio kweli hata kidogo! *VAT* bado iko palepale na mkulima wa kahawa anakatwa wastani wa Sh.10/= kwa kila kilo ya kahawa na fedha hii harejeshewi mkulima kama ambavyo tuliambowi kwamba itarejeshwa kwa mkulima. Kwa hiyo, hapa naomba niishauri Serikali kwamba ilivyofikiria kwamba *VAT* haipo, sio kweli, *VAT* iko pale pale na kwa sababu unapoendelea kumtoza *VAT* mkulima katika udogo wa bei aliyonao maana yake itakuwa mambo ya kufikirika kwamba siku moja angalau watapata zaidi ya asilimia 60 ya bei ya kahawa.

Kwa nini tunasema *VAT* haimwendesi mkulima? Ni kwa sababu tulifanya kosa la kiufundi tukasema *VAT* inakuwa *exempted* badala ya kuwa *zero rated*. Inapokuwa *exempted* maana yake unasema utaikusanya kwanza hiyo *VAT* halafu baadaye utamrejeshea mkulima.

Kwa hiyo, mwanzoni wakulima waliponiuliza, mbona Serikali ilisema haitakata *VAT*? Nikasema ndio nilisema, lakini walisema wanakusanya halafu watareesha. Kwa hiyo, msimu ukapita ikakusanya na tukaona zimekatwa Shilingi kwa kilo kama *VAT*. Lakini mwaka 2004/2005 Serikali ilirejesha *VAT*? Hakuna! Mwaka 2004/2005 Serikali ilirejesha *VAT*! Sasa kwa sababu ushahidi umethibitisha kwamba Serikali ikishakusanya hela, ni ngumu kuzirudisha, basi mimi nashauri kwamba ni vizuri kuanzia sasa au Bajeti zijazo basi, *VAT* katika zao la kahawa iwe *zero rated*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kudanganyana hapa kwamba ni *exempted*, tunachokuwa tunafanya ni kuwasaidia wafanyabiashara ndio wananaufaika kwa kununua

kahawa na baadaye kudai *VAT TRA* na wakishapata zile fedha hawamrudishii mkulima hata siku moja!

Mheshimiwa Spika, ukitizama bei anayopata mkulima, sababu nyingine inayochangia apate fedha kidogo ni kwamba tunakata *CES* kwa ajili ya kusaidia kuendesha Halmashauri zetu. Lakini kwa bahati nzuri baada ya uchumi wetu kwenda vizuri hivi sasa ruzuku inayotoka Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri zetu imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 1,500. Kwa sababu hiyo, hakuna haja tena ya kuendelea kukata *CES* katika kahawa ya mkulima kwa ajili ya kuendesha Halmashauri kwa sababu tayari Serikali imeongeza ruzuku za kuendesha Serikali hadi zaidi ya asilimia 1,500. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kuendelea kukata *CES*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo lingine kwa wale wanaotumia pembejeo, unakuta kwamba hazipatikani kwa uhakika na hii ni kwa sababu pembejeo ni *exempted, zero rated*. Suala hili linafanana na la *VAT*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo itamsaidia mkulima kunufaika zaidi, tuharakishe utafiti wa kuwa na miche ya uhakika ili tuweze kupunguza magonjwa na kuongeza ubora wa kahawa inayozalishwa na mkulima. Kama tukiweza kuongeza uzalishaji wa kahawa kwa heka, maana yake mkulima atazalisha kahawa nyingi zaidi kwa heka ndogo na kwa hiyo, ataweza kupata faida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo niipongeze *TCB* pale Moshi ni kwamba sasa tuna mnada wa kisasa, ambapo sasa wanunuzi wa kahawa wakifika pale wanaangalia kwenye *screen* kama video, mtaalamu mwendesha mnada anasema, leo hii kulingana na bei katika Soko la Dunia ni Shilingi hizi. Kwa hiyo, waliokaa kwenye viti inabidi ubonyeze pale, usipobonyeza mwingine atabonyeza na kwa hiyo, huwezi ukajua nani anafanya nini. Kwa hiyo, ni mnada wa kisasa kabisa na ni pekee katika Afrika Mashariki na pekee katika Afrika.

Namshukuru Mheshimiwa Balozi George Kahama na *TCB* kwa kuweka mifumo, ndio maana nimesema kuweka mifumo ni jambo gumu, lakini mfumo ule haujaunganishwa na minada ya Kimataifa. Litakuwa jambo la busara sasa mfumo huu ukiunganishwa na minada ya Kimataifa ili mnada unapokuwa unaendeshwa Moshi hata walioko London, Washington waweze kushiriki kwenye huo mnada na kwa kuweza kushiriki, basi mkulima ataweza kupata bei kubwa zaidi kuliko ambavyo anapata hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kutizama ni kupunguza gharama za kuendesha Vyama vyta Ushirika. Nimeangalia humu nimeona zipo *apex* zilizofutwa. Lakini napenda niseme bado tunaweza. Tukifanya uchunguzi wa kina ziko gharama nyingine ambazo tunaweza tukazipunguza.

Mheshimiwa Spika, lingine katika Bunge hili linalomaliza kipindi chake katika sheria mpya ya Tanzania, *Coffee Board* tuliweka kipengele kinachoanzisha *Coffee*

*Stabilization Fund.* Kama ninavyosema, kuweka mifumo ni jambo gumu, lakini ule Mfuko hadi sasa haujaanza kufanya kazi zake. Sasa itakuwa ni jambo la busara kama sasa tukihakikisha siku zijazo Mfuko huu uanze kufanya kazi yake mapema ili pale bei zinapoporomoka, basi Mfuko huu uweze kumfidia mkulima wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine itakayosaidia kumwonyesha mkulima kwamba bei inapoporomoka, anaweza kupata fidia. Basi zile fedha za *STABEX* ambazo huko nyuma tulikuwa tunazitumia kwa kumpa mkulima moja kwa moja pamoja na kwamba wanaotoa fedha hizi wamekataa tusifanye hivyo, basi tujipange upya. Tujenge hoja upya tuwaeleze hao wenzetu kwamba sasa hivi tuko katika uchumi wa soko na unapokuwa kwenye uchumi wa soko jambo linaloweza kukusaidia na kumsaidia mkulima kuongeza uzalishaji, kuongeza *productivity* siyo kupitia jambo lolote lile isipokuwa bei anayoipata. Ile bei anayoipata mkulima ndio inaweza ikatoa motisha kutunza shamba lake vizuri, bei anayoipata ndio inaweza ikawa motisha kufanya kila kitu vizuri. Kwa hiyo, natoa changamoto kwamba tujipange upya ili tuweze kuwashauri hawa wenzetu waweze kutoa fedha hizo moja kwa moja kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho, basi wakati umefika kuacha kutoza kodi katika Mifuko ya Wakulima kama Mfuko wetu wa Kagera, Mheshimiwa Balozi George Kahama anafahamu kwamba ule Mfuko wetu unatozwa kodi na umeyumba na pamoja na ukweli kwamba ametangaza kustaafulakini bado ataendelea kuwa Mwana-Kagera, ataendelea kuwa na sisi na naomba uendelee kulifuatilia hili hata baada ya kustaafuli ili wengine wanaofikiria kwamba Mifuko hii ni vizuri ikatwe kodi, basi waweze kuelewa kwamba Mifuko hii ni vizuri isikatwe kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko. Kwanza kabisa naomba nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Balozi Clement George Kahama, Naibu wake Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje na Viongozi wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukweli wa mambo ni kwamba, Wizara imepata wenyewe na wanafanya kazi nzuri, kama wanaangushwa, wanaangushwa na hao Maafisa Ushirika kwenye Wilaya. Lakini wao wana uwezo mkubwa na sisi wengine ambao tuko kwenye Kamati ya Uwekezaji na Biashara tunathibitisha hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kauli mbiu ni MKUKUTA. Ushirika ni njia ya uhakika ya kukuza uchumi na kupunguza au kuondoa umaskini wa kipato. Mimi nitazungumzia zaidi Ushirika ninavyouona katika Wilaya ya Kilosa. Katika Wizara ya Kilosa, Ushirika umefifia sana na kwa kweli unaweza kuulinganisha na mgonjwa aliye katika chumba mahututi yaani katika *Intensive Care Unity*.

Katika sehemu nyingi Vijijini unapowazungumzia wananchi juu ya kuanzisha Ushirika au kufufua Ushirika, wanasita wakikumbuka wizi, ubadhirifu na rushwa

iliyokithiri katika Vyama vya Ushirika vilivyo sambaratika. Kwa hiyo, inahitajika kazi ya ziada kuwahamasisha waingie kwenye Ushirika na mimi naona ziko hatua zinazostahili kuchukuliwa katika kufufua Ushirika, kuanzisha Vyama vipya vya Ushirika na kuimarisha Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwanza Idara ya Ushirika kwenye Halmashauri za Wilaya zinahitaji kuimarishwa. Kuna upungufu wa wataalam wa Ushirika kwenye Halmashauri na wale waliopo hawapewi fedha na nyenzo za kutosha za kufanyia kazi. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Wizara kupeleka pikipiki kwenye Halmashauri, lakini naona inafaa ifikiriwe kuwapelekea magari kwenye Halmashauri Maafisa Ushirika ili waweze kuwafikia wananchi Vijijini jambo ambalo kwa sasa halifanyiki.

Mheshimiwa Spika, pili, Maafisa Ushirika hawa wapimwe utendaji wao wa kazi kwa idadi ya Vyama vya Ushirika vinavyo imarishwa na vinavyofufu liwa katika maeneo yao ya kazi kila mwaka. Tunahitaji Vyama vya Ushirika vya Msingi ambavyo ni imara.

Mheshimiwa Spika, tatu, Viongozi tukiwemo Wabunge kwa kushirikiana na wataalam wa Ushirika, tuwahamasishe wananchi wajijunge kwenye ushirika mpya ambao ni tofauti na ule wa zamani. Waelewe kwamba Ushirika huu tunaouzungumzia sasa ni Ushirika ambao hausimamiwi na wala si chombo cha Serikali bali ni chombo cha wanaushirika wenyewe. Lakini wanaushirika wanahitaji kuelimishwa, kwanza waelimishwe juu ya dhana ya Ushirika, waelewe maana ya Ushirika. Vilevile waelekezwe namna ya Menejimenti, namna ya kuusimamia Ushirika katika Vyama vyao na vilevile, wafundishwe namna ya kusimamia fedha za Vyama vya Ushirika. Vyama vya Ushirika vilisambaratika kwa ajili ya wizi katika Vyama vya Ushirika na vilevile waelimishwe faida ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Ushirika ni chombo mahsusini kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuwapunguzia umaskini wa kipato. Ushirika wa Vyama vya Tiba na Mikopo yaani *SACCOS* ni Ushirika ambao unastahili nao kuwekewa umuhimu mkubwa. Mimi ninavyoona Vyama vya Akiba na Mkopo katika ngazi ya Tarafa ni bora zaidi kuliko Vyama vya Ushirika katika ngazi ya Kata au Vijiji, kwani katika Tarafa Vyama hivi vinakuwa na mitaji mikubwa na kwa kusema kweli vinakuwa imara. Sisi wa Tarafa ya Gairo tunaona wazi mafanikio mazuri ya *SACCOS* ya Gairo ambayo hivi sasa uwezo wao umefikia kuwa na jengo zuri la kisasa na vilevile wana huduma za *Tembocard*.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa maeneo ya wachimba madini nalo ni jambo la muhimu kabisa. Katika Jimbo langu la Gairo, miaka miwili iliyopita vijana, wasichana na wavulana walikuwa wanachimba madini ya *Celsper* na hivi sasa kuna vijana wanaohangaika kuchimba madini ya *vital* katika Milima ya Ukaguru. Lakini hawajahamasishwa wala hawajajiunga katika Vyama vya Ushirika ili waweze kufaidi na kuwa na uwezo wa kununua zana na vilevile vitendea kazi vya kuchimbia madini hayo, wanahangaika na kwa kweli wengine wamekufa wakati wanachimba madini kwa kufukiwa na mchanga kwa sababu wanatumia zana duni na wanachimba katika mazingira ya hatari kabisa. Kwa hiyo, wanastahili kuhamasishwa wajijunge kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, ukweli wenyewe ni kwamba mara nyingi utawaona hawa wachimbaji wadogo wadogo, wanapopata ile mali wana tabia ya kuifuja na matokeo yake ni kwamba hawafaidiki sana na mali wanayoipata wanaitumia ovyo na wanabaki pale pale katika hali ya umaskini. Mimi naamini kwamba wakijiunga katika Vyama vya Ushirika wataweza kutumia mapato wanayoyapata kwa busara zaidi na vilevile wanaweza kupata uwezo wa kuwa na mitaji mikubwa na kuweza kununua zana za kisasa na vifaa vya kisasa kwa kuchimbia madini na ni kwa njia hiyo tu badala ya kubaki katika hali ile ya umaskini watainua hali zao na kuwa na uwezo wa kipato.

*(Hapa umeme ulikatika na kuwaka baada ya dakika mbili)*

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, wakulima katika sehemu nyingi nchini wana tatizo la kukosa masoko ya uhakika kwa mazao yao. Suala la masoko linakwenda sambamba na suala la maghala na suala la maghala limepata umuhimu mkubwa tangu tupitishe Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao katika Maghala. Wakati umefika wa Serikali kuwaelimisha wananchi kwa utaratibu endelevu isiwe ni jambo la kulipua ili waelewe juu ya matumizi ya Mfuko wa Stakabadhi za Mazao katika Maghala na vilevile tujue ni aina gani ya maghala yanafaa kutumiwa katika mfumo huu. Kwa mfano katika Jimbo kwa masaada wa *FREDA* katika Vijiji viwili vya Mkalama na Majawanga wananchi wamejenga maghala. Lakini sina uhakika kwamba maghala hayo yana sifa za kuweza kutumiwa katika mfumo huu wa stakabadhi za mazao.

Kwa hiyo, ingefaa maghala hayo yakaguliwe na waelezwe kama yanafaa au hayafai na hasa tuelezwe ni sifa gani za maghala yanayostahili kuingia katika mfumo huu wa stakabadhi za mazao, kwani mimi naamini kabisa kwamba wakielewaa utaratibu huu na tukajenga maghala au kufufua yale ambayo yalikuwa ya Ushirika, wananchi wanaweza kufaidika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Gairo walionichagua kuwa Mbunge wao na kunipa nafasi ya kuwatumikia kwa vipindi viwili mfulululizo. Tulishirikiana kusukuma gurudumu la maendeleo wote tukiwa tunaongozwa na Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi Oktoba mwaka 2000. Ninaamini kuwa nilitimiza wajibu wangu na sikuwaangusha na msemo wa Kiswahili unasema imani huzaa imani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naishukuru familia yangu kwa kunitia moyo wakati wote katika msukusuko wa Ubunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, shukrani za pekee ziende kwako, umekuwa mhimili mahiri wa Bunge hili kwa muda wote. Tumefaidika vya kutosha na uongozi wako, naamini Taifa bado linakuhitaji. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika hii Bajeti ya Waziri wa Ushirika na

Masoko. Kwanza nampongeza sana Mzee wetu Mheshimiwa Balozi George Kahama pamoja na Naibu wake na wataalam, Wakurugenzi na Katibu Mkuu ambao wameleta Bajeti ambayo ni nzuri, inakidhi matakwa ya Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Balozi George Kahama anastaafu, lakini ametuachia kazi ya kufanya na ameweka mifumo. Ukiangalia hii hotuba yake ni kwamba anatuaga akiwa ametuachia mifumo ya miaka mingi sana ya kutekeleza misingi mizito sana. Kwa kweli Wizara hii imeanzishwa juzi juzi katika kipindi hiki, lakini kazi waliyoifanya ni nzuri kwa kipindi kifupi. Nina hakika wakiendelea kwa mfumo huu na kutekeleza haya ambayo wameandaa, masuala ya ushirika yataimarika.

Mheshimiwa Spika, labda nizungumzie mambo matatu. La kwanza, katika ukurasa wa 68 katika Bajeti yake wamezungumzia suala la Soko la Mahindi la Kibaigwa la Kimataifa. Kwanza nawashukuru sana, wamenikaribisha katika masuala yote ambayo yanafanya katika Soko la Kibaigwa japokuwa hili la mwisho ambalo nimepata barua yao lilipokuja kufunguliwa. Nawashukuru sana. Ila nataka niseme kidogo kuhusu hili Soko la Kibaigwa ambalo liko njiani pale kuelekea Dar es Salaam. Katika Soko la Kibaigwa mimi nadhani walijenga tu kwa sababu kuna mawasiliano mazuri kati ya Dar es Salaam na Dodoma, lakini mahindi haya yanayozungumziwa yanatoka Kiteto. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa wamekuwa na matatizo makubwa ya kwamba mbona soko linakuwa haliendi kama inavyotakiwa? Kwa sababu tukitaka kuleta mahindi Kiteto tunategemea soko liko namna gani katika bei yake. Sasa hivi katika ukanda huu wote, mahindi yanapatikana Kiteto na ndio yanayolisha Dar es Salaam, Soko la Tandale ndio yako Himo ndio yanalisha Kenya. Yanatoka Kiteto. Hili soko limekaa kama *white elephant* pale tukipeleka mahindi mpaka gunia ushone na ushindilie debe nane, debe saba lumbesa hilo. Sasa tukipeleka Himo tunapima kwa kilo! Lile soko ambalo sisi tunasikia kuwa ni soko la Kimataifa liko Himo, sisi kwetu tumeliacha limekaa na mambao yake hapo. Kwa hiyo, lazima mwelewe kabisa kwamba hili soko lazima mliweke katika mazingira ambayo kwa kusema kweli yanavutia na bei yake.

Suala lingine ambalo liko hatarini ni kwamba tuna masoko ambayo tumeyafungua ya Dongo, Engusero na Matui, Naibu Waziri anayafahamu vizuri sana ambayo yanashamiri kama Soko la Kibaigwa. Lakini hatuna mkono wenu wa kuweza kuunganisha kati ya Kibaigwa na masoko yale madogo yanayozunguka. Mmeandika hapa kwamba tunataka kuimarishe barabara, ama sivyo kama huwezi kutengeneza barabara nzuri kutoka Dongo ili sasa waweze kulisha Soko la Kibaigwa sasa hivi kuna barabara nzuri inayojengwa na ninampongeza sana Mheshimiwa Job Ndugai kwa juhudzi zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kujenga barabara inayounganisha pale njia panda mpaka Kiteto, inajengwa barabara nzuri sana ambayo kwa kweli ndio itakayonufaisha Soko la Kibaigwa. Suala la miundombinu ya Kibaigwa lazima ishirikishwe Kiteto ndio sasa ukizungumza Kibaigwa usipozungumza Soko la Dongo, Soko la Engusero, Soko la Matui hujataja chochote pale. Mimi nataka nielimishe tu kwa wale wanaokuja, Mzee

anastaafu lakini kwa huyu anayebaki na usia ambao ataacha akiondoka aandike hilo. Aandike kabisa kwamba nimejenga Soko la Kibaigwa lakini bila kuendeleza masoko haya na miundombinu, aandike kabisa na kuweka saini yake hapo halafu aache, halafu akiondoka, basi ndio niachie hapo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la watumishi. Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo amezungumza sana kwamba hatuna watumishi walioko Wilayani. Mimi kwangu pale sitaki kuzungumza wako, lakini wamekaa kama watoto yatima pale, nani anawaangalia? Siku hizi sijui wanafanya mahesabu ya wapi, maana yake pale Vyama vyta Ushirika vya Msingi hatuna, unamkagua nani pale? Mimi kwangu sijui kama kipo. Najua zilikuwa sijui saba, sijui nane lakini vile vyombo vya Ushirika tulikuwa na *ACU* ikaisha, tukaja *RIVACU* sasa tuko Manyara hatujui Kiteto sasa tuko kwenye *ACU* au tuko *RIVACU*. Vyombo vya Ushirika vimekodiwa vyote sasa na kweli tuna upungufu mkubwa sana sijui wataalam wanafanya utafiti kiasi gani. Kama ingewezekaza sisi Kiteto tupate ushirika wetu, haya masuala ya kutegemea kweli umoja ni nguvu lakini wamekuwa walaji wakubwa sana na wanapokula hata hayabakizi yanaishia huko hewani, bora sisi Kiteto tunganezlisha Chama chetu cha Ushirika, hata tukila tunajenga angalau vibanda vya Kiteto. Lakini wale wakila wanatawanyika huko huko hatujui. Kwa hiyo, mimi nadhani sisi kama mnaturuhusu, tuanzishe Chama chetu cha Ushirika Kiteto na mtuletee wataalam wa kuweza kuanzisha Chama.

Kama tunaweza kuuza mahindi nchi nzima, kwa nini tusianzishe Chama cha Ushirika ambayo ni karibu watu wote wanaweza wakajumuika? Sasa tuna shamba letu la Magungu la Ushirika limekuwa chombo cha kukodishwa, linatukera wanavijiji wa Magungu, Songambele, Orgine wametoa ekari zaidi ya 2500 kwa Chama cha Ushirika cha *ACU*. Chama chenyewe kimesambaratika, hatujui.

Sasa kama kimeshindikana ile ardhi irudi kwa wanakijiji wetu kuliko kuwakodishia watu hatuelewi kama ni wakubwa, wanavijiji wetu wanaangalia. Magungu sasa naomba mfanye haraka sana kabla sijawatangazia tukavamia hilo shamba, maana yake nikitamka mara moja tu wanaingia. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, naomba kabisa tupate suluhu ya lile shamba la Magungu badala ya kukodisha watu wengine wakodishwe basi wanavijiji wetu walime. Wanavijiji sasa hivi hawana mahali pa kulima na wametoa zaidi ya ekari 2500, watu wa Magungu, Orgine, Songambele wanaona watu nyuso mbalimbali wanakuja kukodisha katika ardhi yao. Sasa hilo ni changamoto na mimi niishie hapo hapo. (*Kicheko*)

La pili na la mwisho ambalo nataka kuzungumza, ni suala la utaratibu tu. Hivi katika huu Ushirika, Ushirika yenyewe ni wa mazao tu? Sijaona hata neno la ng'ombe ndani ya kitabu hiki imekuwaje! Yaani hakuna Ushirika wa ng'ombe kabisa! Ni mahindi, kahawa, ngano na masoko.

Hivi tunapouza sisi ng'ombe, sasa hivi ng'ombe wako Pugu kuna masoko kule au hamuhusiki nayo kutafuta bei ya wanyama kama kuku, nguruwe na kadhalika haipo ndani ya Ushirika? Maana yake mimi hapa siyaoni mayai na kadhalika au kuna Wizara

yake? Labda mimi kwa akili yangu haya mambo ya Masoko, ni masoko kwa mazao tu ya wakulima, basi ndiyo tuelewe au masoko, bei ya ng'ombe haihusiki kabisa kwamba uende Uarabuni utafute bei ya ng'ombe ikoje, ninyi hamhusiki kabisa!

Kwa hiyo, mimi nilitaka nielewe tu kwamba kwa kusema kweli ni vizuri kama ni Idara ya Masoko, iangalie kwa nyanja zote za kiuchumi masoko katika nchi nzima na mazao yote ambayo yanahitajika kusema kufanyiwa biashara ili muweze kuunganisha moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote, kwanza nichukue nafasi kukushukuru sana wewe na mimi kwa kusema kweli kwa kuwa nimechelewa, lakini kwa kipindi kifupi cha wiki hii moja nimekuwa nimetimiza wajibu wangu wa kuwa Mbunge wa Kiteto. Mimi kusema kweli bado nahitaji kuwa Mbunge, kwa hiyo, kama ni kuanguka tu, basi lakini kwa kweli nina hamu ya kuja kwenye jumba hili na nimekuwa na Spika kwa muda mrefu sana tangu nilipokuwa kijana sasa hivi na bado tu kijana, hata Spika wetu bado kijana tu, maana yake ndiyo Hazina na Uzee ni Dawa. (*kicheko/Makofi*)

Kwa kusema kweli tunaamini kwamba tutakapoondoka hapa tutakwenda kuomba nafasi katika Majimbo yetu na nina hakika tutafanikiwa kwa sababu mimi nikiwa mzoefu katika kazi ambayo imefanyika katika nchi hii ni kipindi cha mwaka 2000-2005 katika Majimbo na ni kazi kubwa. Miaka ya nyuma tulikuwa hoi, lakini miaka hii ya mwisho tumefanya kazi ambayo ni nzuri sana na Bunge hili limefanya chini ya Spika. Spika anajenga jengo la Kimataifa hapa, nani ataanza kuingia? Ni yeye, abariki halafu aachie kwa sababu ndiyo utaratibu hata ukijenga nyumba nyumbani au boma ukishaweka kwenye boma ni vizuri Mzee boma aanze kukaa na kubariki na kuletewa kiti kwamba hii nyumba ni yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote, tuombeane kila la kheri na wale wanaoingia kwenye Majimbo wanaingia tu lakini wanaingia kwa sifa zetu na lazima watutaje na wasipotutaja hawapati kitu. Kwa hiyo, wala msiogope kwenye mapambano, kwani mapambano ndiyo yenye na ndiyo siasa na nikiwa na uzoefu hapa ni kwamba kwa kawaida theluthi moja inamegeka, theluthi mbili inaingia ndiyo utaratibu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko inayohusu bajeti ya Wizara yake ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha hoja yake kwa ufasaha mkubwa na imetoa matumaini makubwa katika maendeleo ya Ushirika na Masoko ya Mazao yetu katika mwaka huu wa fedha. Naipongeza sana hotuba hii ya Waziri na ninaiunga mkono mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya za kujenga upya Ushirika. Wao wenyewe wanao uzoefu mkubwa na wa miaka mingi katika Ushirika na kwa kweli kwa kusimamia Wizara hii, basi wametoa changamoto kubwa ya kufanikisha maendeleo ya Ushirika. Pia, nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Wakurugenzi wake kwa kazi nzuri na kwa kukubali kuishi Dodoma, kwa kuhamia Dodoma maana hilo nalo ni la msingi, kwani Wizara nyingine na Wakurugenzi wengine wanasuasua kuhamia Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Ushirika na Masoko ni muhimu sana kama walivyosema wenzangu katika kuleta maendeleo ya mkulima na kumwondolea umaskini. Mkulima anapolima anategemea kuyauza mazao yake ili apate fedha za kuijendeleza na kujitoa katika umaskini. Mkulima huyu atafaidika na kilimo chake kama atapata bei nzuri kwa mazao yake, bei ambayo kwanza itarudisha gharama alizotumia katika kilimo na pili ziada au faida ambayo ndiyo itakayomsaidia kupanua na kuboresha kilimo chake na papo hapo kutatua matatizo yake.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mkulima ni soko la kuaminika la mazao yake na bei inayolingana na gharama za uzalishaji wa mazao yake. Hilo ndilo tatizo la msingi la mkulima.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo suala la tatu ambalo nataka nilitaje hapa na ni nimewahi kulisema hapa Bungeni kwamba haitoshi kwa mkulima kuuza mazao yake yakiwa ghafi bila kuyasindika, bila ya kuongezea thamani ili kumwezesha mkulima huyu kupata bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchakato wa kumwondoaa mkulima katika umaskini lazima ukamilike kwa mkulima kuwa na soko la uhakika, soko la mazao ya mkulima yaliyosindikwa. Katika mchakato huu wa uzalishaji wa mazao ya kilimo, soko ni hatua ya mwisho na ya mwanzo ya kuanza mzunguko mwingine wa kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara hii kwa ujumla nataka nisema kama nilivyosema hapo mwanzo, imefanya jitihada za kutosha katika mchakato huu na ninaipongeza sana kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, jitihada za Serikali zielekezwe zaidi katika mazao mchanganyikao hususan ufuta, alizeti, karanga, njegere, mbaazi na kadhalika, kwa mazao ambayo kwa bahati mbaya yanaitwa Mazao yasiyo Asilia.

Mheshimiwa Spika, haya mazao niliyoyataja Waziri na Serikali wanayaita mazao yasiyo asilia, nasema kwa bahati mbaya na nitaelezea kwa nini ni kwa bahati mbaya. Mazao haya yamesahaulika na ndiyo yanayotegemewa na wakulima wa Jimbo langu la Kibakwe na Wilaya ya Mpwapwa kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wakulima wa Jimbo langu walilima ufuta kwa wingi kwa mategemo kwamba ufuta huo utawaondoa katika umaskini wa kipato. Lakini imekuwa tofauti, ufuta huo haukupata soko, ufuta huo bado umo mikononi mwa

wakulima na wale waliouza ufuta wameuza kwa bei ndogo sana tena wameuza ufuta ule kwa walanguzi.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa na walanguzi maana yake ni kwamba hapana Ushirika pale. Walanguzi wanachukua nafasi ya Ushirika au wanachukua nafasi ambayo imeachwa na Ushirika wa namna fulani ambaa ungeweza kuunganisha nguvu za wakulima ili wapate soko la pamoja na soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawana tatizo la kulima, kuitikia kulima mazao ya biashara, wanalima. Mimi hapa ninachoomba wasaidiwe kupata soko la ufuta wao.

Mheshimiwa Spika, hiyo maana yake nini? Maana yake sasa Ushirika uelekeze nguvu zake huko kwenye mazao mchanganyiko, Sheria ya Stakabadhi ya Mazao nayo ilekezwe huko kwenye mazao yasiyokuwa ya asilia.

Mheshimiwa Spika, wanachohitaji ni mazingira ya kuwawezesha kupata teknolojia rahisi ya kusindika ufuta wao, alizeti yao ili wauze mafuta badala ya kuuza mbegu, badala ya kuuza mazao ghafi na hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa maoni yangu bado lipo tatizo la msingi na lazima Serikal iondokane na tatizo hili. Nalo ni lile la kuwa na mtazamo tofauti wa mazao haya ya wakulima. Kwa miaka mingi tumejenga mtazamo kwamba yako mazao ya biashara ya asilia na mazao ya biashara yasiyokuwa asilia yakiwemo ufuta, alizeti na karanga na mengineyo.

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake sehemu kubwa ameelezea ununuzi na uuzaaji wa mazao ya biashara asilia. Ibara ya 70-78 na ametumia Ibara moja tu kuelezea ununuzi na uuzaaji wa mazao yasiyo asilia Ibara ya 79 na kule amezungumzia maua na mbogamboga. Mazao ya mafuta kama alizeti, ufuta na karanga hayakupata nafasi. Kwa sababu hiyo, suala la kuunda Bodi ya mazao haya limeachwa kabisa na Wizara hata katika kazi zilizopangwa na Wizara mwaka huu 2005/2006 suala la kuunda Bodi ya mazao mchanganyiko halimo na ninahisi limewekwa pemberi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana najenga hoja kwamba pengine kuna tatizo la msingi la mtazamo wa Serikali kuhusu alizeti, ufuta na karanga ukilinganisha na mtazamo wake kuhusu kahawa, pamba, tumbaku na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mazao ya biashara yasiyokuwa ya asilia yanategemewa siyo tu na wananchi wa Jimbo langu, lakini na sehemu kubwa ya wananchi karibu nchi nzima. Lakini nataka niulize, ni lini Serikali itaacha kuondokana na mtazamo huo wa kutenganisha mazao ya wakulima wetu? Mgawanyo huu hauna mantiki na niliwahi kusema hapa siku moja kwamba hauna mantiki, unawagawa wakulima kwa msingi wa mazao yao na kwa kweli umepitwa na wakati, tusiendelee nao.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri angenipa maelezo ni kwa nini Serikali imekuwa ikiendelea na mgawanyo huu wa mazao ya wakulima na kuwa na mikakati tofauti ya

kuyaendeleza na ni lini Serikali itajikwamua kutoka katika historia potofu ya mazao asilia na yasiyo asilia?

Mheshimiwa Spika, kuna wakati nilitumia muda mrefu hapa kipindi kilichopita kuelezea historia ya asilia ya mazao. Mimi wakati ule nilitegemea Wizara ingekuwa imelielewa somo hilo na kwa kweli leo sina haja tena ya kulirudia somo hili la Asili ya Asilia ya Mazao, lakini tatizo walipatalo wakulima wetu wa alizeti, ufuta, mbaazi na nyonyo linatokana kwa kiwango kikubwa na asili ya asilia ya mazao yao. Wamekuwa wanaathirika kwa mtazamo huo kwa sababu ya historia ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli leo ningependa kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri lini ataacha huu utaratibu wa kugawa wakulima kulingana na mazao yao? Kwa nini tusiwe na mkakati wa kuendeleza mazao yetu yote ambayo yanawasaidia wakulima wetu na yanawaondoa katika umaskini?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe nawashukuru kwa kunipa nafasi hii niwe Mbunge wao na ninawaahidi wakinichagua tena nitakuwa Mbunge mzuri wa kutetea maslahi yao. Kwa Sir George Kahama anastaafu, namtakia kila la kheri, lakini nina uhakika Ndugu yangu Chibulunje atagombea, namtakia kila la kheri wananchi wajue na watambue kazi zake ili wamchague tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwako wewe kama alivyo sema Ndugu Losurutia hili jengo unalojenga jipya ingefaa uingie ili uweke mazindiko kabla ya watu wengine kufanya kazi humo.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia miwili, matatu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Sir George Kahama kwa hotuba yake nzuri. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ni mtani wetu Mheshimiwa Chibulunje, Mgogo, kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Wizara hii. Niwaponge pia Wataalamu wote kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, Shemeji yangu, kwa kufika Tabora na kufanya kazi nzuri. Kwa hiyo, nilipoiona hotuba yake sikuwa na wasiwasi naye kwa sababu hotuba aliyoitao yeye mwenyewe akiwa kwenye jukwaa ilikuwa ni hotuba ambayo kwa kweli ni nzuri sana kiasi ambacho imeleta matumaini makubwa kwa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nianze moja kwa moja kuzungumzia suala zima la Tumbaku. Kwa kweli kwa Tanzania suala la Tumbaku limeanza Tabora na

tumbaku ni zao ambalo linategemewa sana kwa miaka ya nyuma kwa Mkoa wa Tabora kuwaleta maendeleo. Mkoa wa Tabora ulikuwa unakua kwa haraka sana lakini kwa sasa hivi suala la tumbaku asilimia kubwa ya wakulima wameanza kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, tumbaku ni kazi ambayo ina haribu sana huwezi kulinganisha na kazi ya kahawa na korosho. Haiwezekani kwa sababu yale ni mazao ambayo yanataka usimamizi. Lakini tumbaku unapoanza kuizalisha unaweka kwenye vitalu mpaka unaimaliza hatimaye inaitwa tumbaku. Ni kazi nzito ambayo haina kupumzika, haina hata kusema wanaweza kupata nafuu ya kupumzika.

Lakini uuzaji wake ni tatizo. Matatizo yaliyojitekeza katika uuzaji wake ni zile haribu za kupata soko kwa sababu mnunuzi ni mmoja kwa masharti anayoyataka yeye na kama mnunuzi ni mmoja, basi ni tatizo kwa sababu anatoa amri anazozitaka yeye kwa mfano pembejeo anazitoa yeye kwa mkulima, anawakopesha. Sasa hivi kumeingia suala la kukopesha mahindi, sasa unategemea mkulima atapanga bei? Hawezi kupanga bei, atapanga yule aliyemkopesha kwa riba anayoitaka yeye.

Sasa Serikali na Wizara hii iko wapi kumsaidia mkulima ili angalau basi kuwe na utaratibu mzuri wa kumwezesha mkulima wa Tumbaku ambalo ndilo zao kuu la Biashara kwa Tanzania. Ni vyema kuwapa moyo wa kuwapa mkopo wakulima kwa kupitia Vyama vyao vya Ushirika ili kama kuna uwezekano badala ya huyo mnunuzi wa tumbaku, basi Vyama vya Ushirika vipewe hiyo mikopo.

Mheshimiwa Waziri kwa kazi yako nzuri, naomba hili uliangalie kwa kutoa kifungu maalum cha pesa kwenye Bajeti yako au kwa kuacha maandalizi mazuri hata kwa Bajeti inayokuja angalau kuwe na fungu la wakulima wa tumbaku, kwa kuwa wamekuwa watumwa wa bei kwa sababu wanapangiwa. Kwa hiyo, nakuomba Waziri uliangalie kwa undani kwamba hili ni tatizo kubwa kwa wakulima wa tumbaku.

Mara ya kwanza miaka ya nyuma kulikuwa na Bodi ya Tumbaku (*TAT*) ilikuwa inakwenda kuangalia na kutenganisha *grade* za tumbaku, lakini sasa hivi hawa walipo wanachanganya. Wakulima wetu hawana uzoefu wa kujua kwamba hii ni *grade I* au *grade II*, wataalamu wako wamesomea. Basi wakati wa mauzo ya masoko waende waangalie je, ni kweli kwamba hii ni *grade I* na kiasi wanachopewa ni sahihi? Serikali isijitoe kwa kila kitu, haya mazao ambayo ni ya biashara yanayoleta heshima Taifani kwetu ni vyema Serikali ikasimamia mauzo ya bei.

Kwa mfano pamba. Nilikwenda Kijiji kimoja kinaitwa Kashishi, mpakani na Kahama, wametoka wamepeleka kwenye soko Shinyanga, baada ya kupeleka kule Shinyanga wakaambiwa soko halipo wakarudisha tena, wanakuwa watumwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wataalamu wake wasimamie masuala mazima ya ununuzi wa bidhaa hizi. Ni tatizo! Hayo mazao ni tatizo! Sasa kama tutakuwa tunayaacha ili mradi tu Serikali imejitoa na Taifa pia litakuwa maskini kwa sababu hakutakuwa na jina kubwa, hakutakuwa na biashara ya kitaifa isipokuwa kutakuwa na biashara ndogo za watu ambao wanajiamualia wenywewe.

Itakuwa kama wamachinga kwa sababu hawana msimamo wa biashara zao. Kila kitu Serikali imejitoa. Mimi nilikuwa naomba kwa mazao ya korosho, kahawa, pamba, tumbaku Serikal isijitoe ili kuwasaidia wakulima waweze kuwa na moyo. Wamekuwa masikini, wanaonufaika ni wale wanaonunua, lakini mkulima wa tumbaku au mazao haya yuko chini maisha yote.

Serikali inaangalia nini? Hata mazao mengine Mjumbe amesema kuna mazao mengine madogo madogo ambayo wakulima wanakata tamaa, wakati wa miaka ya nyuma *National Milling* ilikuwa inanunua mpaka ufuta aliosema Mheshimiwa Mjumbe hapa. Mbunge amesema hata haya mazao madogo madogo tusiwarudishe nyuma kwa mfano Tabora wanalima sana mpunga, kuna masuala ya *irrigation* Igunga; je, hawa nao hawatakiwi kutafutiwa soko kama Kibaigwa ili nchi nzima wakawa wanauzza masuala ya mpunga? Kwa hiyo, nilikuwa naomba tusizingatie tu masuala ambayo tuna uhakika yanaleta hela ndogo kuliko haya ambayo yanaweza kuchangia pato kubwa sana la Taifa na hatimaye kuwa na mfumko mzuri wa bei ambayo ni ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuna kiwanda cha nyuzi Tabora, kiwanda cha nyuzi kimeanza hivi karibuni sasa. Kama soko la pamba litakuwa duni au halitaeleweka kitakufa. Hawataweza kununua kwa bei ambayo wameuziwa na wale mawakala kwa sababu wao wanafanya bei yao na wanapanga bei ambayo wanakutana mahali wanaungana, wakishaungana wanapanga bei.

Sasa kila watakapogusa ni bei ileile. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali pia nayo iangalie masuala haya kwa kweli ili viwanda visiweze kufa.

Lingine ni kuhusu kiwanda cha kuchambulia tumbaku, sasa hivi kiko Morogoro na tumbaku inatoka Tabora. Basi angalau kuwe na *center*, muwashauri wawekezaji waje wajenge kiwanda ambacho kitachambua tumbaku kwa Mkoa wa Tabora ili na Mikoa ya jirani iweze kupeleka pale angalau na watu wetu wapate ajira. Tumbaku inalimwa Tabora lakini wanaofaidika na ajira ni watu wa Morogoro huko kwa akina Mheshimiwa Semindu Pawa, hivi inawezekana? Kwa hiyo, ni vizuri na sisi tuangaliwe kuwekewa kiwanda naomba uwasiliane na Waziri wa Viwanda na Biashara hili suala lifikiriwe jinsi gani ya kuweka kinu cha kuchambulia tumbaku katika Mkoa wa Tabora. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba pia nichangie upande wa masoko Vikundi vya Ushirika vya Akina Mama. Mheshimiwa Waziri tuna tatizo kubwa sana la soko la bidhaa za Akina Mama. Wakati nachangia Wizara ya Viwanda na Biashara nilizingumzia soko la Akina Mama bidhaa zao, wamehamasishwa, wamejitokeza, wamekopa mikopo wakajiingiza kwenye elimu ya kusindika mazao yao.

Kilichotokea ni kwamba, wamesindika mazao yao na bado wanaambiwa wayapeleke *TBS*. Hivi mnataka kuniambia kweli mwanamke wa Tabora atakwenda kupeleka mazao yake *TBS* wakati tayari ameshakopa? Je, Wizara ya Ushirika na Masoko inasaidiaje kutafuta masoko ya uhakika na kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyowagusa wananchi ambavyo ni mahusiano baina ya uelewa wa hiyo *TBS* na Wizara ya Ushirika na Masoko? Akina mama kwa kweli wanakwama na vinginevyo watafungwa kwa

sababu ya mikopo wametumia fedha zao nyingi. Sasa wataachika kwa waume zao kwa sababu ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko atusaidie hilo kuhakikisha kwamba anafanya mawasiliano baina ya *TBS* na akina mama ili iwe rahisi kwa wataalam wake kushuka kule chini kutoa elimu kuhusu maana ya *TBS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna hizi *SACCOS*. Akinamama wameanzisha *SACCOS* zao nyingi hapa nchini na wameshaelewa maana ya *SACCOS*. Sasa litakuja tatizo lile lile kuhusu soko na hapo ndiyo penye tatizo. Naomba Wizara ya Ushirika na Masoko ijithadi sana kutafuta masoko. Mheshimiwa George Kahama tunakuomba kabla hujaondoka hebu watafutie masoko hayo akinamama ili waweze kupata masoko ya kuza bidhaa zao. Hilo ndilo ninaloliomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie kuhakikisha kwamba elimu ya masoko inatolewa na pia kupata soko la uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende haraka haraka kuhusu suala la pembejeo. Pembejeo zilikuwa zinatolewa kuitia Wizara ya Kilimo na Chakula. Wizara ya Kilimo na Chakula wanapopata pembejeo, wao wanapitia Vyama vya Ushirika, lakini kuna Mikoa mingine haina Vyama vya Ushirika. Kwa nini Wizara ya Ushirika na Masoko isisaidie kusambaza na kwa nini wasitumie *SACCOS* kusambaza zile pembejeo na kwa nini wasizipeleke kwa wafanyabiashara wakubwa wakubwa hata Tabora tunao wafanyabiashara ambao wanaweza kusambaza pembejeo za aina yoyote za kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri wa Ushirika na Masoko hebu awasiliane na Waziri wa Kilimo na Chakula ili hili suala liingie kwake. Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko ndiye mwenye watu kule kwenye Ushirika na hata *WETCO* inaweza kusambaza pembejeo katika Mkoa mzima.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba kwamba wataalamu watusaidie masuala mazima ya kuvikopesha Vyama vya Ushirika. Ingawaje matumaini makubwa kwa wananchi kuhusu Vyama vya Ushirika yamepungua kutokana na ubadhirifu uliokuwepo, sasa ili kwenda sambamba viwezeshe Vyama vya Ushirika ili angalau wananchi wengi waweze kujiunga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa bidhaa, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko una wataalamu wako. Nilikuwa naomba hao wataalam bado waendelee kutafuta soko kwa kutumia *Internet* au njia yoyote ili wanapokwenda kujadiliana na wanunuzi hao wa soko huria waweze kukubaliana bei ili wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Vyama vya Ushirika ambapo kuna wananchi wengi ambao walijiunga na Vyama vya Ushirika, lakini Vyama vyao vya Ushirika viliingia kwenye ubadhirifu: Je, Serikali inafikiriaje kuwafidia angalau kwa kuwakopesha hao watu maalum ambao walifilisika kutokana na ubadhirifu ambao ni tatizo? Naomba

Serikali nayo iangalie hata kwa kuwakopesha tena ili angalau hao watu waliopatwa na joto hili angalau waweze kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzungumza haraka haraka naona muda wangu unaniishia, nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Sina tatizo nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine niungane na wenzangu kwa kukuomba uangalie muda wako na uangalie mambo yako, utuingize kwenye jengo jipya la Bunge. Angalau tunakuomba uendelee kukalia hicho Kiti. Tunaomba dakika ya mwisho atakapokuja Mheshimiwa Rais tarehe 29 Julai, 2005 usitamke kwamba umefikia wakati wa kustaafuli, tunakuomba umezee usitamke chochote. Sisi hapa wapiga debe wako tupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii tena asilimia mia kwa mia. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Sir George Kahama na aendeleee kumtunza dada yangu na ninakutakia afya njema na kwako nitaingia usiku na mchana bila kuwa na wasiwasi. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha mchana. Wasemaji wote waliojiandikisha kuchangia hoja hii wamebaki wawili tu watapata nafasi katika kipindi cha jioni nao ni Mheshimiwa Henry Shekiffu na Mheshimiwa Jackson Makwetta. Baada ya hapo watoa hoja watahitimisha hoja yao. Basi baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipatia tena nafasi hii kuchangia wa kwanza wakati huu wa jioni.

Awali ya yote, nianze kwa kweli kumpongeza sana Waziri wa Ushirika na Masoko, kaka yetu Kahama. Mimi kwa kweli sioni kitu kinachonistua kwake katika kuandika hotuba hii nzuri. Uwezo anao, nia anayo na mimi nina uhakika alichokifanya si kigeni.

Kwa bahati nzuri mimi nimefanya kazi naye Dodoma hapa akiwa Mkurugenzi wa *CDA* na mimi nikiwa Meneja Mkuu Kampuni ya Biashara ya Mkoa.

Kwa bahati nzuri nilifanya naye kazi kwa karibu kwa sababu mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo inayohusika na uchumi hasa katika kuangalia *impact area* itaboreshwaje ili iweze kuilea Dodoma. Tulifanya kazi nzuri na mipango yake mpaka leo inaonekana na kuondoka kwake Dodoma tukubali tusikubali kumeleta pengo kubwa sana kwa kukua kwa *CDA*. Hata hivyo, kwa sababu alipewa majukumu tena mazito kama haya, basi si vibaya kumpa heshima na kumwambia kwamba tunamshukuru kwa kazi nzuri na utaendelea kutushauri. (*Makofi*)

Ndugu yangu Chibulunje, Msaidizi wake namfahamu vizuri kwa sababu wote tumekulia katika Ushirika, pengine kwa wale wenzangu walioko kule wanawenza wakashangaa hivi huyu ni Bwana Ushirika? Mimi niliacha Ushirika mwaka 1973 baada ya kuingia *STC*. Lakini mlezi wa kwanza kwangu ilikuwa ni Ushirika. Mimi ni mwanzilishi wa *SCCULT* Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mikopo, tulisaidiana kuianzisha na ndiye niliyefungua Kanda zote za Bukoba, Kigoma, Moshi na Dar es Salaam. Namshukuru Mungu na leo pengine nitachangia kidogo katika eneo hili la Ushirika.

Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara hii kwa sababu wameanza hivi juzi juzi lakini wameonyesha matokeo mazuri hasa ya kuandaa jinsi Wizara itakavyokwenda. Kwa kweli tukubali tusikubali inawezekana Wizara hii tusione yale waliyoyafanya kwa sasa, lakini maandalizi ya msingi mzuri ni ujenzi wa nyumba bora. Ukianza vibaya haraka haraka nyumba hiyo haitadumu. Kwa hiyo, nawashukuru sana na kweli ushahidi ni kitabu hiki.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia katika ukurasa wa 84 ambaa unazungumzia suala la maendeleo ya masoko na kifungu cha nane kwa kweli ningekizungumzia kidogo na kukazania. Suala la uanzishaji au tathmini ya kuanzisha ujenzi wa soko la mboga mboga na matunda katika Mji mdogo wa Segera hasa kwa ajili ya Mikoa ya Kaskazini ni jambo muhimu sana. Sisi wa Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro na hasa nikizungumzia Mkoa wa Tanga, tunapozungumza Tanga maendeleo yake yataletwa tu na mazao mawili.

Kudidimia kwa uchumi wa Mkoa Tanga sasa hivi ni kutokana na kushuka kwa zao la katani. Katani ilivyoshuka bei katika Soko la Dunia na vile vile uzalishaji uliposhuka Mkoa wa Tanga umepoteza umaarufu wake. Lakini mhimili mwingine wa Mkoa wa Tanga ni mboga mboga na matunda. Hakuna kitu kitawenza kuusaidia Mkoa wa Tanga hasa maeneo ya milimani kama vile Lushoto, Korogwe, Amani bila kuhimiza uuzaaji na uzalishaji wa matunda na mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Kenya inatumia kilimo cha *horticulture* asilimia zaidi ya 10 ya mapato ya fedha za kigeni kwani nchi ya Kenya inatokana na mazao ya matunda, mbogamboga pamoja na maua. Kenya haina ardhi nzuri kama iliyopo Tanzania, lakini wenzetu wameweza kufikia hapo. Ninapozungumzia fedha za kigeni kwa Kenya tunazungumzia kiasi kikubwa sana kwa asilimia 10 au 15 ni fungu kubwa sana. Sasa mimi nashauri na nahimiza kwamba tathmini ambayo Waziri ameisema ifanyike mapema na iweze kuhakikisha kwamba inaikaribia na kusaidia maeneo ya Mkoa wa Tanga hasa Lushoto, Korogwe na Muheza.

Tunapozungumzia matunda na hasa alivyozungumzia *contract farming* hapa ndio ningependa nitoe ushauri. *Contract farming* kwa kweli ni jambo geni katika nchi yetu. *Contract farming* inataka uaminifu, mtaji na utaalamu. Sasa unapozungumzia tathmini ifanyike kwanza, lazima tuangalie wakulima wetu wataingiaje katika Mikataba ili wazalishe mazao ambayo yataweza kumudu mahitaji ya soko la kigeni. Watakuwaje

waaminifu katika kukubaliana na Mikataba itakayowekwa. Haya mambo yanahitaji sana utafiti na mambo haya yanahitaji Serikali ijiingize na isaidie.

Ni ukweli kwamba wenzetu wa Kenya wameweza kufaulu sana kwa kilimo cha maua kwa sababu wao wameweza kusaidiwa na Serikali. Serikali kutafuta wawekezaji ziko Benki ambazo zilitoa mikopo na mpaka leo Kenya inasamehewa kodi. Ukipeleka mazao yako katika soko la Ulaya unasamehewa *almost* asilimia nane ya *duty*. Sisi Tanzania mwaka 2008 tutaingia katika mpango huo kwamba tutakopopeleka maua katika nchi hizi za Ulaya tutasamehewa.

Mheshimiwa Spika, sasa tumejiandaa vipi ili tuchukue *advantage* ya soko hili? Kwa bahati mbaya mara nyingi sisi ni watu wa kuchelewa. Kwa hiyo, mimi nahimiza na naomba sana tathmini ifanyike kabla ya mwaka huo 2008 maua yawe ni zao moja kubwa linaloleta fedha za kigeni hapa nchini. Matunda pamoja na mboga mboga kwa kuza nchi za Ulaya soko lipo tatizo kubwa ni *quality*. *Quality* yetu haiwezi kushindana katika Soko la Dunia. Sasa tufanye nini ili wananchi wetu waweze kulima *quality fruits, quality vegetables*? Hapo ndio tutapata jibu la kuza nchi za nje. Huwezi ukabeba leo matunda yamejaa michubuko upeleke ukauze Ulaya, sio rahisi. Kwa hiyo, naomba sana katika utaratibu wa *contract farming* na *fruit processing* ni eneo moja muhimu sana. Tunaweza kabisa kuza yakiwa *raw* na pia vile vile tunaweza *ku-process*. Nasikia huko mpango mkubwa, sina uhakika wa kujenga kiwanda kikubwa sana cha kutengeneza matunda Kibaha, lakini nasema haya yote yanahitaji msukumo wa Serikali. Mimi nimeona nisisitize hili kwa sababu ni muhimu sana katika eneo langu na naamini kabisa kama likitiliwa mkazo tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nichangie maeneo mengine. Mimi kama nilivyosema nimeanza katika Vyama vya Akiba na Mikopo. Vyama vya Akiba na Mikopo kwa sasa vimekwishakomaa na kuonekana ndio mkombozi wa wananchi huko Vijijini. Hizi ndio Benki ambazo wananchi wanazichangia wenyewe na zinafanya kazi nzuri. Hapa nichukue nafasi kuipongeza *SCCULT*. *SCCULT* imefanya kazi nzuri kuchukua mikopo na kuvikopesha Vyama vidogo. Sasa hii ni hatua ya kwanza, lakini sasa twende katika hatua ya pili kuunda *SACCOS* ndogo ambazo ndio Benki.

Kwa bahati nzuri wakati nikiwa *SCCULT* tulikwenda kutembelea Ujerumani na tulikwenda kuziona *Reinfencen Banks*. Hizi *Reinforcing Banks* ni Benki ambazo kila kitu kipo. Ukitaka mbolea utaipata pale, fedha zako utazipata pale, ukitaka kuza mazao yako minada iko mle mle, unachukua fedha upande huu unaingiza unakwenda kwenye mnada unanunua kitu unachotaka.

Mimi nina uhakika tukiamua kufanya vizuri zaidi ya hapa tulipo, tumekwishaiva kufikia hatua hiyo. Ziko *SACCOS* ambazo leo zinaweza kuwa Benki Ndogo. Sasa ni juu ya Serikali kuzifanya hizi kweli ziwe Benki Ndogo. Maana huwezi ukakwepa wajibu, Serikali lazima isijitoe. Kwanza watu wetu wanahitaji utaalam, wanahitaji nyenzo na msukumo na elimu ya kutosha kuendesha hizi *SACCOS* ili ziwe ni Benki ndogo. Kwa hiyo, nashauri sana kwamba Serikali isaidie Vyama vya Akiba na Mikopo na tuanze sasa Benki ndogo ndogo Vijijini ambazo kwa kweli zinaanzishwa na *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningeomba nichangie kwa haraka haraka ni umuhimu wa Serikali kulea ushirika. Mimi nakubali kwamba Serikali au Wizara ilikuwa katika kujiweka sawa ili sasa tusaidie Ushirika. Pengine nisisitize hapa kwamba ninaomba mambo matatu yafuatayo ili yafanywe na Wizara. Kwanza ni lazima Wizara ijenge uwezo mkuu wa Ushirika. Halafu ni muhimu sana Wizara ijenge *capacity* ya uongozi. Wenzangu wengi wamechangia udhaifu ulioko katika uongozi wa Vyama vyetu vya Ushirika. Lakini vile vile, pamoja na kwamba mitaji imetajwa humu mitaji inayotajwa sio mikubwa ya kutosha kuendesha Ushirika kuwa ni mshindani mkubwa wa soko huria. Maana bila ya kuwa na Ushirika wenye nguvu soko huria litanyonya tu wananchi, tupende tusipende. Tukitamka tu kwa maneno bila kuweka mikakati, nina uhakika tutashindwa.

Sasa kwa upande wa Ushirika, kwa upande wa watumishi, zamani tulikuwa na chombo kinachoitwa Ujima. Ujima ilikuwa inashughulikia wataalamu na watumishi katika Vyama vya Ushirika. Mimi nashauri ikiwezekana kwa kweli tujenge *think tank* ya Vyama vya Ushirika na ikiwezekana *Commission* ya Vyama vya Ushirika irejeshwe. Pale pawepo na utaalamu wa kulea na kukuza na kuwaelimisha watu wetu wa Ushirika. Bila hiyo bado tutaendelea kulaumiana.

Ni kweli asubuhi kuna aliyezungumza kwa uchungu sana. Unapozungumza *internet*, huko Vijijini yako matatizo makubwa sana. Kuwaambia Kijiji au Chama cha Ushirika kilichoko Lushoto kijue bei ya kahawa ya dunia sio rahisi. Ni lazima tujenge uwezo wa kuweza kuwawezesha wataalamu wetu tulionao. Aidha, tujenge *centre* ya Ushirika ambayo ni *Information Centre*, ukifika pale unazijua bei zote. Pale ndio mahali ambapo wanaushirika wanakaa wanabadilishana mawazo. *CUT* ilijengwa kwa fedha za wakulima, lakini lile jengo mpaka leo mimi siamini halitumiki inavyotakiwa. Bado kwa kweli heshima ya wakulima pale haijaonekana. *CUT* imejengwa kwa fedha nydingi sana na ndio kitega uchumi cha kwanza cha Vyama vya Ushirika. Lakini bado hapajakuwa kama mahali pa kujifunzia Ushirika, kama mahali pa kubadilishana mawazo ya Ushirika.

Kwa hiyo, kwa kweli tujenge Ushirika *Centre* mahali ambapo *information* zote za Ushirika utazipata. Maelezo yoyote ya Ushirika utayapata na pia vile vile kuunganisha na soko la ulimwengu ili unapofika pale unatafuta bei hata kwa kupiga simu. Siku hizi simu zipo unapiga kutoka Lushoto unazungumza na *Centre* wanakwambia bei sasa hivi ya kahawa duniani ni hii. Sasa hata kama wanaushirika wanataka kuuza kesho wanapanda gari wanakuja Dar es Salaam wana *process export* yao. Lakini sasa hivi wako kule Vijijini tunasema tu kuna *Internet*, haya mambo hayatawasaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwamba tuwe na Wizara moja inayohusika na Bodi za Mazao na Bodi za Masoko. Hivi leo tunazo Bodi ziko kilimo. Hizi Bodi za Mazao Mchanganyiko bado hazijaundwa, leo tunazungumzia uuzaji wa mbogamboga, hatujui nani atatusaidia. Sasa mimi nashauri Wizara hii kwa sababu inahusika na masoko, ipewe jukumu la masoko. Sio rahisi kwenda mtu mwagine, Waziri mwagine umpe maelekezo, inawezekana akakataa. Asipotekeleza, unamchukulia hatua gani na hayuko chini yako?

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali inayokuja iliangalie hili. Ushirika ni chombo muhimu sana. Sasa suala la masoko lijengewe katika Wizara hii ili tunapozungumzia soko la kitu chochote Wizara iko tayari kueleza na tuilaumu kwa ukweli. Sio leo Keenja anahuksika huku unakwenda kwa Kahama, unamwambia sijui mbegu zimekuja mbaya, huyu amwulize nani; haya hatujapata tumechelewa kuagiza. Mbolea iko kwa Keenja, Masoko yako kwa Kahama hii ni *ku-confuse*. Kwa hiyo, mimi nashauri Wizara hii moja ishughulike na mambo yote ya masoko. Ikiwezekana Mashirika yote yanayohusika na *export* yawekwe huko. *Board of External Trade* na kadhalika yote yaende kule yakapeane utaalamu na tuuze kile kinachowezekana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivi, mimi napenda kumpongeza kaka yangu na namtakia kila la kheri katika kustaafu kwake. Naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sikutegemea kuitwa. Ningependa niungane na wenzangu walionitangulia kwa kusisitiza mambo yafuatayo:-

Moja, haja ya kuunganisha Masoko na Wizara hii. Hali ilivyo sasa hivi inazua utata na *confusion* na hata ni kinyume cha jina la Wizara yenye. Wizara hii ni Wizara ya Ushirika na Masoko, lakini masoko yako mahali pengine na kamusi ya Ushirika katika nchi hii ni pamoja na ndugu yangu George Kahama amefanya kazi nzuri sana, ni kamusi ya Ushirika katika nchi hii pamoja na Hayati Bomani. Leo tunazungumzia Ushirika wakati Ndugu George Kahama anang'atuka katika uongozi wa Ubunge.

La pili, ubora wa mazao baada ya kuruhusu uchumi wa Soko, kwa kweli kuna tatizo kubwa sana kwa zao la pamba na chai. Chai kwa kawaida unachuma majani mawili, sasa hivi hata sita unaruhusiwa kuchuma na kwa kuchuma sita unachelewesha kuota kwa majani mengine. Kwa sababu ya mashindano, hakuna anayekataa majani sita basi wamehalalisha uchumaji wa majani sita ya chai na ubora wa chai katika nchi yetu unazidi kudidimia na hivyo kuzidi kukosa fedha za kigeni.

Nashauri suala hili litazamwe ili kurudisha hadhi ya nchi yetu na vile vile wakulima waweze kupata faida ya mazao haya. Maadamu kuna wanunuzi wa chai bila kujali ubora maana wengine hawajui chai bora ni chai gani mradi ni chai ina rangi ya kijani tu. Kwa sababu hawajui hilo, basi wanenanua mradi inaitwa chai wanenanua tu. Lakini ubora wa chai uko hatarini na jina la nchi yetu linazidi kuchafuka na ndivyo ilivyo kwa pamba, korosho na sijui tutafanyaje kwa sababu wakulima wa kawaida kwa nini uhangaike na ubora wakati kuna mnunuzi wa mazao yao?

La tatu, naishukuru Wizara imeamua kujenga masoko ya mazao. Msingi wa Ushirika ili uweze kudumishwa ni kuwa na masoko kama haya ya Kibaigwa. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa Wizara yake kuamua kujenga soko la mazao mchanganyiko pale Makambako. Makambako ni *centre* ya Nyanda za Juu za Kusini ya mawasiliano kwa maana kwamba ni *halfway* kwenda Songea, Mbeya, Iringa na

Kilombero. Hata hivi sasa ukienda Makambako kuna wafanyabiashara kutoka Zambia, Congo, Kenya, Zanzibar, Dar es Salaam na Malawi wako pale lakini hakuna soko, wanunua mazao kwenye sakafu tu. Hakuna soko pale.

Kwa hiyo, uamuzi wa kujenga soko la mazao mchanganyiko pale ni uamuzi wa busara na ningependa kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Njombe na wakazi wa Nyanda za Juu za Kusini kukushukuru sana kwa mtazamo huo wa mbali na kuamua kujenga soko la mazao. (*Makofi*)

Nne, suala hili la ubora wa mazao la kila aina nadhani kwa dunia inavyokwenda sasa hivi tusipoangalia tutakwama. Ni jambo sio la aibu, lakini nadhani tunakosa maneno kwamba leo nyama ya ng'ombe inatoka Botswana, nyanya zinatoka Malawi, matunda yanatoka *South Africa*, maziwa yanatoka Zimbabwe, mchele unatoka Thailand, sasa sisi tutauza kitu gani? Nyama wanasema hawa ng'ombe wetu wamekondeana wana magonjwa. Nyanya wanasema zina madawa ya madukani, kwa hiyo, yanaharibu afya za watu.

Kwa hiyo, kitu gani cha Watanzania kitanunuliwa na mahoteli yetu? Hakuna! Kwa hiyo, mwelekeo huu unavyokwenda ni kwamba itafikia wakati Watanzania watakuwa wanlishwa tu mazao kutoka nje na watabaki wamekaa tu wanlishwa kama nguruwe. Kwamba mazao, nyanya kutoka nje, mchicha kutoka nje, pilipili kutoka nje nyama kutoka nje, kila kitu kutoka nje. Sasa nchi ya kilimo, bila ya kilimo kwa sababu ya *quality* tunahitaji washauri kwa wakulima hawa. Kama alivyosema ndugu yangu Shekiffu pale, kumfikiria mkulima wa kawaida baadhi ya mambo haya nadhani tuko mbali. Wenzetu mipakani na nchi fulani kuna washauri wa uchumi kabisa wanaosema leo fedha ya nchi yetu na ya nchi hii iko hivi, uzeni zao hivi. Watu wa kwetu wanababaika tu, ni *deliberate!* Ni mkakati uliojengwa na watu kuchota mali kutoka nchi ya jirani. Sisi tunadhani mkulima, mfanyabiashara wetu yule ataendelea hivi hivi hakwenda Shule, wanamdaganya kiasi gani auze, hakuna.

Mheshimiwa Spika, machungwa ya Tanga yanauzwa nchi jirani kwa majina ya kwao. Mbao za kutoka Njombe zile nimekwenda, mimi juzi Dubai zimewekwa mhuri nchi fulani wakati zinasombwa kutoka Njombe na kule Njombe tunauza tu hazina alama wala nini zinapelekwa tu lakini yeye anabandika alama kuonekana kama zinatoka nchi ya kwao. Hii nchi sijui ni kwa nini?! Yaani ni kama haina mwenyewe! Watu wanafanya kazi lakini wanazidi kukonda tu, watu wa jirani wanazidi kunenepa wakati hawazalishi mazao hayo. Machingwa, mbao, nyama kila kitu hata mabucha, ng'ombe wanategemea kutoka kwa Wamasai wa Tanzania. *This country, cry my beloved country.* Nadhani nimeeleweka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Wizara hii iliyohasisiwa na Mheshimiwa Sir George Kahama, Naibu wake Hezekiah N. Chibulunje, Katibu Mkuu wake Dr. Ladislaus Komba, umeonyesha mwelekeo mzuri. Kwa misingi hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekwisha tamka rasmi kuwa hatagombea, binafsi nampongeza kwa uamuzi wake, naamini kama angeomba tena kugombea Ubunge Jimboni kwake angeshinda kwa ushindi wa tsunami.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akamilishe n'ngwe yake kwa kutembelea Mbinga na kuwapa matumaini wakulima wa kahawa wa Mbinga, kwamba ombi lao la kurejeshewa mali yao iliyokuwa *MBICU* na ambayo iko chini ya mafilisi. Kiwango cha uharibifu wa raslimali hizi inatisha hasa kwa kukosa usimamizi mzuri. Tunasubiri sana maamuzi ya busara kutoka kwa mheshimiwa Waziri.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza sana kwa hotuba yako nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yako.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

- (i) Kwa kuwa Serikali iliahidi kuunda Bodi itakayoshughulikia mazao mchanganyiko kama vile karanga, alizeti, ufuta, mahindi na kadhalika; Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?
- (ii) Je, Serikali itasaidia vipi ili Mkoa wa Dodoma uunde Chama Kikuu cha Ushirika ambacho kitasaidia wananchi wa Mkoa wa Dodoma (Soko la uhakika kuinua kipato cha mwananchi wa Dodoma)?
- (iii) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi na vitendea kazi vya watumishi wa Wizara ya Ushirika na Masoko ambao wapo katika Halmashauri za Wilaya pamoja na kuwaelekeza kitaaluma ili kuboresha utendaji wao wa kazi.
- (iv) Je, Mkoa wa Dodoma umeunda Vyama vya Ushirika vya msingi vingapi na pia *SACCOS* ngapi? Je, Vyama hivyo havitoshi kuunda Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Dodoma?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *DAP*, Wakurugenzi wote, Wakuu wa Idara wote na *officials* kwa kazi nzuri ambayo matokeo yake yanaridhisha sana, kwanza kwa kuhamia Dodoma; pili, kuweka chombo cha ukaguzi *COASCO* na tatu, kuwa pamoja na Kamati ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Masoko, hivi Wizara inayo habari kuwa soko huria ni shetani? Kuna Walanguzi wanaojitokeza kununua ufuta Morogoro debe Sh. 3,000/= tu. Huu ni unyonyaji kweli. Naomba utoe tamko wakome kunyonya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Masoko ya Mfano wa Kuigwa, kuna masoko ya kisasa yalijengwa kama vile Kibaigwa, Tawa, Tandai - Kinole na Nyandisa. Masoko haya yamekamilika na mengine yamefunguliwa bado ufunguzi wa soko la Tawa Jimbo la Kusini na Tandai – Kinole Jimbo la Kusini Mashariki. Je, lini tutafungua masoko hayo? Naomba upange ili baada ya kura za maoni tufungue masoko haya mawili.

Mheshimiwa Spika, hivi kuna Vyama vingapi vyta Ushirika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Kagera na Morogoro?

Taratibu zifi zifuatwe ili wananchi waitwe wanaushirika? Hivi kwa nini wananchi wengi hupenda kujunga kuwa wana vikundi kuliko kuwa wanaushirika? Wanaogopa nini? Ushirika kukimbilia kikundi zaidi, kulikoni?

Madai ya malipo ya pili ya pamba, hivi sasa pamba inapambanisha balada la kumpamba mkulima. Mamlaka ya mazao, naomba sana mamlaka hizi ziwe chini ya Wizara hii badala ya kuwa kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, Maombi Maalum, naomba kujengewa masoko ya kisasa katika maeneo ya Mikese, Ngerengere, Kiloka na Mkuyuni.

Mheshimiwa Spika, shukrani.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Uongozi mzima wa Wizara, siyo tu kuna hotuba nzuri na ya kusisimua, bali pia kwa utekelezaji mzima wa kufufua Ushirika nchini. Kabla ya mwaka 2000 Ushirika ulikuwa umekufa kabisa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba Watanzania wanakuwa maskini zaidi kati ya miaka ya 1980 hadi leo kwa sababu wakulima walinyang'anywa haki ya kudai bei za mazao, kuwa na Mikutano na kuwakilishwa Serikalini. Wakulima kutokana na hali hiyo, walikata tamaa ya kulima hasa kulima mazao ya biashara. Walitembelea katika biashara ndogo, ulipofika wakati Serikali ikaleta sera ya Soko Huria mambo yalimwagika zaidi kwa vile wanunuvi binafsi walinyonya wakulima kwa kujipangia bei na kukopa mazao ya wakulima na wasilipe. Kwanza Kipato cha mfukoni kilipotea; pili, Vyama vyta Ushirika vilikufa; tatu, mashamba ya kahawa, katani, chai yaliendelea kuharibika; nne, Mazao ya pamba,

tumbaku na katani yalikoma kulimwa sana na Vyama na tano, hata watumishi wa Sekta hii walitokomea mistuni.

Mheshimiwa Spika, ili Ushirika uimarike na masoko yafufuke Serikali inahitaji kufanya yafuatayo:-

- (i) Kupata watumishi wenye ujuzi wa dhana ya Ushirika;
- (ii) Kuhamisha watumishi waliobaki kazini waondoke katika Vituo walimokaa kwa miaka mingei. Afisa Utumishi wa Wilaya ya Ngara amekaa kwa takribani miaka 20. Ushirika unazidi kuditidimia, wizi katika Ushirika umekithiri ambavyo nimelalamikia hili kwa miaka yote;
- (iii) Wanunuzi wa mazao binafsi wapate vibali kutoka Wilaya na Mikoa inayohusika badala ya Wizarani;
- (iv) Wizara za Ushirika na Masoko na Wizara ya Kilimo na Chakula zishirikiane kutambua mazao yatakayosaidia kujenga upya Ushirika nchini;
- (v) Wizara hii iunde kitengo cha *Marketing* kwa ndani na nje ya nchi, pia kutangaza mazao yaliyo nchini ambayo hayafahamiki huko nje;
- (vi) Vyama vya Ushirika vinunue aina nyingi au zote ili iwe motisha kwa wakulima kulima mazao ya aina nyingi. Natoa mfano wa Wilaya ya Ngara ambayo inalima aina nyingi za mazao ya nafaka, lakini Ushirika unanunua kahawa peke yake. Hali hii iko katika nchi nzima na inazuia bidii kwa wakulima, vile mazao mengi huharibika baada ya mahitaji halisi ya wakulima.
- (vii) Wizara ya Ushirika na Masoko ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzisha viwanda sehemu nyingi nchini vya kuzindika mazao. Utamaduni wa Wizara hii ni kununua nafaka na mazao ya biashara peke yake ikasahau mazao ya mboga na matunda.

Mheshimiwa Spika, Bodi za Mazao zinafanya kazi kwa utata mkubwa. Kwa nini ziwekwe chini ya uongozi wa Wizara hii badala ya ile ya kilimo na chakula? Lazima wageni kuendeleza sera na mipango yao. Bodi zina vifaa haba vya kutendea kazi. Wakulima wanazilea Bodi, Watendaji Wakuu wa Bodi hizo hawatembelei sana maeneo ya wakulima na Vyama vya Ushirika ambavyo ndiyo vinatoa mazao kwa Bodi. Mahusiano kati ya Bodi na Ushirika sasa yaimarishwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa wakulima wa zao la korosho wapo katika kipindi muhimu cha kilimo hicho. Wakulima wako kwenye palizi

za mashamba yao, upulizaji wa dawa za mikorosho ili wapate mavuno mazuri miezi michache ijayo. Lakini hadi sasa wakulima wa korosho hawajaelezwa bei ya zao hilo mwaka huu itakuwaje. Ni muhimu kilimo chetu kikawa cha kibiashara zaidi kwa maana bei kama za korosho ni vizuri wananchi wakaelezwa mapema kabisa ili iwe motisha kwa wakulima hao kuongeza bidii katika kilimo chao. Bei ya zao ni kichocheo kikubwa kwa wananchi kupalilia mashamba yao na kuhakikisha kuwa madawa ya kupulizia mikorosho yanapatikana mapema.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida wakati wa msimu wa korosho ununuzi wa zao hilo unachelewa kuanza katika maeneo mengine hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi ambao hulazimika kwenda maeneo ya mbali kuuza korosho zao. Wanunuzi wasambae katika Vijiji vyote vyenye korosho ili wananchi wasilazimike kwenda mbali kuuza korosho zao na kupata gharama kubwa za usafirishaji.

Ni vizuri Serikali ikasimamia kikamilifu zoezi la ununuzi wa korosho ili kuondoa kero zinazowapata wakulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo niseme tu kuwa naunga mkono hoja hii moja kwa moja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo yangu, ningependa kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Sir George Kahama na Naibu wake Mheshimiwa Chibulunje wakisaidiana na Katibu Mkuu wao, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote cha miaka mitano ya kufufua Ushirika na kuimarisha dhana nzima ya masoko kwa ajili ya mazao mbalimbali. Naunga mkono hoja hii kwa kila hali.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Wizara ione namna ya kusaidia Mkoa wa Rukwa katika kuwa na masoko makubwa ya mazao ya mahindi/maharage kwenye mipaka yetu na nchi jirani, mfano Kasesya (Mpakanji kati yetu na Zambia). Hii itasaidia kuwa na ushindani mkubwa wa bei kwa mkulima kuwa nzuri na za haki kwa wote watakaokuwepo kwenye masoko hayo. Kibaigwa ni mfano mzuri wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ushirika nao waliopo Wilayani ni budi wapatiwe mwongozo wa utendaji wa kazi zao kutoka *Centre* kwani wengi wao hawafanyi kazi zinazostahili bali hupachikwa kazi zozote zile ambazo Halmashauri zenyewe zinaona zinafa. Ni budi kuundwe Kamati ya Uchunguzi toka Wizarani wakishirikiana na Chuo chetu Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi ili watoe ushauri wa jinsi ya kuratibu utendaji kazi wa Maafisa wetu chini ya mfumo na sera hii.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini baadhi ya wafanyabiashara binafsi wa mazao yetu huwa wanakaidi kutekeleza maagizo ya Serikali? Hivi sababu huwa zipi wakati Serikali kuitia Wizara hii inapotoa maelekezo lakini kunakuwa hakuna wanachokifanya. Serikali huwachukulia hatua zipi? Tukichukua mfano wa bei ya pamba mwaka 2003, kutakiwa ifidiwe na Makampuni lakini bila kufidiwa au wanapoelekezwa wanunue mazao kwenye magilio, lakini wanafuata kwenye majumba ya watu.

Mheshimiwa Spika, je, mpango wa kuwa na *Crop Stabilization Fund* kwa ajili ya mazao yote makuu ya biashara, inaendeleaje au ina ugumu gani kutekelezwa? Ni vizuri likaelekezwa ili baadaye lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nini jitihada za Wizara katika kuwapatia maslahi bora watumishi wa Ushirika ili iwe chachu ya maendeleo endelevu ya Ushirika sasa na mbele ya safari?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na naunga mkono. Hata hivyo, ningependa kutoa ushauri ufuatao:-

Kwanza, pamoja na kupongeza Wizara kwa ujenzi wa Soko la Mazao Kibaigwa, nashauri Wizara ikamilishe maandalizi ya ujenzi wa Soko Kuu la Makambako (eneo ramani, mchoro na ujenzi kwa awamu) mbona kimya?

Pili, Ushirika wa Kuweka na Kukopa ni muhimu kwa maendelo ya wananchi wetu, vipi Wizara ishirikiane kuhamisha Benki ya Ushirika nchini?

Tatu, nashauri kuwa ili kuleta maana mashirika ya masoko yaliyoko chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula yapelekwe Ushirika. Hali ya sasa inaleta (*confusion*) utata kwa wananchi.

Nne, ujenzi wa soko la Makambako ijulikane maandalizi yake.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi George C. Kahama, Mbunge na Waziri wa Ushirika na Masoko kwa hotuba yake nzuri sana na yenye uchambuzi wa kina ambayo ameitoa asubuhi hii ya leo. Kwa kipindi cha miaka mitano tumeshuhudia jitihada za hali ya juu za Wizara ambazo zimeleta msisimko na mabadiliko makubwa na mapinduzi ya hali ya juu katika nyanja ya Ushirika na Masoko. Hongera sana Mheshimiwa Balozi George C. Kahama pamoja na Naibu wako Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje kwa kazi nzuri sana ambayo mmekuwa mnaifanya.

Mheshimiwa Spika, Ushirika Duniani pote ndicho chombo cha kumkomboa mtu mnyonge. Kwa hili, hatuna *choice*, lazima Tanzania tupigane kufa na kupona kuhakikisha kuwa tunakuza Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kukumbushia malalamiko ya wanaushirika wa Siha Kyeyo *Cooperative Society* la kupewa fursa kuamua mambo yao wenyewe bila ya kuingiliwa au kusukumwa na mtu au kundi la watu. Ipo haja ya kuhakikisha kwamba uchaguzi unafanyika ili wanachama wawe na hakika na maamuzi wanayoyafanya. Aidha, wanachama wana haki ya kupata taarifa ya mapato na matumizi bila kucheleweshwa na mtu ye yote yule.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeahidi kwa muda mrefu kuingilia kati katika tatizo hili, lakini haijafanya hivyo. Naomba sana itekeleze ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, ninaitumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maafisa na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yao hii nzuri waliyoiwasilisha hapa Bungeni leo hii. Ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri inaeleza kuwa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 ni matokeo ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais ya kushauri juu ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana sera hii ya maendeleo ya Ushirika ambayo malengo yake makuu ni haya tuliyoelezwa kuwa ni ushauri juu ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana Wizara yetu hii pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kuwa sera hii inaleta mafanikio makubwa kama yalivyokusudiwa kwa maslahi ya Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa sera hii kutaiwezesha Wizara hii kutimiza malengo na majukumu yake iliyopangwiwa ambayo kwa kweli yanalenga kuleta maendeleo ya wananchi wa nchi hii pamoja na nchi kwa ujumla.

Kwa hiyo, ili kuweza kufikiwa malengo yaliyomo katika sera hii, hatuna budi wataalam wote wa Wizara hii wanaohusiana na masuala ya Ushirika waende kwa wananchi Wilayani na Vijiji kushirikiana nao katika kuleta maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa upande wa Serikali, ninaiomba kuwawezesha wataalam wake mbalimbali hapa nchini kwenda Vijiji kushirikiana na wananchi kwa kuwapatia uwezo wa kifedha na vifaa ili waweze kuwasaidia wanachama wa Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tuache maneno, sasa tufanya kazi. Nchi yetu inaweza kufanikisha yale yote ambayo yanalenga katika kutaka kuleta maendeleo katika Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama mambo haya ya kuwapeleka wataalam wa Ushirika Vijiji utafanikiwa kufanywa, basi utaiwezesha Wizara hii kutimiza malengo yake ya kutaka kuleta mabadiliko yanayolenga kutoa huduma kwa umma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 37 katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri unaeleza juu ya sera, sheria na mipango, pamoja na sera ya masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili linaleza kuwa, kwa muda mrefu sasa wakulima, wafanyabiashara na wasindikaji wanakabiliwa na matatizo mbalimbali katika shughuli za masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa kulielezea suala hili la kuwepo tatizo la soko la mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kuongeza juhudzi zake kipatia ufumbuzi tatizo hili la kutokuwepo kwa soko la mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la soko ndio msingi imara utakaowawezesha wakulima na wafanyabiashara wetu hapa nchini utakowawezesha kujipatia kipato na maendeleo. Kwa hiyo, tutumie nguvu, nyenzo na wataalam wetu mbalimbali kuweka mazingira ya upatikanaji wa soko la kuuza mazao ya wakulima na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, ninawatakia kila la kheri katika kutelekeza majukumu yenu Kiwizara na Kiserikali kwa faida na manufaa ya maendeleo ya nchi yetu na wananchi wote wa nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninarudia kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maafisa mbalimbali pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa Watanzania ili wananchi walio wengi wafaidike na mpango huu wa kujiunga na Vyama vya Ushirika. Ni vizuri Serikali ipite Vijijini iwafahamishe wananchi umuhimu wa kujiunga na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, wapo watu ambao wamejiunga na Vikundi vya Ushirika lakini baada ya kuanzisha Ushirika huo hatimaye vikundi hivyo haviendelei kwa ukosefu wa utsalam. Hivyo, ninaiomba Serikali kutoa mafunzo au Semina ili vikundi vya Ushirika viwe na uhai. Vilevile wawepo Wakaguzi wa kutosha katika Vikundi vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kutafuta masoko ya mazao yanayozalishwa, Serikali isimamie bidhaa inayozalishwa katika Vikundi vya Ushirika wapatiwe masoko ya kuza bidhaa zao. Kuwepo kwa Vikundi vya Ushirika inasaidia sana hasa wanapotokea Wahisani ambao wanataka kutoa misaada, inakuwa rahisi kutoa misaada kuliko kumsaidia mtu mmoja mmoja.

Baadhi ya wanaushirika hasa wale wanaoanzisha Ushirika mpya ninaomba wapatiwe mikopo kulingana na ukubwa wa ushirika huo. Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kujenga viwanda mbalimbali. Hii ni kutokana na baadhi ya wazalishaji wengi kukosa soko. Mfano zao la machungwa, hivi sasa limeongezeka lakini wakulima hawana soko la kuuzia machungwa. Hivyo, Vikundi vyta Ushirika wa Mashamba ya Michungwa hivi sasa wanajuta kuanzisha Ushirika huo. Mbali na zao la machungwa msimu huu wakulima na wanaushirika hawajui wauze bidhaa zao wapi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hojo hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. FESTU B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi na maarifa zilizojidhihirisha za kiutendaji kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Ushirika Mkoa wa Mwanza (Nyanza) hawakuruhusiwa kununua pamba msimu huu kwa sababu hawakuwalipa wakulima albaki ya bei ya pamba msimu uliopita. Kuna hatua gani zimechukuliwa juu ya hali hii kwa Nyanza na Wakulima?

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa kifedha katika Vyama vingi vyta Ushirika (*Financial Management Systems*) si wa kuridhisha. Inabidi wasimamiwe sana kama ilivyofanyika walipopewa na Serikali *guarantee* ambapo waliweza kulipa asilimia mia moja. Wakati wanasimamiwa juhudi za makusudi zifanywe *ku-strengthen cooperatives*. Mimi naamini kuwa bila Ushirika imara masoko yetu yatayumba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko ya mazao ya kilimo, juhudi zinafanyika kwenye upande wa uwekezaji nchini kwa ujumla umepelekea ongezeko la ufanisi katika masoko. Tanzania hivi sasa ina-*export* kuititia *Private Investors* kama *AZAM*, Mohamed *Enterprises* na kadhalika, mazao mbalimbali. Lakini haiingii sana akilini kwamba ili *AZAM* auze unga wa ngano nje inabidi a-*import* ngano kama *cereal* aisage halafu ndiyo a-*export*! Ni sawa kwake kwa sababu ngano anayonunua toka nje ni rahisi zaidi kuliko ya ndani. Kwa maoni yangu, inabidi kuwepo *backward and forward linkage* baina ya Wizara ya Ushirika na Masoko pamoja na ile ya Kilimo na Chakula ili ngano iweze kuzalishwa hapa nchini, isagwe/ikobolewe hapa nchini na hatimaye iwe *exported*.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuyatazama magilio huko Vijijini kwa umuhimu wa pekee kwa nia ya kuongeza ufanisi wake. *Rural markets* haziuzi tu mazao ya kilimo bali pia ni chombo muhimu sana katika kuchochea maendeleo Vijijini na Mijini pia. Wizara ya Ushirika na Masoko ni mbia kiongozi katika ku-*influence efficiency* ya utendaji kazi wa masoko Vijijini. Mbia mwingine muhimu ni TAMISEMI. Wizara hizi mibili zikae pamoja, hasa baada ya kuwepo taarifa za kiutafiti juu ya *performance of rural markets in Tanzania* ili kuyapatia ufumbuzi mambo ambayo yanasaababisha masoko ya Vijijini yasiwe na ufanisi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza tena na Mungu awabariki. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wataalam wote kwa kazi nzuri sana ya kusimamia kufufua Ushirika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini ningeomba nipaye maelezo au ufanuzi kwa masuala au maneno yafuatayo:-

Kuhusu mazao mchanganyiko ya chakula, wakulima wengi wa Taifa hili wanajihusisha na uzalishaji wa mazao mchanganyiko ya chakula. Kwa masikitiko makubwa Wizara haijaaelekeza nguvu zake, aidha kuunda Ushirika imara au kuwatafutia masoko ya kuridhisha kwa bei na mzunguko wa uwingi wa mazao. Baadala yake mara Serikali imetoa maagizo kuwabana wakulima hawa, aidha wasiuze mazao haya au wasiyauze mazao hayo nje ya nchi, hasa kwa Mikoa na Wilaya zilizopo mipakani. Hivi Serikali haioni kuwa mkulima wa mahindi, mpunga au maharage zao lake la biashara ni lile lile zao la chakula, ni sawa na mkulima wa pamba, kahawa, chai na kadhalika? Zao lake ni lile lile na sio lingine. Kwa nini mkulima wa mazao ya chakula abanwe na yule wa mazao ya biashara aachiwe huru?

Huu ni wakati wa soko huria, Serikali iache kuwaandama wakulima wa mazao ya chakula hata ikiwa kuna uwezekano wa kuzuka njaa au upungufu wa chakula nchini au sehemu ye yeyote ya nchi. Suala la majanga ya njaa na ukame kuendelea katika nchi yetu ni kwa sababu Serikali inaendelea kuwa na kigugumizi kuona umuhimu wa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo cha kumwagilia. Dunia ya leo hakuna nchi yenye sera safi za kilimo inaendelea kutegemea bahati za msimu wa mvua ila ni Tanzania inayokataa kugeuka.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inafahamika sana kuwa na uwingi wa mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, kuku na kadhalika. Jambo la kusikitisha sana ni kuwa bidhaa zinazotokana na mifugo yetu zina ubora wa chini sana na hata masoko ya Kimataifa nje ya nchi yetu siyo tu hayatambui ila yanapiga marufuku kwa bidhaa zetu kuingia kwenye masoko haya. Sababu zinazotolewa na masoko haya ni kuwa ulaji wa bidhaa hizi ni hatari kwa afya za binadamu. Je, Wizara ya Ushirika na Masoko inatoa kauli gani kuiondolea aibu na fedheha Taifa letu mbele ya jamii ya Kimataifa? Wizara ina mipango gani kuhakikisha kuwa bidhaa za mifugo yetu ikubalike katika masoko ya Kimataifa ?

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kuna mazao mengi ya chakula kama matunda, mboga mboga, nyama, mayai lakini cha kushangaza katika maduka makubwa na mahoteli makubwa vyakula vinavyoliwa au kuuzwa ni vile vinavyotoka nje ya nchi. Nchi zile zile za nje zimepiga marufuku mazao na bidhaa za chakula zinazozalishwa nchini kwetu Tanzania. Serikali inatoa kauli gani kuwalinda wakulima na wazalishaji wetu hasa wakati hata soko letu la ndani linapovamiwa na bidhaa kutoka nje? Ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo hasa wakati maembe, machungwa, viazi, maharage na kadhalika yanayozalishwa hapa ndani yanaachwa yanazagaa pote Vijijini na Mijini kwa bei ya chini ya kutupa.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukushukuru sana kwa kukubali kuchapisha mchango wangu kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge (*Hansard* ya tarehe ya leo).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Ushirika na Masoko.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika hoja hii ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Balozi Sir George Kahama na Naibu wake, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje kwa kazi nzuri na ngumu ambayo wameifanya miaka mitano iliyopita kufufua uchumi wetu katika Ushirika na Masoko. Nawapongeza sana pia Watendaji wote wa Wizara hii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Dr. L. Komba. Kwa kweli utendaji wao mzuri na uongozi bora wa Mawaziri wetu umetufikisha katika mafanikio ya Wizara hii ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri uko katika maeneo matatu yafuatayo:-

Programu ya kuendeleza mifumo ya masoko ya kilimo (*AMSDP*), katika ukurasa wa 70 – 72 fungu la 90 – 94 wa kitabu cha hotuba Mheshimiwa Waziri ametaja Wilaya nane zilizohusishwa katika programu hii ilipoanza mwaka 2003/2004. Ninaomba kufahamu mpaka sasa Wilaya ngapi zimehusishwa katika programu hii na katika Mikoa gani. Nafahamu na tuliomba programu hii iingizwe Wilaya ya Same Mkoani Kilimanjaro. Tayari programu hii ilishaingizwa pale, lakini ningombaa kufahamu mpaka sasa imeanza na mipango gani ya kuendeleza masoko ya mazao ya kilimo.

Kwa kuwa uamuzi wa wapi programu hii iechezwe, inategemea uamuzi wa Watendaji wa Halmashauri zetu na Washauri wa programu (*consultants*), ninaomba iwepo nafasi maalum ya kuwashirikisha Wabunge na wananchi walolengwa. Utaratibu wa sasa wa wataalam hawa kuwahoji wananchi kama kuwapeleleza ili kupata uamuzi wa wataalam haufai. Hata Baraza la Madiwani kule kwetu Same walishirikishwa kuitisha uamuzi wa mwisho wa wataalam bila kushirikisha mawazo/hoja zao. Ili programu hii ifaulu vizuri, ipo haja ya kufanya marekebisho haya.

Vyama Vikuu vya Ushirika, katika ukurasa wa 78 – 82 Ibara ya 99 hotuba ya Waziri imeeleza vyema kuhusu majukumu yatakayotekelozwa ili kuupatia maendeleo Ushirika. Mpango huu ni mzuri na naipongeza Wizara kwa kuubuni. Mgogoro wangu uko katika utekelezaji wake. Je, *National Cooperative Bank* itaanzzishwa? Kama itaanzzishwa, ni lini? Kwa sababu hotuba haikutaja ni lini.

Nafahamu huko nyuma tumeshakuwa na mipango kama hii lakini haikutekelezwa. Mfano mzuri ni Chama Kikuu cha Vuisu kule Same (*VCU*). Tuliomba mkopo wa kununulia *lorry* la *VCU* ili kusambaza kahawa yetu kwa mpango wa *Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)*. Tulitimiza masharti yote ya Wizara/Ushirika, Wizara ya Fedha na hata tulikuwa na barua ya Waziri wa Ushirika/Masoko na Waziri wa Fedha,

tulikwama Benki Kuu. Mpaka leo hatujapata lile *lorry* wala mkopo wake. Naomba kufahamu Mheshimiwa Waziri kitu gani kilitokea? Naomba majibu.

Mradi wa kuendeleza na kuboresha Biashara ya Pamba na Kahawa, katika Ibara ya 101 ukurasa wa 86 Mheshimiwa Waziri ameeleza mpango mzuri na makini wa kuimarisha ubora wa mazao ya kahawa na pamba. Jambo moja na kubwa ambalo ninaomba Mheshimiwa Waziri alipatie ufanuzi wa kina ni vipi mazao haya yatakuwa na tija kwa wakulima wetu kwa kuwa na bei ambazo zinalipa? Bei ya pamba na kahawa hivi sasa iko chini sana. Wakulima wetu wanapunjwa sana. Je, ni kwa nini Serikali haitoi ruzuku kwa wakulima wetu pale bei ya soko ya mazao haya inapokuwa hailipi?

Huko nyuma Mashirika ya Umma yaliendeshwa kwa hasara na bado Serikali iliyapa ruzuku hadi tulipoyabinafisha. Je, wakulima wana dhambi gani ya kupatiwa ruzuku pale ambapo bei ya mazao yao haina tija kwa kilimo chao? Naomba maelezo ya kuwezesha wananchi kuelewa mapungufu haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia zote na kumtakia Mheshimiwa Balozi Sir George Kahama afya njema anapostaafu kazi ya Ubunge. Tunamwomba aendelee kuwa mshauri wetu popote pale tutakapomwona kwa ushauri. Ahsante.

**MHE. ZAHOR J. KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, wakati tulipokuwa tukijadili hotuba ya Wizara hii mwaka jana 2004/2005 nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi kuhusu haki za Vyama vya Ushirika vya Zanzibar kutoka iliyokuwa WASHIRIKA. Mheshimiwa Waziri alijibu kuwa kazi hiyo ipo katika hatua za mwisho ili wahusika wote walipwe haki zao, lakini mpaka sasa hakuna malipo yoyote yaliyofanyika zaidi ya kinachoendelea ni Vikao visivyokwisha.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuvunjika kwa WASHIRIKA mali za Vyama hivyo zilikuwa chini ya usimamizi na dhamana ya Serikali, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwa sasa mali hizo zipo chini ya nani na lini tatizo hili litamalizika au Vyama husika kulipwa haki zao.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Kwa mara nyingine naipongeza Wizara kwa kutekeleza sehemu kubwa ya kazi ambayo ilipangwa kufanywa mwaka wa fedha uliopita 2004/2005.

Aidha, matarajio yaliyowekwa katika hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yanaleta matumaini.

Maombi ya wananchi wa Ruangwa ni kupata Afisa au Mtaalam wa Ushirika ili asaidie katika kuimarisha Vyama vya Msingi vilivypo ambavyo ni vichache na asaidie kuanzisha Vyama vipyta vya Msingi ikiwa ni pamoja na Vyama vya Akiba na kukopa. Hii itasaidia sana katika harakati ya Wilaya ya kukamilisha vikundi vya wakulima hususan wakulima wa mazao ya mbogamboga. Serikali imeanzisha kilimo cha umwagiliaji na

mwitikio wa wakulima umekuwa wa kutia moyo. Wameanzisha zaidi ya vikundi mia moja, vikundi ambavyo msingi mkubwa wa kujenga Vyama vyta Ushirika ili mradi tunapata wataalam makini katika shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba tena kama nilivyoomba mwaka jana 2004 Wilaya ipewe mtaalam wa Ushirika na wasaidizi walio makini ili wakulima waweze kujiongezea kipato chao maradufu kwa kuwa na Vyama vyao vyta Ushirika ambavyo vitasaidia kuuza mazao na kujipatia mahitaji ya pembejeo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko na kuwatachia Mheshimiwa Clement George Kahama ambaye hatagombea tena kila la kheri katika shughuli zake.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Naomba mruhusu uanzishwaji wa Vyama vyta Msingi vipyta. Kuna malalamiko mengi sana huko Vijijini.

**MHE. LUCAS SELELII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimia Spika, kwanza ninakupongeza mno Mheshimiwa Waziri Sir George Kahama kwa utumishi uliotukuka, kujitolea kuimarisha Ushirika nchini, kujitolea kusaidia kutatua matatizo ya *WETCU* na kumpa elimu Kijana Chibulunje.

Mheshimiwa Spika, kwa Watanzania/Waafrika mtu akiwa hai hasifiwi hadi afe. Yote uliyoyafanya tangu enzi za *CDA* na hata leo USHIRIKA ni Mungu ndiye atakulipia.

Mheshimiwa Spika, pili, tatizo la wakulima wa pamba kuwa na matatizo yasiyokwisha, hivi ni kwa nini? Bei haipo wazi kwa mkulima, sina hakika iwapo inalipa. Hebu ingilie kwa makini.

Wananchi wamekubali kujiunga na kuanzisha *SACCOSS* zao za Kilimo, Wafugaji, Wafanyabiashara na kadhalika. Tatizo linakuwa ni mitaji midogo ya kuimarisha Vyama vyao.

Je, kuna utaratibu gani wa kuwawezesha hasa katika mfumo huu wa MKUKUTA na MKURABITA?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja

hii ya makadirio ya fedha ya Wizara yetu ya Ushirika na Masoko ambayo imewasilishwa leo asubuhi na Mheshimiwa Waziri.

Lakini kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa kutoa hotuba toka Bunge lako hili limeanza, ningependa nichukue fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamefariki dunia, Mheshimiwa Abu Kiwanga - Mbunge wa Kilombero na Mheshimiwa Margareth Bwana aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Waheshimiwa Wabunge hawa wawili wote walikuwa ni Wajumbe wa Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara na kwa hiyo, tulifanya nao kazi kwa karibu sana. Kwa hiyo, naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja hii ni kumsaidia Mheshimiwa Waziri mtoa hoja katika kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ama kwa kuandika au kwa kuzungumza hapa Bungeni. Lakini pia nataka tu niseme kwamba Mheshimiwa Waziri atawatambua rasmi kwa kuwataja majina atakapopata fursa ya kuhitimisha hoja yake. Lakini kabla ya kujibu baadhi ya hoja, niwahi tu kutamka kuwa na mimi naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Pengine kabla sijaanza kupitia hoja moja moja, naomba niwashukuru kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja yetu kwa njia zote mbili yaani wale waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Lakini nataka tu niwashukuru wote kwa ujumla wao, waliunga mkono hoja yetu ikiwa ni pamoja na dada yangu Aisha Magina, aliywakilisha upande wa Upinzani. Kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pengine nichukue fursa hii kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao ama kwa kutokuelewa au kwa kupitia hotuba yetu haraka haraka wamejichanganya katika baadhi ya mambo. Wa kwanza nadhani nianze na dada yangu Mheshimiwa Aisha Magina, Msemaji Kambi ya Upinzani ambaye katika mchango wake anasema kuwa kuna Ushirika wa kuigwa toka nje na kwamba Ushirika uliopo sasa hivi ni ule wa *SACCOS* na *SCCULT*. Hii sio sahihi. Sio sahihi hata kidogo! Kama angekuwa amesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 15 na ibara ya 16 angeona jinsi tulivyoainisha kwamba pale kuna Ushirika wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, Ushirika una wigo mpana, sio hiyo peke yake ya *SACCOS* aliyoisema na kwanza *SCCULT* ni aina ya Muungano wa Vyama vya Ushirika ambavyo vinaunganisha *SACCOS* zote. Kwa hiyo, *SCCULT* sio aina ya Ushirika.

Nataka tu niseme kwamba, katika jedwali lililoanishwa katika kurasa hizo nilizozitaja inaonyesha jinsi Vyama mbalimbali vilivytanda katika nchi nzima na kwa hiyo, hata hizo *SACCOS* alizozisema kwamba zinajali zaidi Mjini sio sahihi. Kwa sababu nyingi ziko Vijijini na ushahidi hapa akinamama mara kwa mara tukiwachukua kwa mfano Mheshimiwa Jenista Mhagama anatoa mfano mzuri sana wa *SACCOS* zake

ambazo ziko Vijijini. Hapa Dodoma *SACCOS* nyingi sana ziko Vijijini, kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba *SACCOS* ziko Mijini tu. *SACCOS* ziko kila mahali, lakini nataka nisisitize kwamba Ushirika uko wa aina mbalimbali sio wa *SACCOS* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Lakini pia nijaribu kumsaidia kijana wangu Mheshimiwa Danhi Makanga. Alijaribu kujielekeza kusema kwamba pengine Wizara haijafanya chochote na kwa hiyo, Ushirika uliopo uko tu kwa maandishi lakini utekelezaji haupo. Hasa hili suala la *SHIRECU* ambalo amelizungumzia kwa uchungu sana pengine Mheshimiwa Waziri atakuja alieleze kwa kina zaidi. Mimi nataka tu niseme kwamba bila juhudzi za Serikali na Wizara kwa ujumla hata hiyo *SHIRECU* anayezungumzia sasa hivi kwa uchungu pengine hii leo isingekuwepo.

Kwa hiyo, nadhani pengine badala ya kulaumu tu ingekuwa ni vizuri kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya. Lakini simlaumu sana Mheshimiwa rafiki yangu Makanga pengine ni suala tu la utaratibu kwamba unajua wakati mwingine kama umefunga mbuzi wako kwenye zizi akakaa muda mrefu sana sasa hata ukimfungulia ataona bado amefungwa tu. Kwa hiyo, hili nadhani tungeweza tukamsamehe namna hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hapo napenda nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Iko hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini inayozungumzia kutokana na umuhimu wa *SACCOS* vipi Wizara isifikirie kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika Nchini? Wizara sasa hivi kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania *TFC* inaratibu uanzishwaji wa Benki hiyo. Muda si mrefu taratibu zitakamilika na wadau waweze kuitwa ili waweze wakaamua ni namna gani ya kuanzisha Benki hiyo.

Lakini si hivyo tu, hivi karibuni tumekuwa na mawasiliano na wenzetu wa Mashirika mbalimbali wa kuweza kutusaidia. Ni juzi juzi tu Mheshimiwa Waziri amerudi safari, lakini moja ya madhumuni ya safari yake ilikuwa ni katika kufuatilia suala la uanzishaji wa Benki ya Ushirika. Kwa hiyo, katika hili tunaendelea kulishughulikia. Kwa hiyo, tunashukuru kwa mchango alioutoa Mheshimiwa Makwetta katika hili.

Mheshimiwa Spika, liko suala ambalo limejitokeza la Chama Kikuu cha Ushirika Mkao wa Dodoma ambalo Mheshimiwa George Malima Lubeleje amelisema. Akauliza Vyama vya Msingi ni vingapi na *SACCOS* ziko ngapi?

Nataka niseme tu kwamba hadi mwaka huu wa 2005 Mkao wa Dodoma una jumla ya Vyama vya Msingi 127. Kati ya hivyo Vyama vya Akiba na Mikopo viko 99, idadi hii ya Vyama ukiiangalia inaweza ikatosheleza kabisa katika suala zima la kuanzisha Chama Kikuu.

Lakini kama tulivyokuwa tumejibu na masuala mengine hapa Bungeni huko nyuma ya Mheshimiwa Lubeleje tulisema kabisa kwamba suala la kuunda aina ya Ushirika wowote ule wa ngazi yoyote ile ni suala la wanachama wenyewe.

Kwa hiyo, nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge katika hili tushirikiane na mimi nikiwa kama mdau wa Mkoa huu wa Dodoma kujaribu kuhamasisha watu wetu tuangalie uwezekano wa kuanzisha Chama cha Ushirika. Lakini kusema kweli lazima wanachama wenyewe wawe wameridhia aina ya Ushirika wanaotaka kuuanzisha.

Liko suala ambalo pia amelieleza Mheshimiwa Lubeleje hapa kwamba Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi na vitendea kazi vya Watumishi kwa Wizara? Maslahi yote ya Watumishi wa Umma ni *centrally controlled*.

Kwa mfano, mishahara na posho mbali mbali zinafuata taratibu na miongozo ya Serikali, inayotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Lakini vile ameleeza kwamba, Ushirika wapo katika Halmashauri za Wilaya, pamoja na kuwaendeleza kitaalam ili kuboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, Kiwizara tupo mstari wa mbele katika kuboresha vitendea kazi vya Maafisa Ushirika waliopo katika Halmashauri za Wilaya, kwa kuwawezesha kutekeleza majukumu mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao kwa ajili ya Maafisa Ushirika waliopo katika Halmashauri zetu za Wilaya: Mwaka 2002/2003 zilitolewa Pikipiki 20, mwaka 2003/2004 zilitolewa pikipiki 49 na mwaka 2004/2005 zilitolewa pikipiki 19; jumla pikipiki 88. Sasa hizi ni jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba, tunawasaidia watumishi wetu katika kupata vitendea kazi. Aidha, Wizara inatambua umuhimu wa mafunzo kwa Watumishi wetu na imewadhamini jumla ya Maafisa Ushirika 373 kwa mafunzo ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mbunge wa Ngara, aliongelea juhudzi za kudhibiti ubadhifuru katika Ushirika. Juhudi za kudhibiti ubadhifuru katika Ushirika tayari zimeshachukuliwa na Serikali kwa kutunga Sheria Mpya ya Vyama vya Ushirika, ambayo moja ya vipengere vilivyomo mle ni kusisitiza suala zima la Uongozi adilifu na kwa hiyo ndiyo maana kuna Maadili ya Uongozi na utendaji katika Vyama vya Ushirika. Lakini, isitoshe Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, chini ya Sheria hiyo hiyo, amepewa madaraka ya kuwaamuru wale wote watakaokuwa wamehusika na ubadhifuru waweze kulipa. Kwa hiyo, jitihada za kusimamia ubadhifuru katika Vyama vya Ushirika zinafanyika kwa njia ambayo ni ya karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, alishauri Wataalam wa Wizara, waende kwa Wananchi Wilayani na vijijini, kushirikiana nao katika kuleta maendeleo ya Ushirika. Aidha, Wataalam wawezeshwe kwa fedha na vifaa mbalimbali. Katika hili nadhani nimelieleza nilipokuwa najibu ile hoja ya Mheshimiwa George M. Lubeleje kwamba, jitihada zinazoendelea sasa hivi ni hizo za kuwafanyia mafunzo. Lakini vile tunasisitiza tu kwamba, kule Wilayani sasa hivi ndiko ambako kusema kweli kunatakiwa Watumishi hawa waajiriwe. Mwanzo pale tulipokuwa tumetoa taarifa ile ya Kamati ya Rais ya Kumshauri juu ya Kufufua, Kuimarisha na kuendeleza Ushirika,

tulibaini upungufu wa Watumishi 300 ili kuweza kuendeleza Ushirika nchini. Lakini hii haina maana kwamba, Watumishi hao 300 wangeajiriwa na Wizara, badala yake tulainisha tu ili Wilaya mbalimbali ziweze kubaini mapungufu walijonayo na kuweza kuwaajiri kwa sababu Watumishi hawa ni wa Halmashauri za Wilaya na ndiyo wanatakiwa watume na hata wanaweza kuwfikisha vijijini.

Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, alizungumzia Usajili wa Vyama kuwa una matatizo kwani Msajili hatoi huduma inayostahili hivyo, Wizara isaidie. Mkoa wa Tabora hauna Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, kufuatia aliyekuwepo kupewa majukumu mengine. Hata hivyo, usajili wa Vyama umekuwa ukifanyika Mikoa ya karibu kama alivyosema ya Shinyanga na Singida. Mrajisi wa Mkoa wa Tabora, atarejea Mkoani kunzia Agosti, 2005 kuendelea na kazi hiyo na huyu ndiye yule ambaye kijana wangu, Mheshimiwa Danhi B. Makanga, amezungumzia kwa uchungu sana kwamba, aondoke, nadhani hayo Mheshimiwa Waziri, atakuja aeleze vizuri zaidi. Lakini huyo alikuwa ndiye Mrajisi Msaidizi wa Tabora, alikwenda kuimarisha *Union* yetu kule ya *SHIRECU* na sasa hivi ina hali nzuri.

Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, alizungumzia pia tishio la kufilisiwa *WETCU*. Serikali ya Mkoa na *WETCU* imeshughulikia suala ambalo linatokana na kesi iliyofunguliwa na aliyekuwa Meneja Mkuu wa *WETCU*. Makubaliano yalifikasiwa na utatuza kupatikana, hivyo kwa sasa hakuna tishio la kufilisiwa *WETCU*. Hizo ni jitihada za Serikali, ambazo zimefikisha hapo na *WETCU* inaendelea kufanya kazi kama kawaida. (*Makofit*)

Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, vile vile alizungumzia hoja kuwa, wakulima wa pamba wamelipwa kiwango cha chini sana kinyume na matarajio yao kupitia kwenye Chama cha *KACU*. Serikali inaangalia uwezekano wa dhamana kwa *KACU* na kupata fedha kwa ajili ya kuwalipa wakulima kutokana na pamba iliyokusanywa au kununuliwa na Chama hiki.

Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mbunge wa Chumbuni, anaomba Mheshimiwa Waziri, aeleze kwa sasa mali zilizokuwa za Washirika zipo chini ya nani na ni lini tatizo la mgawanyo wa mali litamalizika na Vyama husika kulipwa haki zao?

Mheshimiwa Spika, mali zilizokuwa za Washirika zipo chini ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika na *CUZA*, *CUZA* ni Chama Kikuu cha Ushirika kule Zanzibar, kufuatia kikao cha *Task Force* iliyokabidhiwa jukumu la mgawanyo wa mali kilichofanyika Bagamoyo tarehe 5 mpaka 8 Mei na Wajumbe wake walifikia muafaka jinsi ya kugawana mali hiyo. Kwa sasa muafaka huo, unafanyiwa marekebisho ya mwisho ili utekelezaji uweze kuanza.

Mheshimiwa Semindu K. Pawa, alitoa hoja akitaka kujua kuwa kuna Vyama vingapi vya Ushirika katika Mikoa ya Dar es salaam, Singida, Dodoma, Kagera na Morogoro. Mchanganuo kwa kweli upo katika kitabu chetu kile cha hotuba. Lakini kwa kumsaidia tu, Dar es salaam viko 437, Kagera 467, Morogoro 231 na Dodoma 127, kama nilivyokuwa nimekwisha sema hapo awali.

Vile vile Mheshimiwa Semindu K. Pawa, alihoji kwa nini Wananchi wengi hupenda kujiunga kwenye vikundi kuliko Vyama vya Ushirika. Sasa, suala la kujiunga na Vikundi au Ushirika ni hiari ya mtu. Hata hivyo, Wananchi huchagua kujiunga na Ushirika au Vikundi baada ya kuhamashisha na kupewa elimu husika. Uzoefu unaonesha kuwa, baadhi ya Wananchi huchelea kujiunga na Vyama vya Ushirika kutokana na historia tu kama ilivyoelezwa mwanzo pale kwamba, huko nyuma kumekuwa na matatizo katika Vyama vya Ushirika, ambayo yamesababishwa na watu wachache lakini siyo kwamba, dhana ya Ushirika yenye ina matatizo. Kutokana na uhalifu huo uliokuwa umetokea kwenye Vyama vya Ushirika, mtu mwingine sasa hivi akiambiwa habari ya Ushirika, anaona kama anapelekwa mahali kusiko husika. Lakini tunasema kwamba, elimu itaendelea kutolewa, kuwaeleza Wananchi juu ya dhana ya Ushirika, waweze kuelewa faida yake.

Mheshimiwa Robert K. Mashala, alizungumzia Wizara kuimarisha Vyama vya Ushirika kwa kuaajiri Maafisa Ushirika, hii nadhani nimekwisha kulieleza kwamba, kwa kweli jukumu hili ni la Halmashauri zenyewe. Sisi tuliweza kuainisha tu kwamba, idadi inayotakiwa ni hiyo, lakini suala la kuajiri ni la Halmashauri za Wilaya, vitendea kazi ni hivyo kama nilivyokuwa nimeeleza katika hoja zilizotangulia.

Mheshimiwa Robert K. Mashala, alisema pia kuwa, Ushirika nchini ni mbaya ukilinganisha na hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Lakini mimi ninasema tu kwamba, vijana wa Kisukuma hawa, nadhani kwa kweli wangeweza wakaangalia utaratibu wa jinsi Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi. Nataka tu niseme kwamba, kwa hapa nchini hakuna Vyama vya Ushirika vinavyosaidiwa sana na Serikali kama Vyama vya Ushirika vya Mikoa ya Wasukuma hasa Shinyanga na Mwanza, wanasaidiwa sana. Lakini kwa bahati mbaya sana, rafiki zangu hawa ndiyo walalamikaji wakubwa. Sasa kama wenzao ambao hawasaidiwi hapa wangekuwa wako katika hali hiyo, sijui wangesemaje! Lakini nataka tu niseme kwamba, *SHIRECU* na *Nyanza Cooperative Union*, Vyama vyote hivi vimekuwa na matatizo makubwa ya aina mbalimbali, lakini Serikali imejitahidi sana kuvisaidia. Kwa hiyo, ningeomba tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu hawa wa Kisukuma, tusaidiane katika kuipongeza Serikali katika jitihada zake hizi na hatimaye Wananchi waweze kuelewa kwamba, Serikali yao inafanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Meneja Mkuu aliyepelekwa na Serikali kwa nia ya kusaidia *SHIRECU*, watumishi hao hawakuisaidia *SHIRECU* ni mufilisi, nimekwisha eleza lakini Mheshimiwa Waziri, atakuja kulitolea maelezo kwa ufasaha zaidi. Lakini nataka tu kusitiza kwamba, nia ya Serikali ni njema ya kusaidia *SHIRECU* na kama nilivyosema kwamba, pengine bila jitihada hizo za Serikali, *SHIRECU* inayozungumziwa sasa hivi pengine isingekuwepo.

Takwimu za Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, zinaonesha Jedwali Na. 5 Ukurasa wa 97, kati ya Vyama hivyo vilivyokaguliwa. Hili ni suala la kuimarisha masuala ya Ukaguzi. Tumeeleza katika hotuba na katika taarifa zetu mbalimbali kwamba, ukaguzi unaimarishwa kwa sasa hivi kwa sababu kama ukiangalia toka huko nyuma, Shirika letu la *COASCO*, lilikuwa na wataalam wachache sana, wenye sifa zinazostahili na tumeeleza kwenye hotuba walikuwa wenye *CPA* wawili tu lakini sasa hivi wamefikia 17. Kwa hiyo,

tunadhani kwamba, hatua zinafanyika kuweza kuhakikisha kwamba, wakaguzi wenye ujuzi na uzoefu wanapatikana kuweza kusimamia Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Philip A. Magani, alizungumzia Wilaya ya Ruangwa kuwa ipewe Mtaalam wa Ushirika na wasaidizi wake. Jukumu la kuajiri Maafisa Ushirika, liko chini ya Wilaya, hili nilikuwa nimeshalieleza katika taarifa za awali.

Wanaushirika wasilazimishwe kujiunga na kuuza mazao yao kwa Vyama Vikuu vya Ushirika, ambavyo ni vya kiimra zaidi kuliko hiari. Haya ni maelezo ya dada yangu mpendwa, Mheshimiwa Aisha P. Magina. Sheria ya Ushirika iko wazi na misingi ya Ushirika inasema, Ushirika ni wa hiari, hivyo Serikali haimlazimishi mtu kujiunga au mtu ambaye siyo mwanachama, kuuza mazao yake. Nataka tu kusitiza hapa kwamba, suala la Ushirika ni la hiari, kwa hiyo, hakuna mtu ye yeyote anayemlazimisha mtu kujiunga na Chama, wala mtu ye yeyote kuuza mazao yake kupitia kwenye Chama cha Ushirika. Hii ndiyo maana hata kuna utaratibu wa Mfumo wa Soko Huria, ambapo wanunuzi wapo wa aina mbali mbali na kwa hiyo, sasa hivi hili linatekelezwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, alizungumzia kuhusu Viongozi kusaidia kuhamasisha Ushirika Mpya, hii nadhani ni rai nzuri ambayo tuseme kwa kweli ndiyo tunayoifanya na hata tunapotoa maelezo na taarifa mbalimbali Bungeni, nia yake ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge, tuweze kuelewa dhana nzima ya Ushirika na faida zake ili tunaporudi kule tunakuwa mfano kwa matendo na maneno, kwa maana ya kwamba, tunajiunga na Vyama vya Ushirika sisi wenyewe, halafu vile vile tunawaeleza wenzetu wajiunge. Vinginevyo tunaweza kuwa tunahamasisha bila kujiunga na Vyama, Wananchi wetu itakuwa ni vigumu sana kulieleta suala hili. Kwa hiyo, nataka nitoe wito tu kwamba, tuanzie sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, hapo tunaporudi kwenye Majimbo yetu na hasa kipindi hiki ambacho tutakwenda kutafuta ridhaa ya Wananchi. Moja ya Sera nzima ya kuhimiza, hilo ni suala la kuhamasisha Ushirika nchini.

Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, amesema *Nyanza Cooperative Union* hawakuruhusiwa kununua pamba msimu huu kwa sababu hawakuwalipa wakulima albaki ya bei ya pamba. Hili nataka niwachie Mheshimiwa Waziri, atakuja kulitolea maelezo, lakini kama nilivyokwisha sema, msaada wa Serikali katika Vyama hivi Vya Nyanza na *SHIRECU*, umekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, vile vile amesema udhibiti wa fedha katika Vyama vingi vya Ushirika siyo wa kuridhisha. Nimekwisha kutoa maelezo kwamba, tunajitahidi kwa kadri inavyowezekana, kupata wakaguzi wa kutosha na wenyewe ujuzi, waweze kusimamia ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

Liko suala la Mheshimiwa Danhi B. Makanga tena la wafayakazi walipwe madai yao. Nadhani hili niache Mheshimiwa Waziri, atakuja kulitolea maelezo.

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, alizungumzia Maafisa Ushirika waliopo Wilayani kwamba, wapewe mwongozo wa utendaji kazi zao, kwani wengi wao hawafanyi wanavyostahili. Hii kazi tunaendelea kuifanya, sasa hivi

mafunzo ya aina mbalimbali yanaendelea kufanyika na sasa hivi katika programu nzima hii ya mageuzi pamoja na *modernization* ya Vyama vya Ushirika, moja ya kipengere muhimu sana tunachokitazamia ni hiki cha kuwapa mafunzo watendaji wetu, pamoja na uongozi kwa ujumla ili kuhakikisha wanafanya kazi zao ipasavyo.

Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, alisema Wananchi kuanzisha *SACCOS* taito linakuwa ni mitaji midogo midogo ya kuimarisha Vyama vyao, je, kuna utaratibu gani wa kuwawezesha hasa katika Mfumo wa MKUKUTA na MKURABITA?

Mheshimiwa Spika, katika kuanzisha hizi *SACCOS*, ukisema kwamba, usubiri mpaka utakapokuwa umepata Malaki ndiyo uanze kijiunga, nadhani hutafanya hivyo. Kinachotakiwa ni kidogo kidogo ulichonacho mnajiunga, unaanza kuweka akiba. Lakini kutokana na hizo akiba mnazoziweka, nadhani kuna Mifuko mbalimbali inaweza ikavutika kuweza kuwasaidia. Lakini cha msingi, tungependa kwanza, watu waanzishe hizi *SACCOS* ili iwe ni njia ya kupitishia hata kama msaada umetokea, ikiwa ni pamoja na Mfumo wa MKUKUTA aliouelezea Mheshimiwa Mbunge hapa.

Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, amezungumzia kwamba, Kiteto hakuna Vyama vya Ushirika, hivyo waruhusiwe kuanzisha Chama chao. Hili ni sawa sawa na lile nililolieza wakati nikijibu hoja ya Mheshimiwa George Lubeleje kwamba, suala la kuanzisha Ushirika kwa kweli ni hiari na wanachama wenyewe, lazima waainishe sababu za kuanzisha na Chama hicho kiwe na kazi ya kufanya, kiwe kinawahudumia Wananchi.

Mshamba ya Magungu yasikodishwe kwa watu wengine bali wapatiwe wanakijiji wenyewe. Vyama vya Ushirika havifungamani na mipaka ya Mkoa, kwa Vyama hivyo vilivyoko Kiteto ni wanachama wa *ACU*, hivyo shamba hilo ni Ushirika wa *ACU*.

Mheshimiwa Spika, ningependa pengine sasa nijielekeze katika masuala machache ambayo yametokana na Sekta ya Masoko. Iko hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Semindu K. Pawa, anasema Wizara itoe tamko kuhusu walangazi wanaonunua Ufuta Morogoro Vijijini, debe shilingi 300 tu, huu ni unyonyaji kweli. Utaratibu uliopo wa kununua mazao ni kwamba, ununuzi wa mazao unatakiwa ufanyike katika vituo maalum vya kununulia.

Mheshimiwa Spika, suala hili tunalalamika sana hapa kwamba, kuna unyonyaji, watu wanunua mazao mashambani, watu wanatumia vipimo visivyo sahihi. Lakini nadhani tunasahau tu kwamba, tunatakiwa sisi wenyewe kule, hasa kutumia mamlaka zilizoko kule kwenye maeneo yetu, Halmashauri za Wilaya wako kule, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata. Hao ndiyo wanatakiwa wasimamie mambo yote haya, lakini kwa hapa, hata kama Wizara inaweza kuwa ina-*enforce* hizi sheria, lakini Wizara iko mbali sana kuweza kuyasimamia haya. Kwa hiyo, wito wangu katika hili, ningependa tu kwamba, pengine elimu itolewe kwa Watendaji wetu walioko kule ili waweze kuelewa taratibu za mazao kwamba, mazao hayatakiwi kununuliwa katika vituo visivyo rasmi, suala hata hili la kupanga bei kwa utaratibu wa *cater*, yote haya ni taratibu ambazo ziko kinyume na utaratibu uliopo. Kwa hiyo, ningependa tu niombe tushirikiane na mamlaka

mbalimbali zilizoko kule na Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane katika hili ili tuweze kufanikisha suala hilo la Wananchi wetu wasiendelee kunyonywa.

Ufunguzi wa Soko la Tawa Jimbo la Morogoro Kusini na Tandai Kinore Jimbo la Morogoro Kusini-Mashariki, Waziri anaombwa kufungua Masoko hayo. Hii hoja tumeizingatia lakini sasa tulitaka tuseme tu kwamba, wakati tunafungua Soko la Kibaigwa, Mheshimiwa Makamu wa Rais, alichofanya kwa kweli ilikuwa ni kufungua Masoko yote haya kwa mtandao wake kwa sababu ilikuwa kama ni mradi mmoja, lakini hata hivyo, hoja hii tumeizingatia, Mheshimiwa Waziri kwanza, alikwishafika wakati ule wa kuweka Mawe ya Msingi na kadhalika, lakini hata hii ni hoja ya msingi na inaonesha jinsi Wananchi wa Morogoro Kusini-Mashariki, wanavyopenda huduma za Wizara yetu ya Ushirika, hususan kazi anazozifanya Mheshimiwa Waziri.

Maombi ya kujengewa Masoko ya kisasa maeneo ya Mikese, Ngerengere, Kiloka, Mkuyuni ya Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini, yamepokelewa na pindi Wizara itakapopata uwezo wa kushirikiana nao, wanaweza kufanya hivyo lakini tunasisitiza vile vile Halmashauri zenyewe ziweze kuibua miradi hii na kuweza kuitafutia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, aliuliza ujenzi wa soko la Makambako, mbona umekuwa kimya? Namshukuru kwanza, ameshukuru kwamba, angalau tumeliingiza soko hili katika mpango na kama nilivyoeleza katika hotuba yangu katika ukurasa wa 84 sehemu ya 100 kifungu cha 10, ujenzi wa soko la nafaka na bidhaa mchanganyiko katika Mji Mdogo wa Makambako ni mojawapo ya miundombinu ya Masoko yatakayofanyiwa tathmini na ujenzi. Kwa hiyo, nataka tumtoe wasi wasi Mheshimiwa Jackson M. Makwetta katika hili kwamba, linafanyiwa kazi na ndiyo maana tunaendelea kulitamka mara kwa mara, kungekuwa na kigugumizi chochote, tusingekuwa tunalitaja.

Bodi za Mazao, Mashirika ya Masoko yaliyo chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula yapelekwe Wizara ya Ushirika na Masoko. Hoja ambayo imetolewa vile hapa mwisho na Mheshimiwa Henry Shekiffu. Lakini kama tulivyokuwa tumeshajibu mara nyingi hapa kwamba, Bodi hizi za mazao ni Bodi za Serikali na zinasimamiwa na Wizara ya Serikali na sisi ni Wizara ya Serikali, kwa hiyo, tunaomba kukubaliana kwamba, kwa hivi sasa tuendelee na utaratibu huo, lakini kusema kweli ni hoja ya msingi.

Mheshimiwa Spika, bei ya pamba kwa wakulima kuwa ndogo na kutokuwa wazi, kama alivyoeleza Mheshimiwa Dr. James Msekela, nadhani hii nilikuwa nimeshaieleza. Lakini pengine niunganishe hapa na hii hoja ambayo ameizingumza Mheshimiwa Danhi Makanga, pale mwanzo mwanzo na mwisho hapa Mheshimiwa Henry Shekiffu, ya kutumika kwa *internet*, maana yake inaonekana kwamba, tunavyotamka hii tunasema basi *internet* ipelekwe Mayuya, ipelekwe huko Malita Bariadi. Si hivyo, tunachosema ni kwamba, tunaishi katika ulimwengu wa utandawazi, ambapo ulimwengu huu unatumia hiyo *internet*. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, Wizara inajizatiti kuandaa utaratibu wake wa kutumia *internet* ili iweze kusambaza hizi taarifa. Kwa hiyo, hatuwezi kuogopa

kusema *internet*, kwa sababu Mayuya kule Bariadi hakuna *internet*, tunachosema ni kwamba, Serikali inajizatiti kuweka *centre*, ambayo itakuwa inakusanya hizi habari halafu inazitawanya.

Jana nilipokuwa najibu swal, nilisema kwamba, taarifa hizi zinapopatikana, zinasambazwa kupitia Redio Tanzania, kwenye vipindi mbalimbali ambavyo vinatoa matangazo haya na tumesema kwenye hotuba kwamba, sasa hivi tunataka itumike redio iliyoko Usukumanzi kule, *Radio Free Africa*, redio zote hizo zitatumika ili kufikisha ujumbe kwa Wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, muda hautoshi na hoja ni nyingi kiasi, lakini nataka niseme kwamba, kwa hizi za masoko ambazo zimesalia, labda nichukue mbili za mwisho ambazo zimetolewa. Habari ambayo imejitokeza waziwazi hapa ni mkakati wa kinga dhidi ya anguko la bei za mazao makuu ya biashara. Hoja hii ameitoa Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Dr. Kamala.

Ili kukinga anguko la bei ya mazao makuu ya biashara, Serikali inaelimisha na kushauri wakulima na wafanyabiashara, kuhusu utumiaji wa mbinu mbalimbali za kukinga anguko la bei za mazao, ambazo ni pamoja na kuingia katika kilimo cha mkataba, ambacho kimeelezwa vizuri hapa na Mheshimiwa Henry Shekiffu, ndiyo tunajiandaa hivyo.

Kuuza kwa miadi (*Forward Selling Sales*), ambayo Mheshimiwa Makanga, asubuhi alikuwa anasema kwamba, ye ye katika hilo anataka azuie. Ukipanya hivyo, kwa kweli huendi na wakati, kwa sababu wenzako wanafikiria suala la kusonga mbele wewe unasema wakulima wangu hawawezi kufanya hivyo kwa sababu kwa kufanya hivyo ndio baadaye unakuja kupata matatizo ya kuwa na Bima ya bei na kadhalika.

Lakini pia liko suala la maghala ambalo aliliulizia Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo kwamba, kuna maghala ambayo yameandalishi na shirika moja ambalo linasaidia, ambalo sisi tunaliita linasaidia utaratibu wa Benki Mazao. Tumetoa sifa mbalimbali ambazo maghala haya yanatakiwa yaye. Yanatakiwa yaye na Bima kama tulivyokuwa tumeeleza kwenye ile Sheria ya *Warehouse Receipts*, yaye na kinga na vitu vyote hivyo ambavyo vimeelezwa katika Sheria. Kwa hiyo, yanaweza pia yaka-*qualify* kama yanaweza yakatimiza masharti yale yote ambayo yako katika Sheria ya *Warehouse Receipts*.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda tu pengine nimalizie kwa kutumia fursa hii, kusema maneno machache ya shukrani mbele ya Bunge lako Tukufu, linalohitimisha uhai wake wa miaka mitano wiki ijayo. Mimi nimekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge hili, naomba nianze shukrani zangu za dhati na nyingi sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kunitfea na kunipa wadhifa huo wa Unaibu Waziri, nafasi ambayo imeniwezesha kujifunza mengi. (*Makofî*)

Lakini pengine kabla ya hapo, Mheshimiwa Rais, alikwisha niteua kushiriki katika Kamati Maalum ya Rais. ambayo aliongoza Mheshimiwa Waziri wangu hapa, ya kumshauri juu ya masuala ya Ushirika chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri. Katika nafasi zote hizo, kusema kweli nataka kukiri kwamba, nimejifunza mengi, kwa hiyo, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa heshima hiyo aliyonipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick T. Sumaye, kama kiongozi wetu na mwelekezi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni na sisi kama Watumishi chini yake. Amekuwa ni msaada mkubwa sana kwetu, kwa kutuelekeza miongozo mbalimbali. Kwa hiyo, nataka tu kuahidi kwamba, nitatumia uzoefu wake na ushauri aliokuwa anatupa mara kwa mara katika shughuli zangu nitakazokuwa nazifanya hapo baadaye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee nataka niseme tu kwamba, kama nilivyokwisha sema awali kuwa, nimekuwa Naibu Waziri, kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano. Hii ilikuwa ndiyo mara yangu ya kwanza kutumikia wadhifu huu. Napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwa kusema kwamba, kipindi chote hiki mimi nilikuwa shule kwa sababu nilikuwa na mwalimu mahiri sana, kiongozi wetu wa siku nyingi wa Kiserikali na Mashirika ya Mataifa, kusema kweli nimenufaika sana na uongozi wake. (*Makofii*)

Nadhani katika Manaibu wenzangu, mimi najiona kama nilipelekwa shule moja kwa moja. Kwa hiyo, nilikuwa nafanya kazi huku nikiwa niko masomoni na kwa sababu ye ye ndiyo alikuwa ananielekeza na kunifundisha, nadhani ataelewa kama nilifaalu ama sikufaulu. Napenda nimalizie kwa kuwashukuru Watumishi wote wa Wizara, vile vile nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa, kwa kunivumilia na nataka niwataarifu kwamba, niko njiani nakuja huko. Kwa hiyo, nadhani watapokea kwa mikono miwili ili tuweze kuendelea kushirikiana kwa mengine yote na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushirikiano mlionipa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja yangu niliyoiwasilisha Bungeni leo asubuhi na kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda pia kusema kwamba, Wabunge wote waliochangia maeneo ya Ushirika na Masoko, tangu tumeanza Mkutano huu wa Bunge ni 59. Kati ya hawa Wabunge 16 wamechangia kwa maandishi na 13 wamechangia kwa kuzungumza katika kikao cha leo. Lakini pia kati ya hao, wapo Waheshimiwa Wabungu 29, ambao walichangia kuititia hotuba za Bajeti za Wizara mbalimbali hasa ya Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli na Wajumbe wote wa Kamati, pamoja na Mheshimiwa Omar Said Chubi,

Mbunge wa Kilwa Kaskazini, ambaye siku ya leo, aliwasilisha taarifa kwa niaba ya Kamati. Namshukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi, ambao nitawataja hivi punde, wamezungumzia masuala mengi mbalimbali ya Ushirika na Masoko. Hoja zao zinalenga katika kuendeleza na kuboresha shughuli za Wizara na tunawashukuru sana. Baadhi ya michango yao kwa kweli imekuwa mahususi, ambayo inaweza kuchukuliwa na kuwekwa katika mikakati ya utekelezaji wa Wizara yetu katika mwaka huu wa fedha. Nawashukuru sana kwa michango yao yote hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda moja kwa moja, kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia katika hotuba yangu leo hii. Kwanza kabisa, waliochangia kwa kuzungumza Bungeni ambao ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Philip Magani na Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, Waheshimiwa Wabunge 29 walichangia kuhusu masuala ya Ushirika na Masoko, katika hotuba za Bajeti ya Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Kutokana na muda nilionao, sitaweza kuwataja mmoja mmoja. Lakini napenda wafahamu kwamba, michango yao tunaitthamini na tutaifanyia kazi ipasavyo katika mwaka huu wa fedha 2005/2006.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuongeza maelezo machache ya ziada yafuatayo:-

Kwanza kabisa, namshukuru Mheshimiwa Omar Chubi, kwa taarifa yake aliyoitoa Bungeni kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli. Napenda kumhakikishia kwamba, ushauri wa Kamati tumeupokea na tutaufanyia kazi na kuutekeleza ipasavyo. (*Makofî*)

Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Aisha Philip Magina, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani, kwa Wizara yangu, kwa pongezi zake na kwa kuunga mkono hoja. Hoja zake nyingi ni za msingi na zinakubalika. Hata hivyo, sikubaliani na rai yake kwamba, tuisisitize zaidi Ushirika wa mazao ya kilimo na kuupa kisogo Ushirika wa aina nyingine. Kwa mfano, Watanzania wengi waishio Vijijini, wanahitaji sana huduma za kifedha zitolewazo na Mfumo wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, wengi waliozungumza walizungumzia hatua mbalimbali ambazo zitahitajika zichukuliwe na Serikali kusaidia kuimarisha Ushirika, hususan kuhusu madeni ambayo yamevisakama Vyama vya Ushirika. Napenda kuchukua nafasi hii, kutoa taarifa kuhusu hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali katika nyanja hii ya uimarishaji wa Vyama vya Ushirika. Programu kabambe ya mageuzi na *modernization* ya Ushirika, ambayo nimeelezea katika hotuba leo asubuhi, ndiyo mkakati mkuu wenye lengo la kuimarisha Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 na Sheria Mpya ya Ushirika ya mwaka 2003.

Kama nilivyoeleza kwenye hotuba, lengo kuu la programu hiyo ni kujenga upya Ushirika wa Karne ya 21, ili uwe ule unaomilikiwa na kuendeshwa kwa biashara na wanachama waliojasilishwa katika mfumo wa sasa wa utandawazi. Ili kufikia lengo hili, uongozi utaimarishwa na kuboreshwa, Elimu ya Ushirika itatiliwa mkazo, Wananchi wengi zaidi watahamasishwa kuijunga na vyama na kadhalika. Hayo yote yataenda sambamba na uimarishaji wa mitaji ya vyama. Hii ndiyo sababu Serikali inatilia sana mkazo uanzishaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo na kuratibu uanzishaji wa Benki ya Ushirika ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushughulikia madeni sugu, itakumbukwa kuwa, Machi, 2000, Mheshimiwa Rais, aliitisha kongamano la kujadili kuhusu sababu za kuzorota kwa Ushirika nchini na hatua za kuchukua ili kuimarisha. Wakati wa kongamano hili, iibainika kuwa madeni sugu ya Ushirika ni sababu mojawapo iliyozorotesha Ushirika. Aidha, Kamati ya Kumshauri Rais, kuhusu suala hili, iliyoundwa baada ya kongamano hilo, ilipendekeza kuwa, moja ya hatua za kuchukua kuondokana na tatizo hilo, ni kwa Serikali kuitia Wizara yenye dhamana ya Ushirika, kufanya tathmini ya kina na kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili. Pendekero hili lilitokana na ukweli kuwa, vyama vingi vya Ushirika, vinakabiliwa na madeni sugu ya muda mrefu na hivyo itakuwa vigumu sana kwa kujenga mitaji upya bila kushughulikia madeni hayo.

Hali hii baada ya kwenda mbele kiuchumi, Vyama hivi vya Ushirika vitakuwa vinafanya kazi ya kulipa madeni tu bila maendeleo yoyote. Tathmini iliyofanyika hivi karibuni imeonesha kuwa, madeni hayo yamefikia takriban shilingi bilioni 23.8, kati ya hizo shilingi bilioni 16 ni za Serikali, shilingi bilioni tatu ni za Mabenki, shilingi bilioni mbili za wakulima na shilingi bilioni 2.6 ni za Watumishi. Msingi mkubwa wa madeni haya ni mwenendo mbaya wa kibiashara katika Masoko ya Kimataifa, utegemezi wa mikopo ya Benki za Biashara zenye gharama kubwa, udhaifu katika uongozi wa Vyama vya Ushirika na mabadiliko ya mifumo ya uendeshaji biashara iliyokuwa ikifanyika wakati Vyama vya Ushirika havijaandalika ipasavyo.

Kwa kuzingatia mapendelezo ya Kamati Maalum ya Rais, mwaka 2000, Wizara yangu ilifanya tathimini ya kina baada ya kushauriana na wadau mbalimbali, imewasilisha suala hili Serikalini ili madeni mengine takriban shilingi bilioni 16, yafutwe na mengine takriban shilingi bilioni nane yakuchukuliwe na Serikali. Hatua kama hiyo, siyo kitu kigeni kwa Tanzania na hata nchi jirani. Katika kushughulikia suala hili tutahusisha pia madeni mbalimbali ya wakulima kwa Vyama vya Ushirika, hatimaye madeni ya wakulima kwa *KACU* yanayofikia takriban shilingi milioni 213,440, ambazo alizitaja leo asubuhi Mheshimiwa Robert Mashala.

Kwa mfano, Tanzania iliwahi kuchukua madeni ya Vyama vya Ushirika ya shilingi bilioni 35 mwaka 1992, yaliyotokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wa vyama. Aidha, kati ya mwaka 2000/2005, Serikali ilivisaidia vyama vya *KCU, KDCU, Nyanza Cooperative Union, SHIRECU, Biharamulo Cooperative Union* na *KNCU*, jumla ya shilingi bilioni 9.7 kulipia madeni ya Mabenki na wakulima. Nchi ya Kenya pia ilifuta madeni ya Vyama vya Ushirika ya Kahawa yaliyofikia jumla ya shilingi za Kenya bilioni 5.8, sawa na takriban shilingi bilioni 72 za Tanzania ili kufufua vyama hivyo.

Aidha, Serikali hiyo ilikomboa na kurudisha kwa Wanaushirika, Kampuni ya Ushirika ya Maziwa *KCC*, iliyokuwa imenunuliwa na mtu binafsi wakati wa zoezi la ufilisi kwa kulipa takriban shilingi za Tanzania bilioni 10. Kampuni hiyo hiyo sasa inafanya kazi nzuri na inauza Maziwa ndani na nje ya nchi, hususan nchi za Uganda na Ruanda. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, pili ni umuhimu wa Wanaushirika kufanya shughuli zao kwa pamoja. Hii ni rai ambayo ameizungumza kwa kirefu, Mheshimiwa Henry Shekiffu. Napenda kuchukua fursa hii, kusisitiza kuhusu umuhimu wa wanaushirika kufanya shughuli zao pamoja katika kujiletea maendeleo na kutatua matatizo yao sugu, yanayoukabili Ushirika. Serikali itasaidia kila inapowezekana, lakini jukumu la msingi linapaswa kuwa lile la Wanaushirika wenyewe, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri katika mchango wake.

Katika hotuba yangu, nimeelezea kuwa, katika mwaka ujao wa 2005/2006, itaundwa Kamati ya Ushauri ya Wanaushirika, hii ni *National Cooperative Advisory Committee*, itakayotoa ushauri na kuratibu utendaji wa pamoja wa Wanaushirika. Suala hili ni muhimu sana katika kujenga mfumo wa Ushirika endelevu na unaojitegemea. Napenda kutaja mifano michache ambayo inaonesha kuwa, kwa kuungana pamoja, Wanaushirika wanaweza kujiletea na kutatua matatizo yao.

Kuhusu kujiendelea kiuchumi, Vyama vya Ushirika vinaweza kumiliki kwa pamoja viwanda kadhaa. Kwa mfano, viwanda vya kukoboa kahawa vya Mbozi na Mbinga, vinamilikiwa kwa pamoja na Vyama vyote Vikuu vya Ushirika vinavyohusika na kahawa katika nchi nzima. Aidha, kiwanda cha kukoboa na kusaga kahawa cha Tanika kilichopo Bukoba kinamilikiwa na *TFC, KDCU* na *KCU*. Vile vile *Tanganyika Coffee*

*Curing Company* kinamiliwi na KCU, ACU, RIVACU, VUASU na *Tanganyika Coffee Growers Association*.

Kuhusu kutatua matatizo kwa pamoja, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hivi karibuni Shirika la Vyama vya Ushirika (*TFC*), kwa ushauri wa Serikali, limeweza kuchukua madeni ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (*KACU*), kiasi cha shilingi milioni 260,000 na hivyo, kunusuru mali zake zisinadiwe kufidia madeni ya Benki ya *CRDB*.

Tatizo la *SHIRECU* ambalo Waheshimiwa Wabunge, wamelizungumzia leo asubuhi, napenda kuweka kumbukumbu kwenye *Hansard* kwamba, matatizo ya *SHIRECU* ni ya kihistoria na Waheshimiwa Wabunge wote, waliozungumza wanalfahamu. Kiini chake ni uongozi uliokuwa madarakani miaka ya nyuma na hilo linafahamika. Uongozi huo ulikuwa unaajiri Watumishi kwa kufuata undugu au kufahamiana, badala ya kufuata sifa zinazotakiwa na hilo pia wanalfahamu. Hali hii iliotesha mizizi ambayo itachukua muda mrefu kuing'oa hata sasa. Ikumbukwe kuwa, hali ya *SHIRECU* ilikuwa mbaya sana na ndipo Serikali ilipoingilia kati na kuwaweka Mameneja na msimamizi wa fedha ili kurekebisha mambo na tangu hapo hakuna wizi uliotokea. (*Makofi*)

Tokea hapo hali ya *SHIRECU* haijawa mbaya zaidi, bali inaimarika. Hata hivyo, Meneja aliyepo sasa, atakabidhiwa madaraka hivi karibuni baada ya kukamilisha taratibu za kumchunguza (*vetting*), meneja aliyechanguliwa. Siku hizi siyo kama zamani, tuna-vet mtu amezaliwa wapi, amesoma wapi, amefanya kazi gani, ana kasoro gani, kabla ya kumruhusu. Kwa hiyo, haitaruhusiwa mpaka tumfanyie *vetting*. Meneja akishafanyiwa *vetting* na kuonesha kwamba ni safi, ndiyo ataruhusiwa kuchukua hiyo kazi. (*Makofi*)

Kwa msaada wa Serikali, *SHIRECU* inanunua pamba, imepata mkopo wa shilingi bilioni 2.5 kutoka kwenye Mabenki na hivi sasa inaendelea na kazi hii ya kununua pamba. Vile vile *Nyanza Cooperative Union*, imepata mkopo wa shilingi bilioni 3.5 kutoka kwenye Mabenki na fedha hiyo sasa hivi inanunua pamba.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa gharama za Bodi za Mazao. Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, alizungumzia suala hili na akatoa rai kwamba, pengine gharama za kuendeshea Bodi zingechukuliwa na Serikali mia kwa mia, kusudi yale makato yaliyokuwa yakifanywa na Serikali kulipia hizi Bodi, yaweze kurudi kwa mkulima na kumwongozea mapato yake. Nataka kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, uamuzi huu umekwisha chukuliwa na Baraza la Mawaziri na Bodi zote zitakuwa zinagharamiwa na Serikali kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo, kwa sasa Serikali inafanya zoezi la kurazinisha idadi, majukumu na muundo wa Bodi za Mazao, kukamilika kwa zoezi hili kutatua pia ufumbuzi wa suala la uundaji wa Bodi ya Mazao mchanganyiko. Nataka kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, suala si tuwe na Bodi ya Mazao mchanganyiko, lakini tuwe na Bodi ya aina gani. Hilo ndiyo suala tunalolizungumza kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha napenda kuzungumzia kuhusu hoja hizi mbili; moja ni ya Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kuhusu mali ya iliyokuwa *MBICU*, ambayo ndiyo iko chini ya ufilisi na hoja ya Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kuhusu masoko ya bidhaa zinazozalishwa na vikundi vya akina mama. Nadhani kama ile hoja ya kwanza aliyoizungumzia Naibu Waziri na mimi ningependa sasa nizungumzie suala alilozungumzia Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kuhusu masoko ya bidhaa za vikundi vya akina mama.

Wizara itaendelea na mikakati ya kuwa na mahali maalum pa kuonesha bidhaa kwa mwaka mzima, badala ya utaratibu wa hivi sasa, ambapo vikundi vya akina mama, vinashiriki mara moja katika maonesho na baada ya hapo kutofanya lolote. Utakumbuka kwamba, akina mama bidhaa zote wanazotengeneza wanangojea mpaka Mama Anna Mkapa, awafanyie utaratibu waende kuonesha bidhaa hizo katika Maonesho ya Saba Saba, baada ya hapo wanarudi nyumbani.

Lakini huu utaratibu hauwezi kuwapeleka mbali. Kinachotakiwa ni kuwa na *display centers*, mnakuwa na *sample* katika *center* hizo. Watu wanaopita wanaona bidhaa gani, ziko wapi, akipenda kitu, mna *catalogue* mnajua ni nani anazalisha, basi mnatoa *order* azalishe tani 500 au 2,000 na za aina gani, mnapata *specification*. Bila hiyo, mtaendelea tu kukwama na hiyo itawasaidia kama nilivyosema katika *speech* yangu kwamba, kazi mojawapo ambayo tutaifanya katika mwaka huu unaokuja ni kuwa na *display centers* hizo kusudi akina mama muweze kuonesha bidha zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa na mimi kufuata nyayo, nitoe shukrani kwa watu wa nchi hii, walionifanya nikafika hapa. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, chimbuko la Ushirika tunaoujenga sasa ni mapendekezo ya Kamati ya kumshauri Rais kuhusu kufufua na kueneza Ushirika wa mwaka 2000. Kwa vile fursa kama hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, inaweza kuwa ya mwisho kwangu, napenda niwataje Wajumbe wa Kamati hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Stephen Mashishanga, Mheshimiwa Tarimo, Mheshimiwa Dr. Ladislaus Komba, Mheshimiwa Ibrahim Kaduma, Mheshimiwa Raymond Kimaro, Mheshimiwa Abdul Mushaweji na mimi mwenyewe, Mheshimiwa Balozi George C. Kahama, niliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. (*Makofi*)

Ni vema Kamati hii ikawekwa katika kumbukumbu za kihistoria kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru sana Wajumbe wote, kwa ushirikiano wao, uliozaa kazi nzuri iliyotoa mwelekeo wa Ushirika tunaoujenga kwa sasa. Napenda kuwashukuru vile vite Marais wetu wa Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere na Mzee Ali Hassan Mwinyi, ambao waliniamini kwa kunipa majukumu mbalimbali ya ujenzi wa Taifa wakati walipokuwa katika madaraka. (*Makofi*)

Napenda kuwashukuru Wananchi wa Mkoa wa Kagera, ambao walinchagua kwa mara ya kwanza, kuwa Mbunge wao, Mjumbe wa *LEGCO* wakati ule mwaka 1957, kuwakilisha Mkoa uliojulikana kama *West Lake Province* na wakati huo huo kunipa nyadhifa za *General Manager* wa *Bukoba Native Co-operative Union (BCU)* na Mwenyekiti wa *Bahaya District Council*, nyadhifa zote tatu kwa wakati mmoja. Nawashukuru pia Wananchi wa Jimbo la Karagwe - Kagera, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa miaka 10 mfululizo. (*Makofi*)

Mwisho, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Pius Msekwa, Mbunge na Spika wa Bunge hili Tukufu, kwa kazi nzuri aliyoifanyia Taifa letu hili la Tanzania, pamoja na kazi ya kuendesha Mikutano ya Bunge *with great distinction*. Pia umeimarisha demokrasia katika nchi yetu. Umetufundisha sisi Wabunge utamaduni uliotukuka wa *Westminster Model of Parliamentary Democracy*.

Umeweza kuwafanya Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala na wa Kambi ya Upinzani, kuheshimiana na kukubali ustaarabu wa kupingana bila kupigana. Kwa maoni yangu, kitabu chochote cha historia ya Tanzania kikiandikwa bila kutambua mchango wako wa kuimarisha demokrasia nchini Tanzania, kitakuwa na mapungufu kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawatachia Waheshimiwa Wabunge wote, mafanikio makubwa katika uchaguzi ujao utakaofanyika Octoba, 2005. Nina imani kuwa hawatanisahau katika ufalme wao wakashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko

Kif. 1001 - *Administration and General* .... ... Sh. 1,831,757,700.00

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu na maombi yangu baada ya hoja zangu niliuliza wafanyakazi hao wa *SHIRECU*, ambao hawajalipwa mishahara yao kwa takriban miaka minne watalipwa lini? Amesema wamepata mkopo wa kununua pamba lakini kama utakawakabidhi hawa, hujawalipa mishahara miezi yote hiyo, kweli pamba itanunuliwa *SHIRECU*? Hilo lilikuwa la kwanza. Lakini la pili, wale wanunuzi wa pamba wanaokaa mezani na kupanga bei ya kwenda kuwapunja wakulima, tunafanya nini; kama Serikali, mnachukua hatua gani kwa sababu mkulima hana mahali pa kwenda kutoa kero zake kuzungumza ili asaidiwe? Hatujapata mbadala, sasa tunafanya nini tuache kweli wakulima wapunjwe zao la pamba?

Katika jibu la swalii la jana, Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri alisema ni senti 43 ya dola kwa ratili moja ya pamba nyuzi na uki-convert katika mahesabu utakuta ni shilingi 321 kilo moja ya pamba mbegu. Sasa hata mkiondoa gharama za uendeshaji, huwezi ukamlipa mkulima sasa hivi Sh.200 ndiyo bei inayotembea vijiji.

Wiki jana ilikuwa ni Sh.270 na mpaka mwanzo wa wiki hii. Lakini leo ni Sh.200 na wanazidi kuteremsha na Wizara ipo, sasa mnatusaidiaje wakulima wa pamba? Kwa nini hamtaki kuingilia kati na kusaidia wakulima hawa waendelee kupunjwa na Serikali ipo maana yake tunakwenda wapi? Aaa!! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Danhi Makanga kama ifuatavyo: La kwanza, mishahara ya wafanyakazi, taratibu zilizofanyika ni kwamba, wataanza kulipwa mwezi wa August, yaani mwezi ujao na mkutano umefanyika kati ya *management* na wafanyakazi na wamelewana. Kwa hiyo, sasa hivi halina matatizo. Kwa upande wa hicho anachokiita kupunjwa kwa makusudi na wanunuzi wa pamba, baada ya kusikia mambo aliyoituambia sasa, tumefanya mkutano pamoja na *Managing Director* wa Bodi ya Pamba, yuko hapa na wote tumezasikia. Utafanya uchunguzi wa kutosha, baada ya mkutano huu wiki ijayo na kama tutakuta kwamba, hilo alilolisema ni la kweli basi wote waliofanya ujanja huu, tutawafutia leseni zao. (*Makofit*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi kifungu hicho hicho cha 1001 - Mshahara wa Waziri, ingawa anastaafu. Katika mchango wangu, nilisema kuwa huu mgawanyo baina ya mazao ya biashara ya asilia na yale yasiyokuwa ya asilia, kwa karne hii tunayoenda nayo sasa hivi imepitwa na wakati na unayanyima mazao ya biashara, yasiyokuwa ya asilia, mazao ya mchanganyiko, fursa ya kuendelezwa na hata kuundiwa Bodi ya kuyaendeleza. Sasa nilitegemea Mheshimiwa Waziri, angesemea hili, angetoa kauli kuhusu jambo hili, Wizara yake inasema nini kuhusu mazao yasiyokuwa ya asilia.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Profesa Mwaga, alipoongea leo asubuhi, nilielewa kwamba, yeze tatizo lake lilikuwa la *semantics*, kuelewa kwa nini mazao asilia na yasiyo asilia. Lakini sasa baada ya kutoa ufanuzi kwamba, kwa kweli alikuwa analenga kupata jibu kutoka Serikalini kujua ni lini tutakuwa na Bodi ya mazao mchanganyiko. Nadhani katika hotuba yangu, nimeeleza kwamba, kwa sasa hivi Serikali inafanya rejea ya Bodi zote za Mazao na katika kuhitimisha hoja yangu, nimeeleza hivyo hivyo, kwamba Serikali inafanya rejea ya Bodi za Mazao na *exercise* hiyo ikikamilika, tutaweza kuamua kama tutakuwa na Bodi ngapi na za aina gani. Lakini naweza kumhakikishia kwamba, kama tutakuwa na Bodi ya Mazao mchanganyiko, lakini tutakuwa na Bodi ya aina gani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, akubali kwamba, hiyo inakubalika kimsingi. Sasa tunachotafuta ni Bodi ya namna gani ambayo tutataka kuiunda. Ahsante.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	...	Sh.	382,694,800.00
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	...	Sh.	619,092,200.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Co-operative Development* .... Sh 3,148,069,700.00

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize tu katika maendeleo ya Ushirika. Mheshimiwa Waziri, alisema Meneja aliyechaguliwa anafanyiwa *vetting*, yaani anaangaliwa kwanza. Sasa katika muda mfupi huyu wa Serikali atakabidhi. Lakini hakufafanua ni muda gani? Kwa nini tusiambiwe ni baada ya mwezi au miezi, tujue *time frame* ya huyu Meneja wa Serikali kuendelea kukaa pale na utawawekaje Mameneja wawili *parallel*.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishasema kwamba, mtu anapita katika utaratibu wa *vetting*, huwezi ukatoa muda. Kwa sababu *vetting* inaweza kuwa *negative* vile vile siyo lazima iwe *positive*. Baada ya kufanya *vetting* wanawenza kutoa jibu kwamba, hafai. Kwa hiyo, kusema *vetting* itachukua muda wa miezi mitatu au miwili, nadhani itakuwa kwa kweli tunafanya jambo ambalo siyo la kweli. Sasa nitaeleza sababu, kwa nini tufanye *vetting* hasa kwa huyu mtu waliyemteua.

*SHIRECU* kama nilivyooleza, limepita katika kipindi kigumu kutokana na matatizo ambayo nimeeleza kwa kina wakati nikihitimisha hoja yangu. Nimeeleza pia kwamba, utaratibu uliokuwepo ulikuwa ni kuchaguana kwa kufuata udugu au kufahamiana na wote mnafahamu na Mheshimiwa Danhi Makanga, nadhani anaelewa hilo.

Walishindwa kutoa hata uongozi huo mbovu, ilibidi niende mwenyewe kufanya hiyo kazi. Walichofanya siku ile Shinyanga, walifanya sherehe kwa siku mbili mfululizo ya kusherehekeja jambo hilo lililofanyika. Sasa huyu waliyemchagua hawakutoka nje, walitangaza lakini naye ametoka humo humo ndani.

Kwa hiyo, nikauliza sasa huyu mtu aliyetoka humo humo ndani nataka kujuu, madhambi yote haya yalipokuwa yanafanyika alikuwa wapi?

Hiyo ni lazima njue na kama alikuwemo na akachukia kwa nini hakutoka *hakuresign*, kwa nini aliendelea. Nilitaka njue. Halafu kuna miaka fulani, kilikuwa kinaonesha hajulikani alikuwa wapi. Nilitaka kujuu alikuwa wapi katika kipindi hicho?

Sasa maswali haya yakishajibika basi mtu wenu *a-take over* na kwa sasa hivi siyo rahisi kusema kwamba, kuna *managers* hapana. Meneja ni mmoja, yule mwengine ni mtarajiwa, akipita hiyo *vetting*. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, imeonekana kabisa huyu aliyeteuliwa hawezi kazi na kama Serikali mulikuwa na maelezo mazuri ya namna hiyo kwamba, huyu ametoka humo humo na kulikuwa na matatizo. Sasa kwa nini msifute na kutangaza tena nafasi watu wakaomba. Sasa tunazidi kufanya *vetting* baadaye sijui iweje, sasa *uta-vet* mara ngapi. (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vetting* haijakamilika. Labda kama anataka nimpe jibu la kuridhisha ni kwamba, nitahakikisha kwamba, hiyo *vetting* inakamilika mwisho wa mwezi huu. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4002 - *Marketing Development* ... ... Sh. 1,188,823,500.00

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... Sh. 511,500,000.00

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Bunge Zima na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa mwaka 2005/2006, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirika na Masoko  
yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.30 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Ijumaa  
Tarehe 22 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*